# Nipashe

Jumatano Aprili 17, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0579894

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper







## Walia kupigwa danadana NSSF fao kupoteza ajira

UKURASA 3

UKURASA 13



# Mawaziri wahamia ofisi mpya za mabati

**NI** utekelezaji wa agizo la Rais Magufuli... *ukurasa 2*

## Uhaba wa watumishi serikalini

UKURASA 2





Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, akikagua jengo la ofisi yake kwenye Mji wa Serikali Mtumba, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Waziri akiri ofisi yake ina udhaifu mkubwa

UKURASA 3







**MICHEZO** WANYAMA AIHOFIA TAIFA STARS AFCON UK. 32

MAONI, KATUNI UK.6

## Tanzania hatarini kugeuka jangwa

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira, imeitaka serikali kuchukua hatua haraka kukabiliana na changamoto ya ukataji miti kwenye misitu ili kuinusuru nchi kugeuka jangwa.

Akiwasilisha taarifa ya kamati yake kuhusu makadirio ya bajeti ya Ofisi ya Rais (Mazingira) kwa mwaka ujao wa fedha, Makamu Mwenyekiti wa kamati hiyo, Kanali Mstaafu Masoud Ali Khamis, alisema takwimu za ufyekaji wa misiti nchini zinatisha.

"Utafiti unaonyesha msitu wenye ukubwa wa kiwanja cha mpira wa miguu hufyekwa kila baada ya dakika moja, takwimu hizi zimeipeleka Tanzania kuwa katika orodha ya nchi tano za juu zinazoongoza kwa ukataji wa misitu duniani," alisema.

Kiongozi huyo wa kamati pia alisema utafiti unaonyesha kuwa asilimia 61 ya nchi iko hatarini kugeuka jangwa, akiitaja baadhi ya mikoa iliyoathirika zaidi kuwa ni Dodoma, Singida, Shinyanga, Simiyu, Manyara na baadhi ya maeneo ya Mkoa wa Kilimanjaro.

Alisema Tanzania pia imeingia katika orodha ya nchi zenye uhaba wa maji kulinganisha na mahitaji, akieleza kuwa hali hiyo ni moja ya viashiria vya uharibifu wa mazingira katika vyanzo vya maji.

"Pia, baadhi ya maziwa yako katika hatari ya kupotea. Baadhi yake ni Ziwa Manyara, Jipe na Chale. Kupotea kwa maziwa haya kwa kiasi kikubwa kumechangiwa na shughuli za kibinadamu zinazoendeshwa katika maeneo ya ziwa ambazo hupelekea uharibifu wa mazingira," alisema.

Alisema kamati yake inaishauri serikali kuchukua hatua za makusudi kuinusuru nchi kutokana na athari zitokanazo na uharibifu wa mazingira.

"Serikali ilipe uzito suala la uhifadhi wa mazingira kwa kutenga fedha za maendeleo na kuzipeleka kwa wakati, kwa sasa asilimia kubwa ya miradi ya maendeleo ya mazingira inatekelezwa kwa kutumia fedha za wafadhili, jambo ambalo si sahihi sana.

"Kwa mfano, hadi kufikia robo tatu ya mwaka, fedha za ndani kwa ajili ya miradi ya maendeleo zilikuwa hazijatolewa kabisa," alisema.

# Mawaziri wahamia ofisi mpya za mabati

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

AGIZO la Rais John Magufuli limesababisha Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, na wasaidizi wake kuhamia kwenye ofisi za mabati mjini Dodoma.

Jaffo na manaibu waziri wake wawili, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu pamoja na watumishi wengine wamelazimika kuhamia kwenye ofisi za muda za mabati hayo kutekeleza agizo lililotolewa na Rais Magufuli mwishoni mwa wiki.

Jengo la ghorofa mbili la wizara hiyo lililopo kwenye mji wa serikali uliopo Mtumba jijini hapo halijakamilika, hali iliyomkera Rais Magufuli ambaye aliwataka wahamie hivyo hivyo.

Mbali na mawaziri hao, pia baadhi ya Idara muhimu za wizara hiyo zimehamia kwenye ofisi hizo za mabati, huku mafundi wakiendelea na ujenzi wa jengo ambalo walipaswa kuwamo.

Rais Magufuli mwishoni mwa wiki alizindua mji huo ambapo aliagiza wizara zote 23 kuhakikisha zinahamia eneo hilo zikiwamo tatu ambazo hazijakamilisha majengo yake.

Akizungumza na Nipashe jana, Jafo alisema walihamia tangu Jumatatu yeye pamoja na manaibu wake, Katibu Mkuu na baadhi ya idara muhimu.

Alisema wanaendelea kutekeleza majukumu yao katika ofisi yao hiyo mpya, huku mafundi wakiendelea na ujenzi ambao unatarajiwa kukamilika Mei 30, mwaka huu.

"Sisi tumehamia kama ambavyo tumetakiwa kuhamia na tunaendelea na shughuli zetu hapa sisi tupo tayari kufanya kazi kwenye mazingira yoyote," alisema.

Alisema ofisi hiyo haijakamilika sawasawa, lakini ameamua kuingia hivyo hivyo.

"Nilipokuwa nakuja hapa, kuna watu walikuwa wananishangaa wakiwamo mafundi wetu ambao waliniambia ofisini kuna joto, mimi najiona nipo sawa," alisema.

Jafo alisema yeye anashinda vijijini kukagua miradi ya maendeleo hivyo katika mazingira hayo ya sasa ya mabati anaona ni jambo la kawaida tu.

Hata hivyo, Jaffo alisema jengo lake ni kubwa la ghorofa mbili na ni miongoni mwa majengo ya kisasa ambayo baada ya kukamilika litakuwa linavutia.

Jafo alisema litakuwa na uwezo wa kuchukua watumishi 88, kutakuwa na kumbi mbili za mikutano ambao mmoja utachukua watu 25 na ukumbi mkubwa utakuwa na uwezo wa kuhudumia watu 60.

"Mikutano yote ya kiofisi, tutakuwa tukiifanyia hapa, watu wanaweza kujiuliza ni kwanini Tamisemi tuliamua kujenga jengo la ghorofa tofauti na wizara zingine, ni waambie tu hii wizara ina watumishi wengi kuliko wizara zote," alisema.

Alibainisha kuwa baada ya serikali kutoa kiasi cha Sh. bilioni moja waliwasiliana na Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) ambao walichora ramani kulingana na fedha walizopewa.

Jafo alisema ujenzi huo unafanywa na Chuo

INAENDELEA UK 8



Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), Dk. Hussein Mwinyi (kulia), Balozi wa China nchini, Wang Ke (kushoto) na Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama, Jenerali Venance Mabeyo (wa pili kushoto), Msaidizi Ofisi ya Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, Geofrey Mponda (katikati) na Mnadhimu Mkuu wa Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), Luteni Jenerali Yakubu Mohamed, wakizindua jiwe la msingi kwa ajili ya ujenzi wa Chuo cha Ulinzi cha Taifa (NDC), jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

# CAG: Kuna uhaba mkubwa watumishi serikalini

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

MDHIBITI na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Prof. Mussa Assad, amebaini changamoto ya uhaba wa watumishi serikalini.

Katika ripoti yake ya ukaguzi wa mwaka wa fedha 2017/18 iliyowasilishwa bungeni na serikali Jumatano iliyopita, CAG Assad anabainisha ameangalia kwa mara nyingine tena changamoto ya uhaba wa watumishi katika taasisi mbalimbali.

Katika ripoti yake hiyo, Prof. Assad anabainisha kuwa changamoto hiyo ina athari kubwa katika utoaji wa huduma na ufanisi wa taasisi.

"Mapitio niliyofanya katika ofisi kama za wizara, wakala, sekretarieti za mikoa na balozi 62 yanaonesha kwamba watumishi waliopo ni 9,714 ukilinganisha na mahitaji ya watumishi 19,469, hali ambayo inapelekea upungufu wa watumishi 9,755, sawa na asilimia 50.1 ya mahitaji," Prof. Assad anabainisha katika ripoti yake hiyo.

"Kuendelea kwa tatizo hili kunahatarisha utendaji kazi wa taasisi ikiwamo utoaji wa huduma hafifu kutokana na mlundikano wa kazi na kuchoka kwa watumishi waliopo.

"Ukilinganisha na taarifa yangu ya ukaguzi uliopita (2016/17), upungufu wa watumishi unaonekana kushuka kutoka watumishi 34,081 katika taasisi 52 kwa ukaguzi uliopita hadi kufikia watumishi 9,755 katika taasisi 62 katika mwaka huu wa ukaguzi, hii ina maana ya kuwa nafasi zilizowazi bado zinaendelea kujazwa.

"Nawashauri maofisa masuuli wote kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi Umma na Utawala Bora kujaza nafasi zilizowazi au kufanya upya mapitio ya uhitaji wa watumishi ukilinganisha kwa watumishi waliopo na huduma zinazotakiwa kutolewa.

**HAKUNA MAFUNZO**

Katika ripoti yake hiyo, CAG Assad pia anabainisha changamoto ya kutozingatia mafunzo kwa watumishi, akieleza kuwa Kanuni namba G.1 (7) ya Kanuni za Kudumu za Watumishi wa Umma za Mwaka 2009 inasema kuwa, taasisi zote zinatakiwa kuandaa mafunzo maalum kwa watumishi waliopo kazini kwa kuzingatia mahitaji ya mafunzo yaliotambulika wakati wa utendaji kazi zao.

"Kila taasisi itatakiwa kutenga bajeti katika mwaka wa fedha kwa ajili ya mafunzo.

"Nilipopitia nyaraka katika taasisi mbalimbali, niligundua kuwa kuna taasisi tano hazikufanya tathimini ya mahitaji ya mafunzo wala kuwapo kwa mpango wa mafunzo kwa watumishi waliopo kazini," Prof. Assad anaeleza katika ripoti yake hiyo.

Anaitaja taasisi alizobaini zinakabiliwa na changamoto hiyo kuwa ni Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mamlaka ya Kuzuia Dawa ya Kulevya, Wizara ya Katiba na Sheria, Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa na Tume ya Kudhibiti Ukimwi.

CAG Assad anasema kukosekana kwa tathmini ya mahitaji ya mafunzo na kutofanya mafunzo kwa watumishi kunahatarisha ufanisi wa taasisi husika kwa kuwa watumishi watashindwa kujiendeleza katika utendaji wao wa kazi kuendana na uhitaji wa wakati huo kama vile maboresho ya taratibu mbalimbali, kutumia vifaa vipya vilivyoanzishwa na taasisi na mabadiliko ya sheria.

"Hivyo ninawashauri maofisa masuuli wote kufanya tathmini ya uhitaji wa mafunzo kwa watumishi, kuandaa mpango wa mafunzo kwa watumishi wake kulingana na udhaifu ulioonekana kwa watumishi hao wakati wa utendaji wao wa kazi, kuandaa bajeti na kutekeleza mpango wao wa mafunzo kwa ajili ya uhai wa utoaji huduma katika taasisi," Prof. Assad anapendekeza katika ripoti yake hiyo.

## HABARI KITAIFA

# Walia kupigwa danadana fao kupoteza ajira NSSF

**Na Salome Kitomari**



BAADHI ya wanachama wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), wamelalamika kupigwa danadana ya kulipwa fedha za mafao ya upotevu wa ajira na michango yao ya kujitoa uanachama kwa muda mrefu bila mafanikio.

Wanachama hao wamedai kujikuta wote wakiambiwa sababu zinazofanana kuwa walikosea kuweka alama ya dole gumba, kuwapo kwa tatizo la mtandao na wasimika mfumo mpya kwa kushirikiana na Hazina.

Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti, mwanachama hao wameilalamikia ofisi ya NSSF Ubungo, kwa usumbufu wanaopata kila siku wa kupewa sababu mpya za kuchelewa kulipwa haki yao kisheria.

Mmoja wa wanachama hao ambaye hakupenda jina lake liandikwe gazetini, aliiambia Nipashe kuwa mkataba wake wa kazi ulikwisha Julai mwaka 2018, alifungua maombi ya malipo na ilipofika Novemba mwaka huo, aliambiwa hawezi kulipwa michango yake, badala yake anatakiwa kufungua fao la upotevu wa ajira ambalo alifungua Desemba 11, mwaka huu.

Alisema walimwambia kuwa hajafikisha umri wa kustaafu hivyo hawezi kulipwa na badala yake anastahili fao la upotevu wa ajira.

Alisema alionana na Meneja wa NSSF Ubungo, kumuuliza lini atalipwa kama rais alivyoagiza Desemba mwaka jana, lakini aliambiwa kuwa wanafuata Sheria ya Mafao.

Alisema alifungua madai ya fao la upotevu wa ajira Desemba 11, 2018, alitakiwa kurudi Januari 10, mwaka huu, na Januari 15, mwaka huu, atakuwa ameanza kulipwa, lakini alienda benki na hakukuta fedha yoyote.

"Niliangalia, lakini sikukuta fedha, nilikwenda kwao wakaniambia walikuwa na kazi nyingi hawajaweza kushughulikia faili langu, na wanalipa za watu wa mwaka jana, nikawauliza nije lini wakaniandikia Machi 16, mwaka huu (jana)," alisema.

"Nategemewa na zaidi ya watu 10 akiwamo mke na watoto watano, kuninyima stahiki zangu maana yake ni kuniangamiza ili haki yangu ipotee," alisema.

Alisema juzi wanachama wote waliofuatilia walikusanywa kwenye ukumbi na kutangaziwa mabadiliko ya tarehe za kulipwa.

Alisema Machi 21, mwaka huu, aliandikia Mamlaka ya Usimamizi na Udhibiti wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii (SSRA), kueleza usumbufu anaokutana nao licha ya kutokuwa na ajira kwa takribani miezi saba na hawezi hata kutumia huduma za matibabu na sababu wanayomweleza ni kwa kuwa hachangii kwa sasa.

Machi 25, mwaka huu, SSRA walimjibu kupitia barua yenye kumbukumbu Na: DB. 154/541/13/69, iliyosaniwa na Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa SSRA, Kitandu Ugula, ambaye

INAENDELEA UK 8

## Ushahidi kesi kina Mbowe kuanza leo

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam imesema itaanza kusikiliza leo ushahidi wa Jamhuri wa kesi ya uchochezi na kufanya mkusanyiko usio halali inayowakabili vigogo tisa wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), akiwamo Mwenyekiti Taifa, Freedman Mbowe.

Kesi hiyo ilipangwa kuanza kusikilizwa shahidi wa kwanza wa Jamhuri jana katika mahakama hiyo iliyoketi chini ya Hakimu Mkazi Mkuu, Thomas Simba.

Jopo la upande wa Jamhuri likiongozwa na Wakili wa Serikali Mkuu, Faraja Nchimba, akisaidiana na mawakili wa serikali, Wankyo Simon, Jacquline Nyantori na Salim Msemo, lilidai kuwa mashahidi wawili wako tayari kuendelea.

Hata hivyo, jopo la mawakili wa utetezi likiongozwa, Prof. Abdallah Safari, Peter Kibatala, Hekima Mwasipu, Jeremia Mtobesya na John Mallya, liliwasilisha barua ya kuomba ruhusa kutoka kwa mshtakiwa wa sita Dk. Vicent Mashinji.

Profesa Safari alidai alisoma barua ya mshtakiwa kwenda kwa mahakama kwamba; "Anaomba ruhusa

INAENDELEA UK 8



Spika wa Bunge, Job Ndugai (kushoto), akisalimiana na Mwakilishi wa Umoja wa Afrika kutoka Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO), David Phiri, kabla ya kufungua Mkutano wa Umoja wa Wabunge wa Afrika ya Mashariki wa kuangalia Usalama wa Chakula na Lishe, jijini Arusha jana. Katikati ni Mwakilishi wa Shirika hilo, nchini, Fred Kafeero. **PICHA: OFISI YA BUNGE**

## Waziri akiri udhaifu mkubwa wizarani

**Na Enock Charles**

WAZIRI wa Viwanda, Biashara, Joseph Kakunda, amesema wizara yake ina udhaifu mkubwa katika kusimamia utekelezaji wa sera zilizo chini ya uratibu wake kutokana na kukosa uwakilishi wa kitaalamu kwa sekta ya viwanda kwenye sekretarieti za mikoa na halmashauri.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, waziri huyo alisema ukosefu wa maofisa wa viwanda katika mikoa na halmashauri kumesababisha udhaifu kwenye upatikanaji wa taarifa sahihi kuhusu usajili wa viwanda na leseni za viwanda, uwezo wa viwanda wa uzalishaji, idadi ya wafanyakazi, shehena zilizouzwa ndani ya nchi, zilizouzwa nje ya nchi na zilizo kwenye maghala.

"Napenda nikiri wizara yangu ina udhaifu mkubwa katika kusimamia utekelezaji wa sera zilizo chini ya uratibu wake," alisema Waziri Kakunda.

"Ni vizuri utaratibu wa utekelezaji wa majukumu ikiwamo takwimu za viwanda uanzie kwenye halmashauri, mkoa ndipo uje makao makuu ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa kuratibiwa na Tamisemi," aliongeza.

Pia aliagiza Shirika la Viwango nchini (TBS), Wakala wa Vipimo (WMA) na Tume ya Ushindani (FCC), kufanya mapitio ya kanuni ili kupunguza viwango vya tozo wanazowatoza wenye viwanda na wafanyabiashara na

INAENDELEA UK 8


### UCHUMI COMMERCIAL BANK LIMITED

### EXPRESSION OF INTEREST

1. Uchumi Commercial Bank intends to cover eligible payments under the contract for which this invitation for quotation is issued.
2. You are hereby invited to submit your application for supplying the goods as described in the Schedule of Requirements.

| LOT | Tender identification no. | Type of requirement |
|---|---|---|
| 1 | UCB/207/001/2019 | Supply of Firewall |
| 2 | UCB/207/002/2019 | Supply of Server Ram |
| 3 | UCB/207/003/2019 | Supply of Server Hard Disk |
| 4 | UCB/207/004/2019 | Supply of Licenses |
| 5 | UCB/207/005/2019 | Supply of Laptops |
| 6 | UCB/207/006/2019 | Supply of External Hard Disk |
| 7 | UCB/207/007/2019 | Supply of Server |
| 8 | UCB/207/008/2019 | Supply of Desk top PC |
| 9 | UCB/207/009/2019 | Supply of Data Cabinet |
| 10 | UCB/207/010/2019 | Supply and installation of CCTV auto backup |
| 11 | UCB/207/011/2019 | Supply and installation of office furniture |
| 12 | UCB/207/012/2019 | Supply and installation of note counting and binding machine |
| 13 | UCB/207/013/2019 | Supply and installation of plastic card printer |
| 14 | UCB/207/014/2019 | Supply and installation of power backup solution |
| 15 | UCB/207/015/2019 | Supply of custom thermal receipt paper roll |
| 16 | UCB/207/016/2019 | Provision of interior construction and design of office services for the Uchumi commercial bank |

**Note: Bidders may opt for one or more lots.**

3. Interested firms must provide information indicating that they are qualified to provide the above services by submitting its profile, description of similar assignments for the past four (4) years with recommendation/reference letters from major companies, experience, financial capacity and availability of appropriate skills among staff and business partners/sub-contractors that will be engaged in the project.
4. A shortlist of firms will be developed on the basis of the Expression of Interest submitted to Uchumi Commercial Bank Ltd. Initial short listing shall be conducted based on technical capabilities, experience and skills after which, the Bank may opt to call for competitive presentation of previous similar assignments, experience and capabilities and due diligence to sites and offices.
5. Deadline for submission will be on 14 days after the date of advertisement.
6. All quotations in one original plus 2 copies, properly filled in, and enclosed in plain envelopes marked, Request for the expression of interest for any of the lots above and must be delivered to;

**Uchumi Commercial Bank Ltd Head office,**
**E.L.C.T ND Building, Market Street,**
**P.O. Box. 7811 MOSH**

215182402

# TCRA kufunga laini za simu za watu wakaidi

**Na Happy Severine,** SIMIYU

MAMLAKA ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), imesema kuwa itawafungia laini zao za simu watu wote watakaoshindwa kuzisajili kwa mfumo mpya wa alama za vidole yaani Biometric Registration.

Mamlaka hiyo imesema kuwa muda wa ukomo utakapotangazwa hakutakuwa na msaada wowote na badala yake watazifungia mawasiliano laini zote zitakazokuwa hajazisajiliwa kwa mfumo huo.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Meneja wa Mamlaka hiyo, Kanda ya Ziwa, Mhandisi Francis Mihayo, katika uzinduzi wa kampeni ya kutoa elimu kwa wananchi juu ya mfumo huo uliofanyika mjini Bariadi, mkoani Simiyu.

Mihayo alisema usajili wa laini zote kwa mfumo huo utaanza rasmi Mei mosi, 2019, wananchi watatakiwa kwenda kwa watoa huduma wa mitandao mbalimbali ya simu kwa ajili ya kusajiliwa.

“Mwezi Mei, ndiyo tutaanza rasmi kusajili laini zote upya kwa kutumia mfumo huu, lakini ukomo wa zoezi hilo bado hatujatangaza, hivyo wananchi wajitokeze kwa wingi kwenda kusajili laini zao,” alisema Mihayo.

Aidha, alisema lengo la TCRA kuja na mfumo huo ni kutokana na kuwapo kwa idadi kubwa ya wananchi waliosajili laini kwa kutumia vitambulisho bandia.

“Katika mfumo huu kitambulisho kimoja tu cha NIDA ndicho kinachohitajika hasa namba ya kitambulisho hicho, tofauti na zamani waliporuhusu vitambulisho vitano,” alisema Mihayo.

“Kwa kutumia vitambulisho hivyo udanganyifu ulikuwa mkubwa hali iliyosababisha ugumu kwa TCRA kudhibiti vitendo vya uhalifu kwa kutumia mtandao,” aliongeza Mihayo.

Akizindua kampeni hiyo, Mkuu wa Wilaya ya Bariadi, Festo Kiswaga, aliwataka wananchi wa wilaya hiyo kujitokeza kwa wingi kusajili laini zao upya kwa mfumo huo huku akiwataka kwenda na vitambulisho vya NIDA.

Baadhi ya wananchi walisema mfumo huo ni mzuri, lakini changamoto ya upatikanaji wa vitambulisho na namba kwa madai kuwa baadhi yao hawana.

## WB: Idadi ya wategemezi Tanzania yaongezeka

**Na Salome Kitomari**

BENKI ya Dunia imesema kuwa idadi ya wategemezi kwa Tanzania inazidi kuongezeka ikilinganishwa na wenye ajira rasmi, kutokana na kupungua kwa ajira rasmi.

Aidha, ajira zisizo rasmi kwenye maeneo ya viwanda na huduma zimeongezeka ikilinganishwa na utoaji wa huduma.

Kiongozi wa uchumi na mradi wa ukuaji wa usawa wa uchumi na taasisi katika nchi za Burundi, Malawi, Somalia na Tanzania, Dk. Yutaka Yoshino, aliyasema wakati akiwasilisha ripoti ya jinsi ya kuuendelea uchumi wa kati iliyotolewa na WB.

Akiwasilisha ripoti hiyo jana jijini Dar es Salaam, mbele ya waandishi wa habari, alisema miaka ya 90 nchi 17 zilikuwa katika uchumi wa chini, lakini baadhi ya nchi zimejikwamua kutokana na mabadiliko kwenye sekta mbalimbali ambazo ni injini ya uchumi ikiwamo sekta binafsi.

Akichambua ripoti hiyo kwa kuziangalia nchi za Tanzania, Bangladesh na Vietnam, Dk. Yoshino, alisema mwaka 1990 nchi hizo zilikuwa na uchumi sawa kwenye pato la mtu mmoja mmoja (Per capital income).

Alisema ongezeko la watu linapaswa kwenda sambamba na ukuaji wa Pato la Taifa, na nchi za Bangladesh na Vietnam ziliweza kudhibiti ongezeko la watu kwa miaka 20 iliyopita ikilinganishwa na Tanzania ambako kuna ongezeko kubwa la

INAENDELEA UK 8

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA,
Tarehe 16/04/2019.

TANGAZO

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya Alhamisi tarehe 18/04/2019 kampuni ya S.S.F Co.LTD itasafirisha mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka DAR kuelekea KAGERA gari hilo lenye namba za usajili:
   **T871 DHC/T 298 BXS.**
2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:
   **Urefu - mita 21.5**
   **Upana - mita 3.2**
   **Kimo - mita 5.2**
3. NJia itakayotumika DAR hadi KAGERA kupitia MWENDAKULIMA gari litasafiri muda wa mchana tu(kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)

Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.

215183802



Mafundi wakiendelea na ujenzi wa mifereji ya maji ya mvua katika eneo la Sinza Kijiweni, Manispaa ya Ubungo, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOHN BADI**

## Makonda atimiza ahadi ya kusomesha wasichana 100

**Na Mary Geofrey**

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda, ametimiza ahadi yake aliyoitoa hivi karibuni ya kusomesha wasichana 100 wa masomo ya Sayansi, waliofaulu kidato cha nne, lakini familia zao hazina uwezo wa kuwasomesha.

Makonda alitimiza ahadi hiyo jana, baada ya kukabidhiwa hundi ya Sh. milioni 20 na Balozi wa Falme za Kiarabu, Khalifa Abdul-Ragman Al-Marzoo.

Makonda alisema aliomba msaada kwa balozi huyo ambaye alikubaliana na wazo lake la kuwasomesha wanafunzi hao 100 wa mkoa wa Dar es Salaam.

“Huu ni msaada, niliomba nikapewa kwa ajili ya wanafunzi wa kike, ombi langu kwa watendaji ambao mtawatafuta wanafunzi hawa, msije mkawapachika ndugu na jamaa zenu ambao wana uwezo hii itakuwa ni laana kwenu,” alionya Makonda.

Alisema katika kila wilaya watatoka wanafunzi 20 wa mkoa huo na atawasomesha katika shule za ndani na nje ya mkoa wao.

“Rais Magufuli amejitahidi kutoa elimu bure kwa wanafunzi hawa wa shule za msingi hadi sekondari kwa kutambua mchango wanafunzi wa kike ambao wanafaulu vizuri, lakini wazazi au ndugu zao hawana uwezo wa kuwasomesha, nimejitolea kuwatafutia ufadhili wa masomo,” alisema Makonda.

Aliahidi kuwa wanafunzi hao atawasomesha hadi kidato cha sita na kwamba kila mwaka ataendelea kujitolea kuwatafutia ufadhili wanafunzi wengine.

Balozi Al-Marzoo, alimpongeza Makonda kwa juhudi zake za kusaidia watoto wa kike katika masomo ya Sayansi ili kupata elimu.

Alisema Falme za Kiarabu zinashirikiana na Tanzania katika masuala mbalimbali ya kusaidia jamii ikiwamo ufadhili wa masomo.

Alisema amependa kusaidia wasichana hao 100 ambao wamefaulu kidato cha nne na hawana uwezo wa kuendelea na masomo kwa sababu anaamini wakipata elimu watakuja kusaidia jamii.

Mbali na hilo, Makonda alisema amemshauri Katibu Mkuu wa Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), kuwabadili wakuu wa idara ambao wamekuwa wakikwamisha miradi ya maendeleo kwa sababu zisizo na mashiko.

Pia aliiagiza Halmashauri ya Manispaa ya Ilala, kumnyang’anya mkataba, mkandarasi aliyepewa kazi ya kujenga mitaro katika bonde la mto Msimbazi kutokana na kile kinachodaiwa kufungiwa ufadhili na moja ya benki kubwa.

## HABARI KITAIFA



Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Anna Henga (kushoto) na Balozi wa Norway nchini, Elisabeth Jacobsen, wakibadilishana hati baada ya kusaini makubaliano ya ushirikiano, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Mkuchika amiminiwa sifa kukemea ubabe ma-DC, RC

**Na Salome Kitomari**

MTANDAO wa Watetezi wa Haki za Binadamu (THRDC), umempongeza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Mkuchika, kwa kuwaelekeza wakuu wa wilaya na mikoa kuacha kutumia vibaya madaraka yao kuwaweka kizuizini raia bila kufuata matakwa ya sheria.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Mratibu wa THRDC taifa, Onesmo Olengurumwa, Sheria ya Tawala za mikoa ya mwaka 1997, inawapa mamlaka ya kuwaweka watu wanaotenda kosa la jinai au kuvunja amani ndani ya saa 48 na siyo vinginevyo.

"Kwa mujibu wa kifungu cha 7(5) cha sheria hii, ni lazima Mkuu wa Mkoa au Wilaya anayemuweka kizuizini raia aandike maelezo ni kwanini amemuweka ndani raia huyo.

"Sio mnadaiana madeni mnaanza kuwekana ndani...haiwezekani," alisema Waziri Mkuchika.

Olengurumwa alisema kutokana na vitendo hivyo vya baadhi ya viongozi hao, mara kadhaa THRDC imewahi kutoa malalamiko na kuitaka serikali kukomesha ukiukwaji huo wa sheria.

Alisema ipo mifano kadhaa juu ya uvunjifu wa haki unaofanywa na baadhi ya wakuu wa mikoa na wilaya na kwa mara kadhaa wamewahi kuunga mkono kauli za viongozi waliowahi kukemea vi-



tendo vya viongozi hao kukiuka haki za binadamu.

Aidha, alisema baadhi ya kauli hizo ni kama za Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Suleiman Jaffo, na Katibu Mkuu wake waliowahi kutoa maelekezo kama haya mwaka 2018.

"Huu ni muendelezo wa kupigania haki ambao THRDC na wanachama wetu tumekuwa tukiendelea kupigania. Hata hivyo matukio haya yameonekana kuendelea kushamiri na hivyo tunaomba kauli ya waziri wa utawala bora sasa iheshimiwe pamoja na maelekezo ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali," alisisitiza.

Kwa mujibu wa Mratibu huyo, waziri ameishatamka wazi kwamba Mkuu wa mMoa au wa Wilaya atakayekiuka sheria achukuliwe hatua yeye binafsi na Mwanasheria Mkuu wa Serikali asihusishwe kwenye kesi hiyo.

# Muhimbili kumtibu bure mwenye ugonjwa wa ajabu

**Na Mary Geofrey**

HOSPITALI ya Taifa ya Muhimbili (MNH), imejitolea kumtibu bure Mariam Rajab (25), mkazi wa Mtaa wa Minga, Kata ya Mnung'una, mkoani Singida, ambaye anasumbuliwa na kidonda kikubwa mgongoni.

Juzi ujumbe mfupi wa video ulisambaa kwenye mitandao ya kijamii, ukimuonyesha msichana huyo akiomba msaada wa nauli ya kutoka Singida kwenda Muhimbili kwa ajili ya kufuata matibabu ya ugonjwa huo ambao haujulikani.

Ofisa Uhusiano wa Muhimbili, Aminiel Eligaesha, aliwaeleza waandishi wa habari jana kuwa, baada ya kupata ujumbe huo wa video, walimfuatilia msichana huyo na kufanikiwa kumpata kwa ajili ya kuja jijini Dar es Salaam kwa matibabu.

"Asante kwa waliosambaza ujumbe huu ambao ulitufikia Muhimbili, nimefanikiwa kumpata huyu dada anaitwa Mariam Rajab atasafiri kesho (leo) kutoka Singida kuja Dar es Salaam kwa ajili ya kuja Muhimbili kupata matibabu," alisema Eligaesha.

Eligaesha alisema amezungumza na msichana huyo ambaye historia yake inasikitisha hivyo baada ya kupatiwa matibabu atapata fursa ya kujielezea.

"Huyu msichana ana mahitaji mengi sana, tuache afike apatiwe matibabu, mtapata kufahamu historia yake inayogusa sana, nina imani watu wengi wataguswa kumsaidia," alisema Eligaesha.

Ujumbe mfupi wa video uliosambaa kwenye makundi mengi ya Whatssap ulimuonyesha msichana huyo akionyesha kidonda kikubwa chenye uvimbe kilichopo nyuma ya bega lake.

Alisema anaishi katika familia masikini ambayo haiwezi kumtibu kidonda kikubwa kinachomsumbua mgongo kwake karibu na bega.

"Naombeni msaada wenu, nahitaji msaada wa nauli kwa ajili ya kwenda Hospitali ya Muhimbili kwa ajili ya kutibiwa kidonda kikubwa kilichopo mgongoni, sina cha kuwalipa Mungu awabariki," alieleza msichana huyo kwenye ujumbe huo wa video.

# Afa maji akiogelea bwawa la umwagiliaji

**Na Steven William MUHEZA**

MKAZI wa Kijiji cha Misozwe, wilayani Muheza, mkoani Tanga, Elinani John (22), amefariki dunia baada ya kuzama katika bwawa la maji wakati akiogelea.

Tukio hilo lilitokea juzi na kuthibitishwa na Kamanda wa Polisi Mkoa wa Tanga, Edward Bukombe.

Akizungumza na Nipashe, Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Misozwe, Andrew Elangwa, alisema kijana huyo alifariki dunia wakati akiogelea katika bwawa la kilimo cha umwagiliaji la kijiji cha Misozwe.

Alisema siku ya tukio kijana huyo aliwasindikiza wenzake ambao ni waumini wa Kanisa la Pentekoste kwenda kubatizwa katika bwawa hilo la umwagiliaji.

Alisema kuwa baada ya waumini hao kumaliza kubatizwa walishauriana wabaki katika bwawa hilo waendelee kuogelea.

Elengwa alisema vijana hao walianza kuogelea, lakini kwa bahati mbaya mwenzao alizidiwa na maji na hatimaye kuzama ndipo wenzake walipotimua mbio.

Alisema vijana hao walitoa taarifa kuhusu mwenzao kuzama ndani ya bwawa hilo ambapo wananchi walifika na kuanza kumtafuta.

Alisema alipatikana siku ya pili akiwa amefariki dunia na kwamba taratibu za kusafirisha mwili huo zinaendelea kumpeleka kwao Moshi, mkoani Kilimanjaro.




Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Elimu kwa wavuvi ya zana bora hatua nzuri

**TAARIFA** kuwa serikali imezindua mafunzo kwa wavuvi yenye lengo la kuzifahamu zana za uvuvi zinazoruhusiwa kwa mujibu wa sheria, ni za kutia moyo.

Pia ilielezwa mafunzo hayo yanalenga kutambua fursa zilizopo katika sekta hiyo na hatimaye kuleta tija kwa maisha yao na ukuaji wa uchumi wa taifa.

Alizindua mafunzo hayo kitaifa katika mwalo wa Kilindoni, Mafia mkoani Pwani, Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina, alisema kutokana na wavuvi wengi kukumbwa na changamoto nyingi, wizara yake imeanzisha mafunzo hayo ili kujenga uelewa wa pamoja na kuondoa kasoro zilizopo.

Mpina alisema pia watafundishwa juu ya matumizi ya zana bora za kisasa za uvuvi, namna ya kuandaa samaki na kuwahifadhi ili kupunguza hasara ya mavuno pamoja na fursa za masoko, utunzaji wa mazingira ili kulinda ikolojia na bioanuai zilizopo majini ili kuwa na uvuvi endelevu.

Kadhalika, alisema wavuvi watafundishwa namna ya kuanzisha vikundi vya wavuvi ili kurahisisha upatikanaji wa mikopo, watafundishwa ufugaji wa samaki kwenye mabwawa na vizimba na biashara zingine mbadala ili kuongeza kipato na kupunguza nguvu ya uvuvi.

Vilevile, watafundishwa kuzielewa Sheria za Uvuvi ikiwamo Sheria ya Uvuvi Namba 22 ya mwaka 2003, Sheria ya Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu Namba 29 ya mwaka 1994 na Kanuni zake za mwaka 2009 pamoja na Sheria ya Bahari Kuu Cap 388 na kanuni zake za mwaka 2007 na 2016 ili kufahamu kwa kina mambo yanayoruhusiwa na yasiyoruhusiwa.

Kutokana na mafunzo hayo, alisema watafahamu pia suala la urefu na uzito wa samaki anayeruhusiwa kuvuliwa, vipimo vya nyavu zinazoruhusiwa na taratibu nyingine kwa mujibu wa sheria ili kuepuka kuingia kwenye mkono wa sheria.

Hatua ya kuandaa mafunzo hayo kwa wavuvi imechukuliwa wakati mwafaka kutokana na mkakati ulioanzishwa na kutekelezwa na serikali ya awamu ya tano wa kuhakikisha rasilimali za nchi zinalindwa ili zilinufaishe taifa.

Katika kuhakikisha kuwa lengo hilo linafikiwa, serikali imekuwa ikitekeleza operesheni mbalimbali kwa kutumia sheria zilizotajwa hapo juu kuhakikisha shughuli zote za uvuvi unaokiuka sheria zinadhibitiwa, huku wahusika wakikamatwa na kuchukuliwa hatua za kisheria.

Baadhi ya hatua ambazo zimeendelea kuchukuliwa ni ya kukamata na kutaifisha nyavu zisizofaa ambazo zinachangia uvuaji wa samaki wadogo, kukamata na kutaifisha samaki wenye uzito mdogo, kuwakamata na kuwafungulia kesi wanaojihusisha na vitendo vya uvuvi haramu.

Matokeo ya operesheni hizo yameleta matokeo chanya. Kwa mfano, hivi sasa katika maeneo mengo wanavuliwa samaki wenye uzito unaoruhusiwa, na vilevile inaelezwa kuwa upatikanaji wa samaki umeongezeka.

Tunaziunga mkono hatua hizo zinazochukuliwa na serikali kudhibiti utoroshaji wa samaki kwenda nje bila kulipa mapato ya serikali pamoja na vitendo vyote vya uvuvi usiozingatia sheria za nchi.


Tunaona kuwa hatua ya kuendesha mafunzo kwa wavuvi itawawezesha kuwa na uelewa wa kutosha kuhusu uvuvi bora hususan zana zinazopaswa kutumika pamoja na sheria na kanuni zinazoongoza shughuli za uvuvi.

Tunaelewa kuwa baadhi ya mambo ambayo yamekuwa yakichochea uvuvi haramu, ni kukosekana kwa elimu kwa wavuvi wengi. Tunaamini mafunzo hayo yatawafikia wavuvi wengi zaidi nchini.


Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com


## Muungwana Lazima Nilonge



# Pongezi ASP Sokoni, muswada Usalama Barabarani 'kuiva'

Na Margaret Malisa, Dodoma

**NI** muda mrefu wadau wa usafiri wamekuwa wakipigia kelele Sheria ya Usalama Barabarani ya Mwaka 1973, ifanyiwe marekebisho yanayoendana na wakati uliopo.

Hiyo inatokana na tathmini na tafiti za wadau wa usafiri, baada ya kubaini ajali barabarani zimeendelea kutawala. Ilibainika sheria ya mwaka 1973 haijakaa sawa.

Sheria ina mchango katika kukabili changamoto za usalama barabarani. Utafiti uliofanyika unaonyesha upungufu unaohitaji maboresho, ili yaendane na wakati na kukabili changamoto za ajali barabarani.

Katika sheria hiyo, imependekezwa kufanyiwe kazi suala la mwendokasi, matumizi ya mikanda, kofia ngumu, vilevi na vizuizi vya watoto.

Ndani ya mwendokasi, unaotajwa kuwa chanzo kikuu cha ajali na sasa inahitajika kuangaliwa kwa upana na si kama zamani, kuna mambo kadhaa yametambuliwa kwa mujibu wa Sheia ya Usalama Barabarani ya mwaka 1973, katika kudhibiti mwendokasi.

"Wadau wa usafiri walipendekeza sheria itamke maeneo yote na si yale ya mjini tu/makazi. Itamke wazi kuhusu maeneo ya shule, hospitali na maeneo yenye mikusanyiko mikubwa ya watu," ni sehemu ya mapendekezo hayo.

Pia kuna matumizi ya mikanda, inayotakiwa sasa katika mapendekezo, imembana dereva na abiria wake kufunga mikanda na kukiuka iwe kosa, tofauti na zamani haikusema kitu kwa abiria walioko viti vya nyuma.

Utafiti uliofanywa na Shirika la Afya Duniani (WHO), unaonyesha iwapo ajali zitatokea, matumizi ya mkanda kwa mtazamo huo mpya, unaweza kupunguza nusu ya ajali kwa abiria wa kiti cha mbele, pia asilimia 70 kwa walioko nyuma.

Katika hilo, Mamlaka ya Usafiri wa Barabarani na Majini (Sumatra), kupitia kanuni zake inahitaji abiria wote wafunge mkanda, huku sheria iliyopo ya Usalama Barabarani imekaa kimya, hali inayotoa wakati mgumu, utekelezaji wa kanuni husika.

Ni pendekezo la wadau wa sheria hiyo, ibadilishwe na kuwataka abiria wote, wanaokuwa katika chombo cha usafiri wa kibiashara au binafsi kufunga mikanda wakati wote wa safari na abiria ambaye hatafunga mkanda wa usalama, ataadhibiwa binafsi.

Pia kwa waendesha pikipiki, biashara iliyotawala kila mahali nchini, kuna suala la matumizi ya kofia ngumu. Sheria ya sasa ya Usalama Barabarani inatamka kosa kwa mwendesha pikipiki kutokuvaa kofia ngumu, wakati anaendesha chombo chake.

Hata hivyo, inafafanuliwa kuwa sheria hiyo haisemi chochote kwa abiria anayepanda chombo hicho, hali kadhalika sheria haielezi jinsi gani kofia inatakiwa kuvaliwa na aina maalum ya kofia inayopaswa kutumika.

Kwa mujibu wa WHO, iwapo ajali itatokea, madhara ya upungufu katika uvaaji kofia ni makubwa, ikinganishwa na kofia hiyo kama ingevaliwa kwa usahihi.

Hivyo, kwa kukizingatia kuwa sasa hivi usafiri wa pikipiki umekuwa unatumika kwa kiasi kikubwa, kuna majibu ya maboresho ya sheria kwa abiria wake.

Katika suala la vilevi, hadi sasa sheria inakataza uendeshaji chombo cha moto akiwa na kiwango cha kilevi katika damu yake kinachozidi miligramu 80 kwa mililita 100 katika mfumo wa mwili.

Kiwango hicho kinatajwa ni kikubwa sana, kikilinganishwa na utafiti wa WHO inayopendekeza kiwango cha miligramu 50 kwa mililita 100 kwa dereva aliyebobea na miligramu 20 kwa mililita 100 kwa dereva mchanga.

Msukumo wa wadau ni kutaka sheria ifanyiwe marekebisho, iendane na kiwango kilichopo cha kimataifa.

Hadi sasa Umoja wa Mataifa na shirika lake na WHO, wote wanakiri hitaji la mabadiliko ya haraka katika Sheria za Usalama Barabarani, ili ajali zipungue nchini.

Inaelezwa kwamba katika kipindi cha miaka mitano sasa, nchi 17 zenye jumla ya wakazi milioni 409 zimefanya maboresho ya sheria za barabarani.

Nchini Tanzania, baada ya jitihada za wadau wa usafiri kuipigia kelele maboresho ya kisheria, sasa tunafurahi nuru ya mabadiliko yanaonekana, dalili ya safari ya kupenya katika hatua kuelelea katika muswada kujadiliwa bungeni.

Mwenyekiti wa kamati ya Bloomberg Initiatives for Global Road Safety' ambayo inaratibiwa na WHO tawi la Tanzania, kwa kushirikiana na Wizara ya Afya, Mrakibu Msaidizi wa Polisi, Deus Sokon, ambaye pia ni Mwanasheria wa Kikosi cha Usalama Barabarani, anasema baada ya kupita hatua mbalimbali, kufikia hatua zake za mwisho kusogea bungeni. Kila la kheri sheria mpya, kwa niaba ya wadau, pongezi sana ASP Sokoni.

## HABARI KITAIFA

### *Tupambane kabisa na wenzetu wanaovuta sigara hadharani*

*Mhariri Pole na majukumu ya kila siku.*

*NAOMBA unipatie nafasi kwenye gazeti letu linalotupatia fursa sisi wasomaji wake ya kueleza dukuduku na kero mbalimbali zinazotukabili katika jitihada za kuhakikisha kuwa tunapiga hatua kubwa za kimaendeleo kama watu binafsi na taifa kwa ujumla.*

*Kero niliyonayo kwa leo ni ile ya watu wanaovuta sigara kila mahali hata kwenye sehemu za wazi au za umma ambazo kimsingi haziruhusiwi kwa wavutaji kufanya starehe yao hiyo.*

*Tabia hii inakera katika mazingira yoyote kwa sababu inasumbua wengine wasio wavutaji wa sigara, hali inayowasababishia adha isiyokuwa na sababu, eti tu kwa baadhi ya watu kuendeleza starehe zao.*

*Ikumbukwe kuwa kwa mujibu wa utafiti toka vyanzo mbalimbali vya kiafya, inabainishwa kwamba moshi wa sigara unapomfikia mtu asiyevuta, humwathiri zaidi kiafya kuliko hata huyo mtumiaji mwenyewe.*

*Bahati mbaya zaidi hata pale wananchi wenzetu hawa wavutaji wanapokanywa ama kunasibiwa waache kuwakera wenzao, baadhi yao huziba masikio na wengine hutoa majibu yasiyofaa.*

*Ninaomba mamlaka zinazohusika zisaidie kulimaliza tatizo hili sasa kwa kuchukua hatua za kuwakamata na kuwapeleka kwenye vyombo vya sheria wale wote wanaozidi kuvuta sigara sehemu za wazi ama za umma.*

***Jumanne Ayoub, DSM***

### *Tusilee binadamu wa aina hii*

***Mhariri,***

*UKISOMA vitabu vya dini na hata kusikiliza mahubiri na mawaidha ya viongozi wetu wa dini ni dhahiri utapata jinsi ambavyo misahafu na maelekezo ya viongozi hao inavyosisitiza juu ya umuhimu wa kulinda uhai wa binadamu.*

*Inafafanuliwa kwamba uhai wa binadamu ni lazima ulindwe kwa kuwa ndivyo yalivyo maagizo ya Muumba na kwamba hata sheria, kanuni na taratibu mbalimbali katika jamii na makabila zinasisitiza juu ya hilo.*


*Ninaandika katika ukurasa huu kuelezea namna ninavyochukizwa na watu ambao hutupa watoto ovyo jalalani ama kwenye vyoo wakati mwingine na hivyo kukatisha maisha ya watoto wasio na hatia.*

*Tatizo hili kimsingi liko sana kwa wasichana ambao matukio mengi yamekuwa yakiripotiwa mara kwa mara juu yao katika vyombo vya habari.*

*Ninawatahadharisha watu wanaofanya unyama huo wakumbuke kwamba Mwenyezi Mungu anawaona.*

*Ninaomba kwa serikali yetu tukufu iwachukulie hatua kali watu wa aina hii wasiothamini kabisa uhai wa binadamu.*

***Lufunga Jifenenge-Kahama***




# Tutafikia malengo ya mawasiliano kwa ushirikiano wa wadau wote

**Na Mwandishi Wetu**

WIKI iliyopita, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) ilikuwa mwenyeji wa mkutano wa nane wa kila mwaka wa Umoja wa Mamlaka za Mawasiliano katika nchi za Kusini mwa Afrika (CRASA).

Mkutano huo ulifanyika jijini Dar es Salaam kupitia kauli mbiu ya 'Making Smart Societies a Reality' na ulihudhuriwa na wadau mbalimbali wa tasnia ya teknolojia ya mawasiliano pamoja na wale wa masuala ya posta.

Lengo kuu la mikutano hii ni kutoa nafasi kwa wanachama wa CRASA kupata fursa ya kufanya mapitio na mijadala kuhusu sera na mambo mengine yanayohusu mawasiliano katika eneo hili la dunia.

Katika mkutano wa mwaka huu mambo mbalimbali yalijadiliwa ikiwamo jambo nyeti la kodi kubwa, gharama ya mawasiliano ya simu, namna ya kuboresha mawasiliano katika maeneo ya vijijini na uzuiaji wa uhalifu wa kimtandao.

Katika wakati huu ambapo TCRA inatafakari kuhusu maazimio yaliyofikiwa katika mkutano huo na kutazama sera na kanuni mwafaka kwa ajili ya kutimiza azima ya kuboresha sekta hii hapa nchini na katika ukanda wote huu wa Kusini mwa Afrika, nadhani huu pia ni wakati muhimu kufanya tathmini ya sekta hii kwa kiwango cha Tanzania.

Pasipo shaka yoyote ile sekta ya mawasiliano ni miongoni mwa zile zinazokua kwa kasi zaidi hapa nchini.

Kwa mujibu wa ripoti iliyo karibuni zaidi iliyochapishwa na taasisi ya kimataifa ya mawasiliano duniani ya GSMA, teknolojia ya mawasiliano kupitia simu za mkononi ndiyo kitovu cha mabadiliko ya kiteknolojia yanayoendelea Tanzania.

Ripoti hiyo inaeleza kuwa mapinduzi hayo ya kiteknolojia yamekuwa mojawapo ya chachu za ukuaji wa uchumi wa Tanzania.

Kwa mfano, ripoti hiyo ya utafiti imeonyesha kwamba mchango wa sekta ya mawasiliano ya simu katika uchumi wa Tanzania unabashiriwa kuongezeka kutoka dola bilioni 2.5 mwaka 2016 hadi dola bilioni nne mwaka 2020.

Kiwango cha dola bilioni nne (zaidi ya shilingi trilioni nane za Tanzania) ni sawa na asilimia sita ya Pato la Taifa (GDP).

Ripoti hiyo ya wataalamu hao wa GSMA imesema kwamba ili mchango huo wa sekta ya mawasiliano ufikiwe, ni lazima mambo kadhaa muhimu yafanyike.

Kwa mfano, mojawapo ya mapendekezo ni kuwekwa kwa mazingira wezeshi yatakayochochea kukua zaidi kwa sekta hiyo.

Kwa sababu ukuaji wa sekta yoyote ile hutegemea ukaribu wa pande tatu; serikali, wawekezaji na wadau (wateja na wahusika wengine katika sekta) ni muhimu sana kwa pande hizo kukaa chini na kubungua bongo kufahamu changamoto za kisheria na kiwekezaji ambazo endapo zitafanyiwa kazi ipasavyo, hakutakuwa na kikwazo kufikia ubashiri uliotabiriwa.

Kwa mtu ambaye ameisoma ripoti hiyo ya GSMA, atakuwa amebaini kwamba mojawapo ya masuala ya kisera yanayotakiwa kuangaliwa kwa undani katika mchakato huu ni suala la washindani wa sekta husika kufikiria kuungana ili kupunguza utitiri wa washindani uliopo katika sekta hiyo.

Utafiti huo wa GSMA umeonyesha kwamba kwa mujibu wa takwimu zilizopo, Tanzania ni miongoni mwa nchi zinazofahamika kwa kuwa na washindani wengi katika soko moja la biashara ya mawasiliano ya simu.

Hili ni tatizo kwa sababu mahali penye washindani wengi wa sekta hii humaanisha faida kidogo sana kwa wawekezaji.

Kwa vyovyote vile, hakuna tena mtu anayeweza kubisha kuhusu umuhimu wa sekta hii katika maendeleo ya uchumi wa taifa letu. Takwimu ziko wazi na kuna msemo maarufu kwamba namba huwa hazisemi uongo.

Ni jukumu la serikali, wadau na kampuni za simu kukaa chini, kututua changamoto hizo ndogondogo zilizopo ili kwamba lengo la kuwezesha mamilioni ya Watanzania kunufaika na mapinduzi haya ya kiteknolojia liweze kufikiwa.

**KABWELA** NA FADHILI MOHAMMED



## Mawaziri wahamia ofisi mpya

INATOKA UK 2

Kikuu cha Mbeya na wanashauriwa na TBA.

"Wizara hii ilipatiwa eneo lenye ukubwa wa ekari 11 na tuliamua kugawa maeneo mawili, ambapo eneo jingine tumewapatia Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (Tarura), ambao wamepanga kwenye jengo kule mjini wanalipa kodi ya pango la zaidi ya Sh. milioni 400 kwa mwaka,"alisema.

Jumamosi iliyopita Rais Magufuli alitoa agizo hilo baada ya Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, kusema kuna baadhi ya wizara ikiwamo Tamisemi ambazo majengo yao yamechelewa kukamilika kutokana na kuchelewa kupata fedha.

Hata hivyo, Rais Magufuli alisema hataki kusikia kunakuwa na kisingizio cha majengo mengine kuwa hayajakamilika na kama mtu ameshindwa akae hata chini ya mwembe ilmradi awe Mtumba ambako ndiko mji wa serikali ulipo.

"Nataka wote muwe hapa ili muda wote nitakapowahitaji mawaziri muwapo, hakuna sababu ya kuwaita bali nitawafuata kwenye majengo, nataka kila mmoja ahamie kwa vitendo siyo maneno," alisema.

## Idadi ya wategemezi Tanzania yaongezeka

INATOKA UK 4

watu.

Alisema wakati nchi hizo zikidhibiti ongezeko la watu, wenye uwezo wa kufanya kazi waliongezeka na walipata kazi, huku Tanzania watu wenye uwezo wa kufanyakazi walizidi kupungua.

"Idadi ya wategemezi Tanzania imeendelea kuongezeka ikilinganishwa na wenye uwezo wa kufanyakazi, kwenye nchi hizo wenye uwezo wa kufanya kazi waliongezeka ikilinganishwa na idadi ya watu," alisema.

Alisema nchi hizo zilifanya mabadiliko mbalimbali kwenye sekta zinazoajiri watu wengi, na kwamba kwa sasa sekta ya kilimo haifanyi vizuri, lakini sekta ya viwanda na huduma ndiyo inaajiri watu wengi.

Aidha, alisema sekta binafsi imeendelea kuwa katika mazingira magumu ya ukuaji ikilinganishwa na nchi sita, na kwamba sekta binafsi ndiyo injini ya uchumi wowote duniani.

Kuhusu mazingira ya ufanyaji biashara, alisema ripoti ya mwaka 2018 imeonyesha bado kuna vikwazo kwenye mipaka kwa kuwa wananchi hawawezi kuvusha mizigo kwa haraka huku Bandari ya Dar es Salaam ikitumika chini ya uwezo wake.



Mfanyakazi wa kampuni ya usafi akizoa mchanga kwenye barabara ya lami katika eneo la Kijitonyama, jijini Dar es Salaam. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Tarura yawezeshwa kwa bajeti zaidi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, amesema serikali imeongeza Sh. bilioni 33 kwenye bajeti ya Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (Tarura) kutokana na kilio cha wabunge wengi, wakitaka fedha ziongezwe kwa wakala huo ili kutimiza majukumu yake.

Akihitimisha hoja ya makadirio ya bajeti ya Wizara yake kwa mwaka ujao wa fedha, Jafo alisema fungu namba 59 la Ofisi hiyo zimeongezwa fedha hizo ambazo zitapelekwa Tarura kwa ajili ya ujenzi wa barabara.

"Baada ya kusikia kilio cha wabunge humu ndani serikali imeona iongeze Sh.Bilioni 33 ambazo zitakwenda Tarura kutatua matatizo ya wananchi wetu," alisema.

Alieleza kuwa bajeti ya maendeleo ya Ofisi hiyo itasomeka Sh. bilioni 496.5 badala ya Sh. bilioni 463.5 na hivyo katika miradi ya maendeleo na matumizi ya kawaida itakuwa Sh. bilioni 550.2.

"Bajeti nzima ya Tamisemi itakuwa na Sh. trilioni 6.24," alisema.

Jafo alisema kama kuna mambo hayajakaa sawa kwenye utoaji wa vitambulisho vya ujasiriamali watashughulikia kwa kuzingatia maoni ya wabunge.

"Wabunge walisema inaweza kuwa njema lakini utoaji haufuati taratibu, kazi yetu ni kuchukua maoni na kufanyia kazi, tutaenda kurekebisha,"alisema.

"Madiwani wanafanya kazi kubwa sana na wanasimamia kwa fedha zinazopelekwa kule, tumechukua suala hili tunaenda kutafakari ili tuweze kuhakikisha angalau kipato chao kiongezeke,"alisema.

Aidha, alisema wanaenda kupitia mwongozo wa utoaji wa posho haraka iwezekanavyo ili madiwani wasiwe na kinyongo kwenye utendaji kazi zao kwa kuzingatia wanapotoka na kazi wanayoifanya.

Kuhusu kamuni za uchaguzi wa Serikali za Mitaa, alisema wataalamu wameandaa kanuni za uchaguzi wa serikali za mitaa kwa umakini na umahiri wa hali ya juu kwa kushirikisha wadau mbalimbali ikiwemo vyama vya siasa.

"Tulifanya mkutano na vyama vya siasa wadau walishiriki vizuri na jambo hili lipo hatua za mwisho ili zikamilishwe na kutangazwa gazetini ili zifanye vizuri katika uchaguzi wetu mwezi Novemba mwaka huu," alisema.

Jafo alisema kanuni za utoaji mikopo ya wanawake, vijana, na watu wenye ulemavu zimeshatangazwa gazetini na zitawabana wakurugenzi kwenye hilo.

Kuhusu ajira, alisema walimu walioajiriwa ni 13,632 na wamesharipoti kwenye vituo na pia ajira nyingine zaidi ya 4,500 na kuahidi kuwa serikali itaendelea kuongeza idadi ya walimu kama mipango ya serikali inavyosema.

## Ushahidi kesi

INATOKA UK 3

ya kutokuhudhuria kesi hiyo jana kwa sababu amekwenda kwenye kesi ya jinai inayomkabili katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Songea kwa ajili ya utetezi Aprili 15 na 16, mwaka huu".

Aliendelea kunukuu:

"Kutokana na sababu hiyo mimi Dk. Vincent Mashinji, nimeridhia kesi inayonikabili katika Mahakama ya Kisutu kuendelea kusikilizwa bila uwepo wangu," Profesa Safari alinukuu barua ya mshtakiwa.

Hata hivyo, Nchimbi alidai kuwa sababu za mshtakiwa hazina mashiko kisheria kwamba kwa mujibu wa kifungu namba 197/cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai (CPA) kifungu (b), kinatoa mwanya kupokea ushahidi pale tu mshtakiwa/washtakiwa wanapokuwa na matatizo ya afya na wana wakili wa kumwakilisha kusikiliza kesi yake bila uwepo wake/wao.

Pia, sababu za kuhudhuria kesi hazina mashiko ya kisheria kwa sababu usikilizwaji wake ulipangwa wiki mbili zilizopita na mshtakiwa Mashinji alikuwapo.

"Tunaomba tarehe ijayo mshtakiwa aieleze mahakama kama siku ilipopangwa kesi hii alikuwa na taarifa ya kesi ya Songea na kama ndiyo kwa sababu gani ameamua kwenda huko na kuacha kusikiliza kesi hii, kwa sababu kesi ilipangwa kusikilizwa siku mbili leo (jana) na kesho (leo), tunaomba ipangwe kesho," alidai Nchimbi.

Prof. Safari alidai hawezi kuelezea kuhusu uamuzi wa mshtakiwa kwenda Songea badala ya kusikiliza kesi hiyo na kuhusu kesi kusikilizwa leo hana pingamizi.

Hakimu Simba alisema kesi hiyo itasikilizwa leo saa 4:00 asubuhi dhamana za washtakiwa zinaendelea.

Mbali ya Mbowe na Mashinji washtakiwa wengine ni Mbunge wa Bunda, Ester Bulaya, Mbunge wa Tarime Mjini Esther Matiko, Katibu Mkuu Taifa ,Vicent Mashinji, Mbunge wa Iringa mjini, Peter Msigwa, Naibu Katibu Mkuu Taifa, Zanzibar, Salum Mwalimu, Mbunge wa Kibamba, John Mnyika, Katibu Mkuu Taifa, Vicent Mashinji, Mbunge wa Kawe, Halima Mdee na John Heche.

Katika kesi ya msingi, washtakiwa hao wanadaiwa kuwa kati ya Februari Mosi na Februari 16, mwaka huu, Mbowe na wenzake wakiwa Kinondoni, Dar es Salaam kwa pamoja walikula njama na wengine ambao hawapo mahakamani ya kutenda kosa la jinai ikiwamo kuendelea na mkusanyiko isivyo halali na kusababisha chuki na uchochezi wa uasi.

# Walia kupigwa danadana fao

INATOKA UK 3

alimwandikia Mkurugenzi Mkuu wa NSSF kumtaka wafuatilie malalamiko hayo na kutekeleza kwa mujibu wa sheria.

"NSSF makao makuu walionigea na Meneja wa Ubungo, ambaye alimtaka aende ofisini kwake, wasaidizi wake waliniambia nirudi Aprili mosi, mwaka huu, baada ya muda akaniandikia Mei 22, mwaka huu, nikaenda kwa meneja ambaye alirekebisha akaandika Aprili 23, mwaka huu, wakaniambia niende Aprili 16 yaani jana, ambako pia nimepigwa kalenda hadi Mei 30, mwaka huu," alisema.

Mwanachama mwingine aliyefungua maombi Januari mwaka huu, aliambiwa arudi Februari 22, alipofika alipigwa tarehe hadi Machi na jana alisema ameambiwa hadi Mei, mwaka huu.

"Katika kuzungumza watu tuliokuwapo pale tulijiuliza kwanini wanatusumbua, wote tukajikuta tulijibiwa Januari mwaka huu kuwa tulikosea kuweka dole gumba, baadaye tuliambiwa mtandao unasumbua na baadaye wanasimika mfumo mpya," alisema na kuongeza:

"Kama hakuna fedha watuambie kuliko kutusumbua na majibu yanakuwa tarehe fulani nenda benki utakuta fedha zako."

Naye, mwanachama mwingine alisema kwa muda mrefu anafuatilia fao la upotevu wa ajira ya asilimia 33.3 ya mshahara wake ambalo lipo kwa mujibu wa sheria, lakini anasumbuliwa kiasi cha kukata tamaa.

"Rais alishatangaza tulipwe fedha zetu, lakini kila siku wanakupa sababu mpya ilimradi uondoke, wakati wanakuja kuomba michango yetu wanatuomba kwa upole na ushawishi, lakini tunapokuja kudai haki yetu tunasumbuliwa," alisema.

Nipashe ilimpotafuta Meneja Mahusiano wa NSSF, Lulu Mengele, kwa njia ya simu kutoa ufafanunuzi kuhusu madai hayo, alimjibu mwandishi kuwa yuko kwenye kikao, atafutwe baadaye.

## Waziri akiri udhaifu

INATOKA UK 3

kuleta marekebisho kabla ya Juni 30, mwaka huu.

Aidha, aliagiza WMA kufanya ukaguzi wa uzalishaji wa bidhaa hasa katika viwanda vya nondo, mabati, marumaru, misumari na mabomba ya chuma ili kuangalia uzingatiwaji wa vipimo na kuwapa elimu kuhusu vipimo sahihi wenye viwanda hivyo.

"Nimeagiza WMA wafanye ukaguzi wa uzalishaji wa bidhaa ili bidhaa zinazotoka Tanzania ziendelee kukubalika kuwa bora kwenye masoko ya nchi za Afrika Mashariki, SADC, Afrika na nje ya Bara la Afrika," Kakunda alisema.

HABARI KITAIFA

# Magufuli awakuna wadau wa SAGCOT

**Na Mwandishi Wetu, NJOMBE**

WADAU wa Kituo Cha Kuendeleza Kilimo Nyanda za Kusini mwa Tanzania (SAGCOT), wamepongeza hotuba ya kizalendo ya Rais John Magufuli kuhusu uwekezaji na kuelezea kuwa dhamira hiyo itachochea ukuaji wa sekta ya viwanda nchini.

Akizindua Kiwanda kipya cha Kuchakata chai cha Kabambe kinachomilikiwa na Kampuni ya Unilever Tanzania, wiki iliyopita, Rais Magufuli aliwaonya watendaji katika ngazi zote serikalini kuachana na urasimu usio wa msingi kwa kukwamisha uwekezaji.

Mwenyekiti wa Wood Foundation, Sir Ian Wood, alisema kauli ya Rais Magufuli imeonyesha dhamira ya wazi kuwa anakerwa na watendaji wachache wanaokwamisha ukuaji na maendeleo ya sekta za viwanda na uwekezaji.

Mbali ya kumpongeza Rais Magufuli, Sir Wood alisema taasisi yake itaendelea kufanya kazi kwa karibu na SAGCOT kwani kuwepo kwake kumechangia kuleta mageuzi mengi katika sekta ya kilimo katika ukanda huo.

"Maendeleo yanayopatikana hapa ni matokeo chanya kazi na uratibu mzuri wa SAGCOT kama kiunganishi sahihi kwa wadau wote. Taasisi yangu kama mdau tutaendelea kufanya kazi kwa karibu na SAGCOT," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa SAGCOT, Geoffrey Kirenga, alisema katika kipindi kisichozidi mwaka mmoja, Rais Magufuli amefungua viwanda viwili muhimu katika eneo la SAGCOT.

"Kabla ya uzinduzi wa Kiwanda cha Kabambe ambacho kitawanufaisha sana wakulima wadogo wa chai katika vijiji vyote vinavyozunguka kiwanda hicho, Rais pia alifungua kiwanda cha kuzalisha vifaranga vya kuku na chakula cha Silverlands kilichopo mkoani Iringa," alisema Kirenga.

"Ukitembelea eneo la SAGCOT utaona namna gani serikali na sekta binafsi zinavyofanya kazi kwa pamoja. Miaka michache ijayo utashuhudia mabilionea wakitoka katika sekta ya kilimo," alisema na kuongeza kuwa Unilever Tanzania na Silverlands Tanzania ni wadau wa SAGCOT.

Alisema kitendo cha Dkt. Magufuli kufungua viwanda hivyo kimechochea msukumo mkubwa wa wadau wa SAGCOT. Rais magufuli hufanya kazi kwa vitendo na mfuatiliaji mzuri wa maendeleo.

"Ni faraja kubwa sana wadau wetu wanapomwona mheshimiwa Rais akifanya ziara katika maeneo yao. SAGCOT itaendelea kuwa nguzo kwa ubia kati ya sekta za umma na binafsi," alisisitiza.

Naye Mkulima wa chai na parachichi wilayani NJombe, Christom Mkole, aliishukuru SAGCOT kwa kuwa mstari wa mbele kuwajengea uwezo wakulima wadogo na kufanya kilimo biashara.



Wafanyakazi na wadau wa kampuni ya kukopesha ya Kopafasta wakisherehekea uzinduzi wake jijini Dar es Salaam Jumatatu.
**PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Fursa kukopesha sekta binafsi yaanza

**Na Mwandishi Wetu**

MAKUNDI yaliyopo katika sekta isiyo rasmi yamepanuliwa wigo wa kukopa baada ya kuanzishwa na kuzinduliwa kwa Kampuni inayotoa mikopo ijulikanayo kama kopafasta.

Kampuni hiyo inayotoa mikopo kwa wanachama waliosajiliwa kupitia miradi mbalimbali kama TACIP na PSG-P inayotekelezwa na kampuni ya DataVision International kwa kushirikiana na Taasisi na Wizara za Serikali, ilizinduliwa Jumatatu jijini Dar es Salaam.

Inaelezwa kuwa lengo kuu la kopafasta ni kusaidia kurasimisha na kuboresha sekta zisizo rasmi kama sanaa za ufundi na ulinzi binafsi kwa kuanzia, ili kuwasaidia kuwapa mikopo ya fedha, vifaa na vitendea kazi, na kujenga uwezo kupitia mafunzo ya usimamizi wa fedha, biashara na uwekezaji.

Akitoa ufafanuzi wa huduma hiyo wakati wa hafla ya uzinduzi, Meneja wa kopafasta, Patrick Kang'ombe alieleza sababu ya kutoa huduma ya mikopo kwa makundi hayo na kusema:

"Huduma yetu ni tofauti na ya kipekee, kwani tumechagua sekta ambazo zimesahaulika na zimekuwa zikichukuliwa kuwa hazikopesheki, kwa maana ya kutokuwa na uwezo wa kuweka dhamana na kutoaminika kupewa mikopo.

Hizo zimekuwa changamoto kubwa kwa sekta zisizo rasmi, na kuzifanya kubaki nje ya mfumo rasmi, pamoja na kwamba zimekuwa na mchango mkubwa katika pato la Taifa."

"Hivyo kopafasta tunaamini kuwa, tukiwezesha makundi haya na kuyaingiza katika sekta rasmi, tutakua tunaunga mkono na kutekeleza sera na jitihada za Serikali ya awamu ya tano ya Dk. John Magufuli kama vile kupanua wigo wa walipakodi na kuongeza pato la Taifa, kukuza ajira, uanzishwaji wa viwanda vidogo vidogo na kuvutia wawekezaji katika Taifa letu," alisema Kang'ombe na kuendelea:

"Tungependa pia kutoa wito kwa Serikali kuendelea kusaidia na kuwezesha miradi inayolenga kutambua na kuratibu wa sekta zisizo rasmi kama TACIP na PSG-P kwa nia ya kurasimisha sekta hizo ili kufanya makundi haya kujitambua, kutambulika na kujidhamini ili kopafasta iendelee kuyakopesha."

Alieleza kuwa kopafasta pia imeshirikiana na wadau mbalimbali katika kutoa huduma hii, ikiwamo huduma ya utumaji na upokeaji wa pesa kwa njia ya simu ya mkononi kupitia MLIPA. HI inasaidia kuhakikisha walengwa wa wanapata huduma ya mikopo kwa urahisi na kwa wakati.

Meneja wa MLIPA, Maclean Geofray Mwaijonga, alisema mikopo hii hutolewa kwa njia ya kielektroniki kupitia mfumo wa MLIPA na kumfikia mlengwa kupitia akaunti yake ya pesa ya mtandao wowote wa simu yake ya mkononi kama vile Tigo pesa, M pesa, au Halopesa popote alipo nchini."

# Miaka 29 ya kijiji bila maji

**Na Yasmine Protace,**

**MKURANGA**

KIJIJI cha Sangatini wilaya ya Mkuranga mkoani Pwani, kina miaka 29 bila ya shule ya msingi, hali inayosababisha wanafunzi kutembea kutoka kijiji hicho kilomita 10 kwenda kusoma shule za msingi Kigamboni jijini Dar es Salaam..

Pia kijiji hicho hakina sekondari na kusababisha wanafunzi kutembea kilomita 14 kwenda kusoma katika sekondari ya kijiji cha Vianzi Mkuranga.

Hayo yalisemwa na baadhi ya wakazi wa kijiji hicho walipokuwa wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti.

Hakijiki Rashid, alisema kutokuwapo kwa shule ya msingi na sekondari kunawafanya watoto wao kutembea umbali mrefu kwenda maeneo mengine.

"Kijiji hakina shule ya msingi na sekondari, kwa sasa watoto wanaosoma shule ya msingi hulazimika kwenda Kigamboni kusoma na wanatembea kilomita 10," alisema.

Aliongeza kuwa wanaosoma sekondari nao hutembea kilomita 14 kwenda kijiji cha Marogoro kusoma.

Alisema wanamuomba diwani wao na mbunge wawasaidie ili kijiji kipate shule na kuwapunguzia umbali mrefu watoto kutembea.

Aliongeza kuwa maeneo yote ambayo watoto wanasoma inatakiwa kulipa nauli ya Sh. 1,500, lakini wazazi hawana uwezo wa gharama hizo.

Mwenyekiti wa kijiji hicho, Abdallah Ramadhani Mhando, alisema kuwa kijiji kilianzishwa mwaka 1970 na kina wakazi 2000, lakini kinakabiliwa na changamoto ya umeme, shule na barabara.

Diwani wa Vianzi, Nassoro Chuma, alikiri kijiji hicho kuwa na changamoto ya umeme, maji na barabara.

Hata hivyo, alisema wameshapata Sh. milioni 37 kwa ajili ya ujenzi wa shule ya sekondari Marogoro ambapo wanafunzi watasoma kutoka vitongoji vya kijiji hicho.

**"Kijiji hakina shule ya msingi na sekondari, kwa sasa watoto wanaosoma shule ya msingi hulazimika kwenda Kigamboni kusoma na wanatembea kilomita 10," alisema.**

# PSSSF yalipa bil. 890/- wastaafu 10,000

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

SERIKALI imesema hadi kufikia Februari 28, mwaka huu jumla ya wastaafu 9,971 walikuwa wameshalipwa stahiki zao takribani Sh. bilioni 888.39 na Mfuko wa Pensheni wa Watumishi wa Umma(PSSSF).

Hayo yalielezwa jana bungeni na Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu (Vijana, Kazi na Ajira), Anthony Mavunde, alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Mbozi (Chadema), Paschal Haonga, aliyetaka kujua ni lini serikali itawalipa wastaafu ambao walikuwa wanachama wa Mfuko wa Pensheni wa PSPF viinua mgongo vyao.

Akijibu swali hilo, Mavunde alisema hadi kipindi hicho kimelipwa kiasi cha fedha hizo na kwamba mfuko huo wa PSSSF umekamilisha kulipa malimbikizo ya deni la wastaafu lililorithiwa kutoka mfuko wa PSPF.

Aidha, alisema mfuko huo umekamilisha mfumo wa ulipaji mafao utakaowezesha kufanya malipo katika ngazi ya Mkoa, hivyo kuwezesha mfuko kulipa mafao ndani ya muda uliowekwa kisheria wa siku 60 tangu mwanachama anapowasilisha madai.

"Mifuko ya Hifadhi ya Jamii inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Bunge iliyoanzisha mfuko husika na pamoja na mambo mengine inasimamia muundo wa utawala na mfumo wa maamuzi na usimamizi wa uwekezaji wa fedha za mfuko," alisema.

Naibu Waziri huyo sheria inaipa Bodi ya Wadhamini ya mfuko jukumu la kusimamia uwekezaji wa fedha za mfuko kwa uhuru na kwamba si kweli serikali inaweza kuingilia uendeshaji wa mifuko, au kufanya maamuzi ya uwekezaji ikiwamo kukopesha taasisi au watu binafsi.

Hata hivyo, alisema mifuko ya Hifadhi ya Jamii imekuwa ikitoa mikopo yenye masharti nafuu kwa wanachama wake kupitia vikundi vya kuweka na kukopa (SACCOS) katika maeneo ya kazi.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akizungumza na Mbunge wa Mikumi, Joseph Haule (Chadema), wakati wa kikao cha Bunge jijini Dodoma, jana. **PICHA: OWM**

# Sababu shilingi kuendelea kuwa tulivu zabainishwa

BUNGE limeelezwa kuwa katika kipindi cha miaka miwili iliyopita thamani ya Shilingi ya Tanzania imekuwa tulivu dhidi ya Dola ya Marekani ikilinganishwa na sarafu zingine.

Kauli hiyo ilitolewa jana bungeni na Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Ashatu Kijaji, alipokuwa akijibu swali la Mbunge Tumbatu (CCM), Juma Othman Hija.

Katika swali lake, Mbunge huyo alihoji serikali ina mkakati gani wa kudhibiti mporomoko wa shilingi ya Tanzania dhidi ya sarafu zingine ikiwemo Dola la Marekani.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri huyo alisema hali hiyo inatokana na utekelezaji thabiti wa sera ya fedha na bajeti pamoja na kudhibiti mfumuko wa bei.

"Thamani ya shilingi ilipungua kwa wastani wa asilimia 2 mwaka 2017/18 na 2016/17 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 22 mwaka 2015/16, kiujumla, shilingi ilikuwa imara ikilinganishwa na sarafu nyingine kama vile Franc ya Rwanda iliyopungua kwa wastani wa asilimia 5 na shilingi ya Uganda iliyoshuka kwa asilimia 3.8 katika kipindi kama hicho," alisema .

Dk. Kijaji alisema ili kuimarisha utulivu wa thamani ya shilingi dhidi ya fedha za kigeni serikali inatekeleza mambo mbalimbali, ikiwamo kuhakikisha kuwa ongezeko la ujazi wa fedha linaendana na ukuaji wa shughuli za uzalishaji.

"Kadhalika, kuongezeka kwa uzalishaji wa bidhaa na huduma ndani ya nchi, kuongeza mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi na kudhibiti hali ya wasiwasi katika soko la fedha za kigeni inayosababishwa na hisia pamoja na biashara ya kuotea ambapo Benki Kuu hununua na kuuza fedha za kigeni katika soko la jumla," alisema.

Pamoja na hayo, alisema serikali katika kuimarisha thamani ya shilingi ina majukumu mawili ambayo ni serikali kupitia Benki Kuu ina jukumu la kutekeleza na kusimamia sera ya fedha ili kudhibiti mfumuko wa bei, viwango vya kubadilisha fedha na ujazi wa fedha katika soko.

## Uteuzi wa wahasibu AMCOS wahojiwa

MBUNGE wa Mtwara Mjini (CUF), Maftaha Nachuma, amehoji mkakati wa serikali wa kuteua wahasibu wenye vigezo kwenye vyama vya msingi vya ushirika (AMCOS) ili kuepuka wakulima kuibiwa.

Akiuliza swali jana bungeni, Mbunge huyo alisema kwenye vyama vya msingi vya ushirika kumekuwa na changamoto mbalimbali kwa wahasibu kuibia wakulima.

"Je, serikali ina makakati gani kuhakikisha kuwa wahasibu wanateuliwa kwa vigezo vya elimu ili kuepuka wakulima kuibiwa pindi wanapoenda kuuza mazao yao?"alihoji.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri wa Kilimo, Omary Mgumba, alisema wizara hiyo itafanya mchakato wa kupata wahasibu wenye weledi ili kuwahudumia wakulima nchini.

Mgumba alisema kuwa wameshaanza mchakato wa kuwatambua wahasibu wenye sifa ikiwamo wilaya ya Tunduru mkoani Ruvuma.

Alieleza kuwa walianza mpango huo katika mkoa, tajwa waliajiriwa kwa vigezo vya elimu, hivyo awamu ijayo watafanya nchi nzima ili kupata wahasibu wenye weledi wa kuwahudumia wananchi na kuondokana na changamoto za kuibiwa.

Katika swali lake la nyongeza, Mbunge wa Rombo (Chadema), Joseph Selasini, alisema zao la kahawa lina tatizo nchi nzima kutokana na uhaba wa pembejeo na bei yake kuwa juu, hivyo kupunguza uzalishaji.

"Je, Serikali ina mkakati gani kunyayua soko hilo kutokana na kuwa kahawa inayozalishwa mkoani Kilimanjaro ni tamu kuliko mikoa mingine,"alihoji.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Mgumba alisema kuwa wapo kwenye mazungumzo na kampuni ya nje inayozalisha mbolea ili kufungua kiwanda hapa nje hali itakayowezesha upatikanaji wake kwa urahisi na kwa wakati.

Awali, katika swali la msingi Mbunge wa Mbinga Vijijini (CCM), Martin Msuha, alihoji ni vyama vingapi vya msingi vya ushirika vimeundwa Wilaya ya Mbinga.

Akijibu swali hilo, Mgumba alisema hadi sasa mkoa wa Ruvuma una jumla ya vyama vya ushirika vya kahawa 67 na chama kikuu cha ushirika kimoja (Mbifacu) ambavyo vimeanzishwa na wakulima wa kahawa katika mkoa huo.

Alibainisha Wilaya ya Mbinga ina jumla ya vyama vya msingi vya kahawa 58 ambavyo ndio vitasimamia na kuendesha biashara ya kahawa katika wilaya hiyo.



# Watumishi 9 wa serikali mbaroni kwa utapeli viwanja

**Na Mwandishi Wetu, ARUSHA**

WATU tisa wakiwamo wanne kutoka Halmashauri ya Jiji la Arusha na Ofisi ya Ardhi Kanda ya Kaskazini, wametiwa mbaroni na polisi kwa tuhuma za utapeli wa viwanja na mashamba.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Arusha, Jonathan Shana, alisema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake.

Alisema watu hao wanatarajiwa kufikishwa mahakamani pindi tu upelelezi utakapo kamilika.

Kamanda Shana (pichani) alisema kukamatwa kwa watu hao kunafuatia operesheni iliyofanywa na polisi baada ya kuwapo kwa wimbi kubwa la watu wanaojihusisha na utapeli wa aina mbalimbali.

Alisema wapo baadhi ya watu wanaojidai kukwa ni maafisa ardhi, wamiliki wa mashamba na wengine wakijifanya matajiri wanaohitaji kununua ardhi.

Kamanda Shana alitoa wito kwa wananchi kufuata sheria na kufanya uchunguzi kabla ya kununua au kuuza nyumba au kiwanja.




# Soko la mifugo kudhibiti njia panya mipakani kufunguliwa

**Na Novatus Makunga, NAMANGA**

SERIKALI inatarajia kufungua soko la kimataifa la mifugo mpakani mwa Tanzania na Kenya eneo la Namanga katika wilaya ya Longido mwishoni mwa mwezi ujao kwa lengo la kudhibiti utoroshaji wa mifugo nje ya nchi kupitia njia za panya.

Mkuu wa Wilaya ya Longido, Frank Mwaisumbe, alisema taratibu zote za kuanza kwa soko hilo ifikapo Mei 29 mwaka huu zimekamilika.

Mwaisembe alisema hatua hiyo itafuatiwa na kufunguliwa kwa kiwanda kikubwa cha nyama mwezi Oktoba, mwaka huu, katika mji wa Longido.

Alisema kiwanda hicho kitakuwa na uwezo wa kuchinja ng'ombe kati ya 200 hadi 500 kwa siku na nyama kusindikwa kwa ajili ya kuuzwa ndani na nje ya nchi

"Hatua zote mbili hizo zitafanya biashara ya mifugo kuwa rahisi ambapo wafugaji watanufaika kwani tozo mbalimbali zitalipwa na mnunuzi wa mifugo au nyama iliyozindikwa kiwandani," alisema.

Alisema kwa kuanzishwa Kituo cha Forodha cha Pamoja cha Namanga, (OSBP) kumeondoa urasimu uliokuwa unawakwamisha wafugaji ukiwemo wa kutafuta vibali Dodoma au Dar es Salaam.

"Kituo hiki ni muhimu katika kuhudumia watu na kurahisisha ufanyikaji wa biashara mpakani," alifafanua Mwaisumbe.

Alisema kituo hicho kimeweza kupunguza magendo na kuongeza makusanyo ya mapato ambapo kwa sasa zinakusanywa kati ya Sh. milioni 300 hadi ya Sh. milioni 500 kwa mwezi katika kituo hicho cha Namanga

Akizungumzia mchakato wa uanzishwaji wa mnada wa kimataifa mpakani hapo, Meneja Msaidizi wa Mamlaka ya Mapato Nchini, (TRA), mkoani Arusha anayeshughulikia forodha, Godfrey Kitundu, alisema tayari wameweka mkakati wa kuhakikisha unafanyika kwa ufanisi mkubwa.

"Malengo ya kuwa na kituo hicho ni pamoja na kurahisisha na kuharakisha upitishaji wa mizigo mpakani na wasafiri pamoja na kuratibu usimamizi wa pande mbili za nchi yaani Kenya na Tanzania kwa maana hiyo hakutakuwa tena na changamoto zitakazokwamisha biashara ya mifugo," alisema.

Kwa mujibu wa mkuu wa kituo cha mifugo mkoani Arusha, Obed Nyasabwa, Wilaya ya Longido inashika nafasi ya pili mkoani Arusha kwa kuwa na wingi wa mifugo ikiwa nyuma ya Ngorongoro ambapo wilaya hiyo ina jumla ya ng'ombe 222,909, mbuzi 423,813 na kondoo 322,295.



Mkuu wa Wilaya ya Arumeru, Jerry Muro, akishirikiana na Mchungaji wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dayosisi ya Meru, Elias Katoi, wakitoa ng'ombe 20 kwa familia zisizojiweza. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# Ajiaua kwa kujichinja kwa kisu

**Na Woinde Shizza, ARUSHA**

MKAZI wa Mtaa wa Simanjiro, Kata ya Sombetini jijini Arusha, Lazaro Keorori, (53), anadaiwa kujiua kwa kujichinja kwa kisu kutokana na msongo wa mawazo uliosababishwa na mgogoro wa kifamilia.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Arusha, Jonathan Shana, alithibitisha hayo wakati akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake jana.

Alisema tukio hilo lilitokea majira ya usiku wa Jumatatu iliyopita huko nyumbani kwake.

"Uchunguzi tulioufanya tumebaini marehemu alichukuwa uamuzi huo kutokana na mgogoro wa kifamilia uliokuwepo kati yake na wake zake wawili.

"Marehemu alikuwa na msongo wa mawazo uliomsababishia kuamua kuchukuwa uamuzi wa kujiua na kwa maelezo ya watu waliohojiwa walisema, aliingia ndani usiku akachukua kisu kidogo chenye makali akaanza kujichinja na alipokaribia kufa alipiga kelele na hapo ndipo watu waliingia chumbani kwake kwa lengo la kumuokoa, lakini hawakufanikiwa," alisema.

Kamanda Shana aliwataka wananchi wakiwemo wanaume kutochukua maamuzi ya haraka haraka na kuwasihi iwapo wakipata msongo wa mawazo ni vizuri wakaenda kupewa ushauri katika nyumba za ibada au katika familia na siyo kujichukulia sheria mkononi.

# Baraza la madiwani Hai latangaza kutwaa ardhi

**Na Godfrey Mushi, HAI**

AZIMIO la Baraza la Madiwani wa Wilaya ya Hai, kutaka kutwaa eneo la ardhi inayodaiwa kushikiliwa na Manispaa ya Moshi ndani ya siku 21 kuanzia sasa, limepitishwa huku wawakilishi hao wa wananchi wakitaka kuwapo kwa maridhiano.Mwenyekiti wa baraza hilo, Helga Mchomvu alitangaza azimio hilo la kutaka kurejeshwa kwa sehemu ya ardhi ambayo Manispaa ya Moshi ilichukua na kuifanya kama dampo.

"Ardhi hiyo ambayo Manispaa ya Moshi walipewa na kuifanya dampo, tunataka tujadiliane nao katika muda usiozidi siku 21 kuanzia sasa ili tupate viwanja ambavyo tutatekeleza miradi ya kimkakati ya kuongeza mapato ya ndani.

"Ardhi ile kwa siku zinavyokwenda inaendelea kuvamiwa na watu na kuna maeneo tulivyoenda kule tulikuta tayari yameshavamiwa na watu.Kwa hiyo tutamshikirikisha hili jambo DC wetu (Mkuu wa Wilaya) aone namna ya kulishughulikia."

Eneo hilo la dampo wanalotaka kugawana Halmashauri ya Wilaya ya Hai na Manispaa ya Moshi lina ukubwa wa zaidi ya ekari 60.

Ofisa Ardhi Mteule wa Wilaya ya Hai, Jackob Mhumba aliwaeleza madiwani wa halmashauri hiyo kuwa wataomba kukutana na Manispaa ya Moshi kabla ya Mei 2, mwaka huu.

Alipotafutwa Meya wa Manispaa ya Moshi, Raymond Mboya, kuzungumzia madai hayo hakupatikana katika simu yake hata alipotafutwa mara kadhaa.

Pia wiki iliyopita, Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya aliagiza wananchi zaidi ya 200 kutoka Kijiji cha Foo, wilayani humo kumegewa ardhi kiasi cha ekari 100 katika eneo ambalo wawekezaji wameshindwa kuliendeleza kwa miaka mitatu sasa.

Ole Sabaya aliagiza: "Mkurugenzi Mtendaji, Katibu Tawala wa Wilaya na Afisa Ushirika na Mwenyekiti wa wakulima, naomba mkae mjadiliane kesho (leo) muone mnawagawiaje ekari 100 katika eneo walilopewa watu wa EPK (wawekezaji waliopo katika Shamba la Lambo Estates)."



Mwenyekiti wa Chama cha Wafanyakazi wa Malori Tanzania (Chawamata), Michael Wimile, akizungumza kwenye mkutano wa chama hicho, uliofanyika jijini Dar es Salaam juzi. Mkutano huo ulizungumzia changamoto mbalimbali zinazowakabili wanaposafirisha mafuta nje ya nchi. **PICHA: SABATO KASIKA**

## Waweka mikakati kupanda miti kukabiliana na ukame

**Na Godfrey Mushi, SAME**

MPANGO wa serikali wa kuifanya Wilaya ya Same, mkoani Kilimanjaro inayokabiliwa na ukame kuwa ya kijani, umeanza kutekelezwa kwa mafanikio, baada ya kupanda miti umbali wa kilomita 90 kando kando ya barabara kuu ya Arusha, Tanga.

Mkuu wa Wilaya ya Same, Rosemary Senyamule alisema nia ya serikali ni kubadili fikra za wananchi kuhusu mazingira hasa wanaopita katika barabara hiyo kudhani mji huo hauwezi kubadili taswira yake kutokana na ukame.

"Ni kwa lengo la kuhakikisha Inabadilisha mtazamo wao na wapitaji wa njia hiyo kuwa Wilaya ya Same ni kame,"alisema Senyamule. Zaidi ya watu 11,000 wanapita njia hiyo kwa siku.

Upandaji miti huo unaunganishwa na mpango mkakati wa mazingira wa Wilaya na maagizo ya Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan aliyotoa Oktoba, 2018 alipofanya ziara Wilayani humo.

Kwa mujibu wa Mkuu huyo wa Wilaya, wananchi wafurahia mpango huo na kutoa ushirikiano mkubwa wa kuchimba mashimo 32000 kwa kujitolea na sasa wanapanda miti hiyo iliyotolewa na Wakala wa Misitu Tanzania (TFS).

Senyamule ameeleza zaidi kuwa: "kazi kubwa iliyopo mbele yetu ni kuhakikisha miti hiyo inakuwa haijalishi ukame, mchwa wala mifugo. Tunataka kuondoa fikra kuwa Wilaya ya Same ni kame, tuanze kuona Same ya kijani."

Tayari, serikali wilayani humo imewaalika wadau mbalimbali kushiriki na kuchangia utunzaji wa miti hiyo.

Mkuu wa mkoa wa Kilimanjaro, Dk. Anna Mghwira aliagiza Wilaya zote kupanda miti kwenye barabara zao ili Kilimanjaro ing'ae.

# Taasisi ya Mwalimu Nyerere yatoa neno kwa viongozi, wananchi

**Na Mary Mosha, MOSHI**

TAASISI ya Mwalimu Nyerere Foundation, imewataka viongozi na wananchi wa Mkoa wa Kilimanjaro kuacha tabia ya kupenda rushwa, vitendo vya unyang'aji, dhuluma na kujilimbikizia mali kupindukia.

Mkurugenzi wa Taasisi hiyo, Joseph Butiku amesema kukithiri kwa matendo hayo kunasababisha kukwama kwa maendeleo ya mkoa huo.

Butiku alionya kuhusu matendo hayo jana, wakati akichangia mjadala katika mdahalo uliofanyika mjini hapa.

Mjadala huo uliwakutanisha viongozi wa kidini, wa kisiasa watendaji mbali mbali ambao kwa umoja wao wanajadili amani, umoja, haki na maendeleo ya mkoa huo.

"Taasisi hii tunasema mkoa wa Kilimanjaro, viongozi waache kufanya siasa za chuki, kunyoosheana vidole, kuhubiri uchumi wa viwanda kwa maneno na kuacha itikadi za vyama na badala yake kuhubiri, Amani,

Haki, Umoja pamoja na Maendeleo ili kuongeza ajira miongoni mwa wanajamii wakiwemo vijana,"alisema Mkurugenzi Butiku.

Alisema kuwa mkoa wa Kilimanjaro ni miongoni mwa mikoa iliyokuwa iking'ara kwa maendeleo yakichangiwa na uwepo wa viwanda, uwajibikaji wa vijana pamoja na ushirikiano uliokuwepo miongoni mwa wananchi na viongozi wao jambo ambalo kwa sasa halionekani kwa vitendo.

Wakichangia mdahalo huo baadhi ya viongozi wa dini, Padri, Dk. Idan Msafiri alikiri kuwepo kwa changamoto nyingi katika viongozi jambo linalopelekea kukwamisha maendeleo ya mkoa na taifa kwa ujumla

"Tafiti zinaonyesha kuwa viongozi wamegawanyika katika makundi ya matatu.. kundi na kwanza ni 5% ambao unauwezo wa kuwapa takataka wakazifanya dhahabu, kundi la pili ni 20% ni viongozi waliozoea kupewa miongozo na kuifuata bila kupambanua kwa kutumia busara ndani yake, na kundi la tatu ni 75% ya viongozi ambao ukiwapa dhahabu wanaifanya takataka, hii ni tahari na nilazima tujitadhimini hasa wanatuongoza,"alisema Padri Dk. Msafiri.

Alisema ni ngumu kuhubiri Amani na umoja itakayopelekea maendeleo bila kumtaka kila mmoja kutimaza haki yake katika eneo alilopo. Naye mwenyekiti wa halmashauri ya wilaya ya Rombo,

Evarist Silayo, alisema Amani sio kitu kinachoshuka kutoka mbinguni na kupewa watu, ni kitu kinachotengenezwa kwa kuzingania haki mifumo ya kisera na kila mtu kutekeleza wajibu wake katika nafasi aliyopo.

"Tupo baadhi ya viongozi badala ya kuonyesha njia ya wapi tunaelekea badala yake wamekuwa wakihubiri siasa za chuki, ubinafsi itikadi za kisiasa badala ya kuangalia masilai mapana ya taifa kwa kuhakikisha kunakuwepo na maendeleo,"alisema mwenyekiti wa halmashauri ya Moshi Michael Kilawila.

Baadhi ya wananchi, Faustina Msaki, waliziomba baadhi ya taasisi kuhakikisaha wanawakumbusha viongozi kwani wengi wao wa mkoa wa Kilimanjaro hawana maadili ya uongozi, wanaongoza kwa mihemko ya kisiasa na kuwapendeza waliowateuwa bila kuyatizama masilahi mapana na taifa pamoja na wananchi.

"Ipo haja ya taasasi za dini kuwa na semina mbali mbali za kiroho kwa viongozi wa mkoa wa Kilimanjaro hasa wakuu wa wilaya na wakurugenzi ili wawe na hofu ya mungu na waongoze kwa hekima huku wakisimamia haki na upatanishi,"alisema Elias Kimario Mkazi wa kiusa Moshi.

Ukurasa 18



MAFUNZO YA UONGOZI, MAISHA KUTOKA KWA NJELU KASAKA- 2

## MAKALA:

Jeshi Sudan lakwama kuteka mapinduzi ya kung'oa utawala wa Rais Al Bashir



Ukurasa 14

## KIMATAIFA:



Ulaya waipa Uingereza miezi sita, May atafuta msaada wa Corbyn

Ukurasa 20

siasa

JUMATANO APRILI 17, 2019

Nipashe

HABARI BORA NA KAMILIFU



Ruto ajimaliza; Akwama akitetea wala rushwa, ajilipua kudai hakuna njaa

Ukurasa 15

# ACT-WAZALENDO:

## Tuna plan B, iwapo Msajili...

- Kuzuia mikutano ni uonevu, uminywaji wa demokrasia na uvunjwaji wa sheria
- Kwetu ni heshima kumpata Maalim Seif ambaye ameamini katika katiba ya ACT-Wazalendo

**Na Enock Charles**

MOJA ya vyama vya upinzani ambavyo jina lake katika siasa za Tanzania kwa hivi sasa linachukua nafasi za juu, ni chama cha ACT- Wazalendo kilichopata usajili wa kudumu Mei, 2014.

Moja ya sababu ya chama hicho kuvuta macho na masikio ya wadau wa siasa nchini, ikiwa ni pamoja na vyombo vya habari ni hatua yake ya kupata wanachama wapya waliohama kutoka Chama cha Wananchi (CUF).

Mnamo Machi mwaka huu, aliyekuwa Katibu Mkuu wa CUF, Maalim Seif Sharif Hamad, alikihama chama chake akiwa na wafuasi wake na kujiunga na ACT Wazalendo, chama kinachoongozwa na mwanasiasa machachari na Mbunge wa Kigoma Mjini, Zitto Kabwe.

ENDELEA UK 16



Kiongozi Mkuu wa ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe. **PICHA: MTANDAO**

UCHAMBUZI

# Jeshi Sudan lakwama kuteka mapinduzi ya kung'oa utawala wa Rais Al Bashir

**Na Michael Eneza**

Ni matukio yanayoendana kabisa na dhana ya mapinduzi halisi yasiyo na umwagaji damu (au tuseme kwa wazi, kwani kuna wakati Rais Omar al-Bashir alitoa amri ya kutumia nguvu kuwaondoa waandamanaji, na baadhi wakapigwa risasi au kuumia kwa mabomu ya machozi, risasi za mpira, n.k.)

Ilikuwa ni kipindi kifupi cha takriban siku moja tangu mfululizo wa maandamano uanze kuelekea mwisho wa mwaka jana, na miezi minne baadaye utawala wa miaka 30 madarakani, wa Jenerali al-Bashir, ukafikia tamati yake.

Jitihada hiyo ya mfamaji ya kutaka kugeuzia silaha waandamanaji haikuungwa mkono na jeshi lote au polisi, hivyo ikatulizwa.

Baada ya hapo, maofisa wa ngazi za juu wa jeshi na serikali wakaamua kuwa waachane na Rais al-Bashir na kuchukua hali hiyo mikononi mwao, jeshi lisimamie kipindi cha mpito cha miaka miwili halafu ufanyike uchaguzi mkuu, wakidhani hayo ni mabadiliko makubwa.

Kumbe wanajaribu kurudia kilichojitokeza Algeria ambako rais Abdulaziz Bouteflika, ambaye uhalali wake wa utawala umevurugwa zaidi na hali ya kuwa mgonjwa na kutembea kwa kiti cha kusukuma na bado anataka muhula mwingine.

Jeshi pia lilimwondoa rais madarakani na kutaka kuchukua madaraka hayo kwa kipindi cha mpito, lakini wananchi wakagoma kuondoka barabarani.

Ina maana kuwa hii sasa imekuwa Arab Spring kamili kwani wakati ule machafuko yalipotokea Misri na utawala wa Rais Hosni Mubarak kuanguka, yalitekwa nyara na maswahiba wa kina al-Bashir wa makundi ya siasa kali na uzalendo wa kibaguzi ambayo yametawala Sudan kwa miaka mingi.

Ndiyo wamesheheni jeshini na katika vikosi maalum vya usalama wa taifa, ambao ndio hasa walitaka kuchukua madaraka kwa miaka miwili kuzuia mabadiliko halisi dhidi ya maslahi ya washika dau wa utawala wa al-Bashir.

Kwa vile nguvu ya itikadi ya kidini ilikuwa bado kubwa wakati yule, siyo Tunisia wala Misri ambako demokrasia iliinuka kikamilifu, ila sasa.

Chama cha watalaamu katika sekta mbalimbali nchini Sudan, ambacho ni kama mkusanyiko wa NGOs na watumishi serikalini na pia serikali za majimbo, bila kuhusisha vyama vya siasa, ndiyo walioratibu maandamano hayo na kusisitiza madai yake yatekelezwe na jeshi.

Vyama vya siasa vya Sudan vinategemea fedha kutoka wakubwa maeneo ya Ghuba na migawanyiko yao haina faida kidemokrasia kwani wana malengo mapana yenye kufanana na kutengana kidogo, kwa mfano kati ya chama cha National Islamic Front cha al Bashir na kile cha Umma, cha Sadik el-Mahdi. Itikadi yake ina tofauti za hapa na pale na NIF lakini siyo demokrasia.

Waziri wa Ulinzi wa aliyekuwa rais Bashir (ambaye ni mmoja ya waliokuwa wanatafutwa na Mahakama ya Kimataifa ya Jinai huko The Hague kwa kampeni na mauaji ya kuiba mifugo, kupora ardhi na kuua waliodiriki kupingana na vikundi vya wapanda farasi vya wabaguzi wa siasa kali huko Darfur, Kusini Magharibi ya nchi hiyo) ndiye aliyekuwa akijaribu kuongoza 'kipindi cha mpito.'

> Bado wanafanya jitihada ya kuwavuta watu katika chaneli za televisheni, redio na kurasa za mitandao, kuunga mkono itikadi za utumiaji nguvu wa kusimamisha sheria lakini hawasikilizwi; ni kizazi kipya kinachotaka demokrasia tu.

Watu zaidi ya 300,000 waliuawa huko Darfur ndipo mashtaka yakafunguliwa dhidi ya Rais al-Bashir, lakini jeshi, usalama wa taifa na vyama hafidhina vyenye uzalendo wa Sudan uliochanganyika na siasa kali walimpa 'tafu' al-Bashir. Hadi alipokwama yeye mwenyewe.

Ilikuwa ni kitu kinachokaribia kichekesho kusikia wakuu wa jeshi na taasisi za usalama wa taifa walivyokuwa wakijaribu kuihadaa dunia na wananchi wa Sudan kuhusu dhamira yao, au kudhania kuwa nchi zozote zile zitajitahidi kulinda kilichopo.

Hadi kufikia Jumapili, Wizara ya Ulinzi ilikuwa bado inafanya juhudi kuungwa mkono kimataifa, lakini matazamio hayo hayakuwa na mashiko kwani hakuna taifa linaloweza kuwashauri wananchi wa Sudan waache madai yao waliamini jeshi kuwa litatenda vyema, au lina nia ya kutenda haki.

Baadhi ya asasi za kimataifa au mahusiano na nchi kubwa yanategemea kuelewana na wananchi kwanza, basi.

Waziri wa Ulinzi wa al-Bashir, Jenarali Awad ibn Auf aling'olewa madarakani baada ya kudumu kwa siku moja, alipotangaza hali ya hatari na kutotembea kuanzia jua kuchwa hadi kucha ambayo wananchi waliipuuza na kubaki barabarani.

Alijua kuwa akitoa amri ya kuwapiga watu risasi kama al-Bashir alivyofanya wiki moja kabla hatafika kokote, tena angeingia kwenye matatizo kama ya Rais Hosni Mubarak ambaye alitumia nguvu watu wengi wakauawa ila jeshi likashindwa kuzuia 'tsunami' hivyo utawala wake ukaanguka.

Ni kufungwa maisha kwa makosa ya kuua waandamanaji kwa kudhamiria, mali zote kukamatwa, hata hofu ya kupigwa risasi si haba.

Jenerali Ibn Auf alikuwa aina ya kichekesho alipotangaza wakati wa kusisitiza kuwa aongoze kipindi cha mpito cha miaka miwili kuwa 'atang'oa mizizi ya utawala wa al-Bashir,' wakati ndiye shina na tawi kubwa la utawala huo.

Aliongoza vikosi vya Janjaweed kuwang'oa raia walio Waafrika zaidi kuliko wa maeneo ya Kaskazini wanaopenda kujiita Waarabu, na ndipo akapewa uongozi wa idara ya usalama wa taifa kabla ya uwaziri wa ulinzi.

Utawala wa al-Bashir ni pamoja na yeye mwenyewe na hata huyo aliyechukua nafasi yake kwenye kiti cha utawala wa muda wa jeshi ambao unapingwa na wananchi; hauna uwakilishi wa kiraia, ni jeshi na usalama tu.

Kinachotokea Sudan kinaweza kufananishwa katika maeneo mengine na kinachotokea Algeria kwani wananchi wameng'ang'ana kuwa jeshi liachie madaraka kikamilifu, iingie serikali ya mpito ya kiraia.

Waandishi wa habari wa BBC wakataka kujua kuna nafasi gani katika maandamano ya kung'oa utawala wa Mzee Bouteflika mwenye umri wa miaka 82 na alikuwa anataka muhula mwingine (kuilinda mianya ya rushwa) kwa kundi la siasa kali la FIS (National Salvation Front kwa Kifaransa) wakaambiwa hawana nafasi katika maandamano hayo.

Bado wanafanya jitihada ya kuwavuta watu katika chaneli za televisheni, redio na kurasa za mitandao, kuunga mkono itikadi za utumiaji nguvu wa kusimamisha sheria lakini hawasikilizwi; ni kizazi kipya kinachotaka demokrasia tu.

Mwandishi wa CNN, mwanadada Nima Elbagir ambaye wakati Rais al-Bashir anaingia madarakani alikuwa bado mtoto mdogo alionyesha mshangao wake kuwa mapinduzi halisi ya demokrasia yamefanyika, yanafanyika katika nchi ambayo haijawahi kuwa na uhuru kamili wa kisiasa.

Wandamanaji ni kizazi kilichokulia wakati wa utawala wa al-Bashiri na hawafahamu kiongozi mwingine ila yeye hivyo angeamini kuwa yeye ni baba yao na wangemsikiliza kwani amewakuza tangu wakuwa watoto.

Haikuwa hivyo, kwani kinachotokea katika nchi nyingine na kuonyeshwa katika mitandao kuwa 'inawezekana' ndicho kilichojiri, na siyo uzalendo wa siasa kali.



Rais Omar al-Bashir wa Sudan (katikati aliyenyanyua fimbo) ambaye amepinduliwa na Jeshi kufuatia maandamno ya wananchi waliotaka aondoke madarakani. **PICHA: MTANDAO**



Naibu Rais wa Kenya William Ruto katika moja ya mikutano yake. **PICHA: MTANDAO**

# Ruto ajimaliza; Akwama akitetea wala rushwa, ajilipua kudai hakuna njaa

**Na Ani Jozeni**

SIASA nchini Kenya na hasa hatima ya umoja katika chama tawala cha Jubilee inaelekea kuchukua mkondo wa kasi zaidi dhidi ya Naibu Rais William Ruto ambaye yuko katika mapambano kuokoa au kuendeleza uhusiano wa karibu na Rais Uhuru Kenyatta uliowafikisha madarakani mwaka 2013.

Baada ya 'kupeana mikono' kati ya Uhuru na kiongozi wa upinzani Raila Odinga mwezi Januari mwaka jana ili kuzuia hali isibadilike kuwa mbaya zaidi nchini humo, mpango wa utawala uliojificha wa pamoja kati ya Uhuru na Raila 'umekula' kwa naibu huyo.

Moja ya maeneo yanayompa shida ni vita dhidi ya rushwa ambayo Uhuru anaelekea kutoifanyia mzaha kabisa.

Takriban kila kigogo aliyesombwa na maji katika vita hiyo, iwe ni kwa kuondolewa tu madarakani au hata kufikishwa mahakamani ameonekana ni mtu wa karibu na Ruto, iwe ni kwa kutafuta nani awajibishwe kwa uangalifu, au ni uhalisia wa mahusiano halisi ya kiutawala.

Ruto amejikuta akikoromewa na watu wa Uhuru (yaani wenzake katika Jubilee) na watu wa Raila (upinzani kwa jumla au chama cha ODM cha Raila, licha ya migawanyiko katika upinzani na ODM kuhusu Ruto) aunge mkono vita dhidi ya rushwa.

Licha ya kuwa hawezi kuipinga moja kwa moja, anasema watu wake wanaandamwa, lakini hawezi kuthibitisha au kudau madai ni feki.

Moja ya maeneo ambayo yamekuwa mzigo kwa Ruto kuyatetea mbele ya wananchi na wafuasi wa Jubilee kwa jumla ni rushwa katika kampeni ya ujenzi wa mabwawa ya umwagiliaji kutokana na hali isiyoridhisha ya mvua.

Kati ya miradi kadhaa iliyotiwa saini mwaka 2017 na kutazamiwa kuchukua miezi 22, na hivyo baadhi ilitazamiwa imalizike kuelekea mwisho wa mwezi huu (Aprili 2019) hakuna hata mmoja uliosonga mbele na katika miradi kadhaa kuna mkanganyiko hata saini zinazoonekana zilikuwa kati ya nani na nani, kwani baadhi ya makabrasha ya tenda yalikuwa feki, na fedha zikalipwa kwa kampuni ambayo haikuwa katika mchakato wa tenda, zikapotea.

Tangu taarifa itoke katika vyombo vya habari kuwa Sh. bilioni 38 za Kenya (zaidi ya Sh. bilioni 800 za Tanzania) ziko hatarini kupotea kuhusu ujenzi wa mabwawa katika majimbo tofauti ya kiutawala nchini humo, wasomi na wafuatiliaji wa suala hilo wamepata kigugumizi.

Polisi wanachunguza kwa karibu mikataba kuhusu mabwawa matatu ya kuanzia, lakini mikataba mingine iko mbioni kuingizwa katika mchakato huo wa uchunguzi na kutafuta kama fedha zilizolipwa bado ziko katika akaunti husika au zilipotea bila kazi kufanywa, kukamilika.

Taarifa nyingine kuhusu suala hilo ilisema kuwa Mkurugenzi wa Makosa ya Jinai (DCI) ameagiza maofisa wa idara yake kuharakisha upelelezi wa miradi ya mabwawa ya maji yenye thamani ya Sh. bilioni 90 (za Kenya, hapa ni takriban shilingi trilioni mbili).

Inaelekea miradi ya Sh. bilioni 38 za Kenya ilikuwa ni mabwawa matatu ambayo polisi walianza kuchunguza, lakini kwa vile miradi hiyo ni mingi kiasi, kuna juhudi za kuangalia kila mradi na hesabu zake au utekelezaji wake, na karibu kila mahali 'madudu' yanaonekana.

Hali hiyo imekuwa mbaya kiasi ambacho mchakato mzima wa ujenzi wa mabwawa ya maji kukabiliana na ukame umesimamishwa.

Moja ya maeneo yaliyopigiwa kelele zaidi ni kuwa mikataba ya ujenzi wa mabwawa matatu ya kwanza kuanza kuchunguzwa ilionyesha mapengo ya wazi na ya kudhamiria yenye lengo la kumlinda mkandarasi huku ikimzamisha mlipa kodi, kulingana na ilichosema Kamati ya Bunge ya sekta ya maji.

> Jubilee inafahamu kuwa isipojiweka sawa kupambana na ufisadi upinzani unaweza kuchukua nafasi kubwa zaidi katika uchaguzi mkuu ujao, ila mtandao huo ni ngome ya kisiasa ya Ruto anayojaribu kuitetea ipasavyo.

Isitoshe, katika fungu hilo la Sh. bilioni 90 za kujenga mabwawa, sehemu isiyo ndogo ilikwishalipwa, wakati mkandarasi husika akiwa amechukua mikopo mikubwa ya benki ambayo inaelekea imehusishwa na kazi anayofanya, kana kwamba serikali itahakikisha mikopo hiyo kulipwa.

Ndiyo hapo wabunge wanashindwa kuelewa mikataba hiyo ilifikiwa kwa njia gani, na ni ngazi zipi za serikali zilihusika, wakati naibu rais alikuwa ndiye msimamizi wa miradi yote.

Magazeti ya Kenya yalieleza kuwa uchunguzi unaonyesha kuwa kampuni moja ya ujenzi iitwayo CMC Di Ravenna ya Italia ambayo ni mkandarasi tangulizi katika miradi ambayo sasa imesimamishwa, haikuwahi kuingia mkataba na taasisi za kitaifa nchini Kenya.

Badala yake, makabrasha tofauti ya tenda yalitiwa saini na kampuni za Italia, Afrika Kusini na Kenya.

Katika mkataba mmoja, mtu aitwaye Paulo Porcelli alitia saini mkataba wa Sh. bilioni 38.5 kwa ajili ya bwawa la Kimwarer jimbo la Marakwet, ila akiwakilisha CMC Di Ravenna ya Afrika Kusini, na siyo kampuni mama ya Italia.

Halafu akajiwakilisha mwenyewe kama wakala katika ujenzi wa bwawa linalogharimu Sh. bilioni 28 pia katika jimbo la Marakwet. Ni mikataba hewa, kimsingi.

Licha ya kuwa kampuni hiyo ya Afrika Kusini ni kampuni tanzu ya hiyo ya Italia, moja haiwezi kutia saini kwa niaba ya nyingine, hivyo kampuni ya Italia ya jina hilo hilo haitambui mikataba iliyoingiwa na mawakala wa ujenzi na maofisa wa mashirika ya maendeleo katika jimbo hilo, kwani haikuhusika na haikupeleka mwakilishi wake.

Halafu kampuni ya Afrika Kusini haina habari ya kilichotokea kwa sababu haikutoa saini na serikali au taassi ya kitaifa, na isitoshe aliyetia saini, licha ya kuwa wanamfahamu, alitia saini kwa kuwakilisha kampuni mama ya Italia, na siyo hii ya Afrika Kusini.

Endapo kuna tatizo ni lake na kampuni ya Italia, na siyo wao.

Ni katika mazingira hayo ambako polisi wanachunguza maofisa gani wa serikali na majimbo husika waliopokea milungula kutia saini mikataba feki ya aina hiyo, miradi hiyo ikiwa imetiwa saini Mei 5, 2017 bila mchakato wa kuridhisha wa tenda hizo.

Ujenzi ulitakiwa kuchukua miezi 60 na kwa hesabu za gazeti moja kubwa nchini humo ilikuwa Aprili 22 iwe ndiyo tarehe ya kukamilisha baadhi ya miradi, ila cha kushangaza ni kuwa hata michoro ya miradi hiyo, alipoulizwa mkandarasi husika, alisema bado haijafanyika.

Polisi walisema waliona mkanda wa fedha ulioanza baada ya mikataba hiyo kutiwa saini (ili wakandarasi wakope pesa za ujenzi kwa kutumia mikataba hiyo, na mikopo iwe imethibitishwa na serikali ya Kenya).

Wapelelezi waliona mkanda unaoanzia Nairobi kupitia London, benki ya Intesa SanPaolo ya Brazil na Uni-Credit zikiwa ndiyo wapasha moto kutolewa mikopo, pamoja na benki ya PNB Parisbas (ya Ufaransa, ila kwa tawi la Ubelgiji).

Waziri wa Maji Simon Chelugui amekuwa akijitetea kuwa hajafanya kosa lolote katika mkasa huo, akijaribu kutupia lawama maofisa wa majimbo au jimbo husika kwa ushauri waliotoa kwa wizara.

Kwa jina lake siyo vigumu kuona kuna uwezekano mkubwa kuwa ni mshirika wa karibu wa naibu rais, na ni watu wa aina hiyo wanaohusika moja kwa moja na ushawishi wa naibu rais na wanaobanwa katika masuala mazito ya rushwa.

Jubilee inafahamu kuwa isipojiweka sawa kupambana na ufisadi upinzani unaweza kuchukua nafasi kubwa zaidi katika uchaguzi mkuu ujao, ila mtandao huo ni ngome ya kisiasa ya Ruto anayojaribu kuitetea ipasavyo.

Halafu Ruto alijikuta akijikanganya alipodai kuwa taarifa za ukame na njaa katika maeneo tofauti ya nchi hiyo, na hasa maeneo ya Kaskazini na hasa eneo la Turkana ambao ni jamii ya Wakalenjin anaotegemea sana kura zao.

Alitangaza hadharani kuwa taarifa za vifo ni za kutunga, hali iliyosababisha sononeko na kulaaniwa na vyombo tofauti vya kiraia, na vyombo vya habari kupeleka waandishi kuonyesha kwa udani hali ilivyo.

Kwa vile wengi waliopatwa na balaa la njaa ni wapiga kura wake halafu anazuia nchi na dunia kuelewa hali ilivyo, ni wazi alidhihirisha kuwa siyo kiongozi makini bali mdau wa makubaliano ya juu juu na kufukia dukuduku, hata njaa.

MAKALA

Inatoka Uk.13

# ACT-WAZALENDO: Tuna plan B, iwapo Msajili...

Uamuzi wa Maalim Seif kujiunga wa ACT- Wazalendo kulifuatia uamuzi wa Mahakama Kuu ya Tanzania kumpa ushindi wa kumtambua kuwa mwenyekiti halali wa CUF, Prof. Ibrahim Lipumba.

Hiyo ilifuatia shauri lililokuwa limefunguliwa mahakamani hapo likihoji uenyekiti wake baada ya kuwa amejiuzulu.

Mwandishi wetu Enock Charles alifanya mahojiano na Kaimu Katibu Mkuu wa chama hicho, Dorothy Jonas Semu, Makao Makuu ya Chama hicho jijini Dar es Salaam.

Mahojiano yalijikita kuhusiana na muelekeo wa chama hicho baada ya kundi la Maalim Seif kujiunga na ACT- Wazalendo na pia ustawi wake kwenye siasa za Tanzania.

**Yafuatayo ni mahojiano hayo:**

**SWALI: ACT-Wazalendo ina mtazamo gani kuhusu kuzuiliwa kwa mikutano yake mbalimbali nchini?**

**JIBU:** Tunaona hizi ni jitihada za makusudi za chama tawala, kikitumia Jeshi la polisi kuzuia vikao halali vya ndani ambavyo sana sana tunatakiwa kutoa taarifa tu.

Na tukizingatia kwamba huu ni mwaka wa uchaguzi wa viongozi wa serikali za mitaa, hivyo hakuna jina rahisi la kusema zaidi ya kuwa huu ni uonevu, uminywaji wa demokrasia na uvunjwaji wa sheria kwa sababu tunajua nchi hii ni ya vyama vingi na ukuaji wa vyama unategemea mikutano ya nje na mikutano ya ndani.

Na mikutano yetu siyo siri, ni ya kawaida tu ya kuimarisha chama kama wao wanavyofanya mikutano ya kujiimarisha, wanapokea wanachama wapya tena wengine kutoka upinzani... na sisi pia tuna haki hiyo hiyo. Kwa hiyo sisi tunaona huo ni uonevu na hakuna fursa sawa kwa vyama.

Pia jeshi la polisi linakuwa lina-turn a blind eye (linafumba macho), yaani linajua kabisa kwamba hiyo ni haki yetu... hatujasikia jeshi la polisi likizuia mikutano ya Chama cha Wananchi (CUF), hatujasikia likizuia mikutano ya CCM.

**SWALI: Wanachama waliojiunga na ACT- Wazalendo kutoka Chama cha CUF ni wengi na wazito kisiasa. Je upo mpango wowote wa kuwapatia nafasi za uongozi?**

**JIBU:** Tumepata wanachama wengi wenye uzoefu mkubwa wa kujenga vyama, wenye uzoefu mkubwa wa kiuongozi... na wanachama hawa hata kabla hawajaja kwetu rasmi, nia yao ilikuwa ni kupata jukwaa la kisiasa na si nafasi za uongozi.

Hata hivyo, kama chama ni lazima tuone ule uwezo wao na kuutumia vizuri kukijenga chama chetu. Kwa hiyo tuliweka mpango jinsi ya kuwaweka kuwa sehemu ya chama ili waanze kufanya kazi na kukiimarisha chama.

Hiyo ni kwa maslahi ya chaguzi zilizoko mbele yetu na kuwa na chama bora ambacho kitaweza kupata platform (jukwaa) nzuri ya kushinda na kupata pia wanachama wengine wengi.

**SWALI: Kumekuwa na maazimio mbalimbali yakifanyika kutoka upinzani, mfano Azimio la Zanzibar n.k lakini utekelezaji wake ni wa kusuasua. Je kuna changamoto ipi?**

**JIBU:** Hakuna changamoto yoyote tofauti na maazimio mengine yaliyokuwa yanafanyika. Kutokana na uzoefu walioupata wenzetu walipokuwa wanafanya maazimio mbalimbali sasa hivi katika Azimio la Zanzibar, iliamriwa kwamba haya maazimio yaende yakapitishwe na kamati kuu za vyama.

> Tumefanya kazi na vyama vingine 10 katika kutoa maoni yetu kuhusu sheria ya vyama na jinsi ambavyo inachangia kudumaza siasa za upinzani na bado tunaendelea kushirikiana kwa kila hali. Kwa mfano sasa hivi tumepewa kanuni za uchaguzi wa serikali za mitaa, kwa hiyo tumekuwa tukifanya kazi kwa ushirikiano na vyama vyote.



Maalim Seif Sharif Hamad (wa tatu kushoto), akiwa pamoja na kiongozi wa ACT-Wazalendo (wa tatu kulia) na viongozi wengine wa ACT-Wazalendo. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**



Kaimu Katibu Mkuu wa ACT-Wazalendo, Dorothy Jonas Semu.

Kwa hiyo ni suala la summit (mkutano) kukutana kuangalia kwamba baada ya muda vyama vyote sasa vitoe mrejesho kwamba kamati kuu zao zimepitisha na kama kuna maboresho then (ndipo) twende kwenye hatua nyingine ya utekelezaji.

Kwa hiyo ni ndani ya muda mfupi, tutaona kamati kuu zimefikia wapi za vyama husika ambavyo vilikuwa sita na sasa vimebaki vitano... baada ya hapo tutajua na tutatangaza hatua nyingine inayofuata.

**SWALI: Mwaka 2015 ACT-Wazalendo iliingia katika uchaguzi bila kushirikiana na vyama vingine. Je chama kilipata uzoefu upi kuhusu hili?**

**JIBU:** Kwanza tulionekana kwamba sisi tumekwenda kugawa kura za upinzani na tukapewa dhana kwamba sisi ni CCM B kitu ambacho hakikutupendeza.

Lakini pia tuliona kuwa tumezigawa kura kweli na kweli kura ziligawika kwa kuwa wapinzani tulikuwa wengi na hiyo ipo documented (kinyaraka) kabisa. Unakuta sehemu nyingi kura za upinzani ni nyingi kuliko zile za chama tawala na hivyo zimegawanyika kutokana na wingi wetu.

Na uzoefu wa tatu ni kuwa na wagombea wengi na chama kichanga na hivyo kuwa na rasilimali chache za kuwasimamia wale watu na kuhakikisha kwamba tunakuwa effective (tija) na kupata kura nyingi. Kwa hiyo ni kwamba tulikuwa na watu wengi na kushindwa kufocus (kuwa na lengo) na hivyo kushindwa kupata zile kura ambazo tulizitegemea.

Tuliweka wagombea zaidi ya 250 wa ubunge... tulikuwa chama cha pili kuwa na wagombea wengi, ukilinganisha na vyama vilivyotutangulia na tulifanikiwa kupata jimbo moja na madiwani 30 hivi... kwa hiyo nafikiri ni uzoefu ambao ulitujenga.

**SWALI: Ni upi mkakati wa ACT- Wazalendo katika kushirikiana na vyama vingine?**

**JIBU:** Sisi tuliomba kuwa sehemu ya (Umoja wa Katiba ya Wananchi) Ukawa, lakini bado hatujapewa majibu rasmi ya kuwa sehemu ya Ukawa.

ACT-Wazalendo imekua ikiamini katika ushirikiano wa vyama na tumeendelea kufanya kazi na vyama vilivyo ndani ya Ukawa na vingine ambavyo viko nje ya Ukawa. Tumefanya kazi kwa mfano na Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) katika Jimbo la Buyungu.

Tumefanya kazi na vyama vingine 10 katika kutoa maoni yetu kuhusu sheria ya vyama na jinsi ambavyo inachangia kudumaza siasa za upinzani na bado tunaendelea kushirikiana kwa kila hali. Kwa mfano sasa hivi tumepewa kanuni za uchaguzi wa serikali za mitaa, kwa hiyo tumekuwa tukifanya kazi kwa ushirikiano na vyama vyote.

**SWALI: Dk. Bashiru Ally kabla ya kuwa Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi (CCM), alikuwa akionekana kuwa mshirika wa karibu wa ACT- Wazalendo. Je aliwahi kuwa mwanachama wenu?**

**JIBU:** Hilo sijui. Sisi tuna kitu tunakiita mkutano wa demokrasia ambapo tunakuwa tuna mada mbalimbali. Kwa hiyo tunaalika wataalam wenye uzoefu labda wa hizo mada.

Kwa mfano mwaka 2017, mada ya mkutano wetu wa kidemokrasia ilikuwa ni masuala ya Azimio la Arusha. Kwa hiyo ndugu Bashiru Ally alialikwa kutupa uzoefu wake wa-kiuanazuoni lakini pia aliweza kutupa maoni yake kuhusu chama chetu pale alipopenda kufanya hivyo.

Amekuwa ni rafiki wa ACT-Wazalendo na bado yupo huru kutoa maoni yake. Unajua mtaalam anapokupa maoni ya kitu si lazima awe ana-kipractice (anafanyia kazi), hiyo lazima tutofautishe sana. Kuna mtu kuamini na kuna mtu kutenda na kuna ile practical (uzoefu).

Lakini pia kitu kingine muhimu cha kunote (kuangalia), ni kwamba tusifanye siasa kuwa kama ni uadui. Kwa mfano kama mimi mwanasiasa ninaweza ku-comment (toa maoni) kwenye katiba ya chama kingine au kuwapa uzoefu wangu au hata kuwapa ushauri, yaani tufanye siasa kuwa ni kitu ambacho tuna- challenge (kosoa) sera, tuna challenge mawazo, tuna challenge matamanio ya watu kufika kwenye hiyo nchi ya ahadi.

Kwa baadhi ya wanasiasa wa Tanzania, ni kawaida kutenda tofauti na wanachoamini kutokana na kubanwa na mazingira.

**SWALI: Maalim Seif alipojiunga na ACT- Wazalendo, alipewa kadi namba moja. Je ni upi umuhimu wa kadi namba moja?**

**JIBU:** Kwanza sisi tuna policy (sera) tofauti sana kuhusu masuala ya kadi katika chama chetu. Kadi namba 1 mpaka 100 na 100 mpaka 1000 zilitengwa mahsusi kwa ajili ya kuongeza kipato cha chama.

Lakini kadi namba moja iliyotolewa kwa Maalim Seif symbolically (kiashara) kwa kuamini jitihada zake na mchango wake katika siasa za Tanzania na uzoefu wake katika kujenga demokrasia, hasa siasa hizi za upinzani. Kwa hiyo sisi tuliona kwetu kuwa ni heshima kumpata Maalim Seif ambaye ameamini katika katiba ya ACT-Wazalendo na kuamua kujiunga kama sehemu ya ACT.

**SWALI: Ukiwa kama kiongozi wa chama cha siasa. Je una mpango wowote wa kugombea ubunge?**

**JIBU:** Nia yangu ya kwanza ni kuwa sehemu ya chama chenye utendaji mzuri, chama ambacho kinasimamiwa na Katiba. Kwa hiyo nia yangu ni kuwa sehemu ya ujenzi wa chama na kukisaidia kiwe na taswira ambayo ni ya tofauti na ya kipekee kwenye usimamizi, kwenye jinsi wanachama wake wanavyokitumikia, jinsi wanachama wake wanavyotenda, jinsi kinavyofanya shughuli zake... kwa hiyo ndio ilikuwa nia yangu ya kwanza na muhimu.



Baadhi ya Wanachama wa chama cha ACT-Wazalendo.

Lakini najua baada ya hiyo lazima mwanasiasa uwe na mipango mingine... aah baadaye nitakuja kugombea ubunge kuanzia hata udiwani kwa sababu ndiyo fursa.

Lazima niingie kwenye michakato ya kuchaguliwa na wananchi, ili nipate fursa ya kutoa mchango wangu kwenye Bunge au Serikali za mitaa au udiwani n.k. Lakini lengo langu la kwanza hasa ni chama cha siasa.

**SWALI: Kabla ya kupewa nafasi hii ya kuwa Kaimu Katibu Mkuu, ulikuwa ukishikilia nafasi gani na Je, una mpango wowote wa kugombea nafasi yoyote ya juu katika chama?**

**JIBU:** Hehehe, ndio nina mpango wa kugombea. Kabla ya kuwa Kaimu Katibu Mkuu, nilikuwa katibu wa sera na mipango. Ilikuwa enzi hizo inaitwa sera, utafiti na mipango kuanzia mwaka 2015 na mpaka mwaka 2017, ndio nikapewa kukaimu u katibu mkuu au unataka na kabla ya hapo? Kabla ya hapo nilikuwa mtumishi serikalini. Nimekuwa mtumishi serikalini kwa miaka 17.

Nimefanya kazi kwenye program ya ukoma. Nilikuwa nasimamia watu wenye ulemavu wa ukoma kupata urakibishi. Halafu nikafanya kazi pia Taasisi ya Mifupa ya MOI, kama clinical physiotherapist... mimi ni m-phyisiorerapia.

**SWALI: Ni upi uzoefu wako katika elimu?**

**JIBU:** Nimesoma KCMC , Diploma miaka mitatu halafu nikaenda kusoma Afrika Kusini, inaitwa B.sc honors yaani unaunganisha ile Diploma inakuwa Degree. Halafu nikasoma pia na Shahada ya Pili (Masters of Science in Physiorephy, katika chuo kinaitwa Western Cape.

**SWALI: Mlifahamiana vipi na wapi na Kiongozi wako Mkuu wa chama?**

**JIBU:** Aah mimi nipo interested (navutiwa) na siasa siku nyingi kwa sababu nilijua siku moja nitakuja kuingia kwenye siasa, tena sio siku moja actually (hasa) niliandika sehemu kuwa nitakapofika miaka 40, nitakuwa active (najihusisha) kwenye siasa. Niliingia nikiwa na miaka 40, now am (sasa nina) 44.

Kwa hiyo wakati natafuta sasa chama cha kujiunga nikawa nataka kujiunga na chama kingine fulani, lakini ikawa tu inashindikana. Lakini nilishaanza kufuatilia kusoma sera zao nini, natafuta sasa where (wapi) ntaanza kufanya siasa.

Ukaibuka ule mgogoro wa lile andiko lililofanya Zitto wakafukuzwa na wenzake kina (Samson) Mwigamba na Kitila (profesa Mkumbo), kwa hiyo baadaye tukapata hiyo tetesi kwamba wameanzisha chama chao. Kwa hiyo nikawaomba kwamba naweza kujua hicho chama kikoje... wakati huo nikawa nimeshasoma mambo ya vyama vingine.

Kwa hiyo niliposoma hiki nikavutiwa, nikahisi kwamba ni more comfortable (kinafaa) kufanya kazi nao, kuchangia vile ambavyo navijua. Nilikuwa nafuatilia ile scenario (hali) na mimi kwangu nili-take side (nililalia upande) nikaona hawa ni watu tu walikuwa na mkakati wa kupata uenyekiti na kuongoza chama. Sikuona kama ilikuwa ni shida, kwa hiyo baadaye ndio nikasikia sasa wameamua kuanzisha chama cha siasa.

Kwa hiyo nikafuatilia lakini nafikiri exactly (haswa) kufahamiana na Zitto Kabwe ilikuwa ni twitter... palikuwa nafikiri kuna mjadala wa hisa za serikali na enzi hizo nafikiri alikuwa kwenye mambo ya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC). Kulikuwa kuna mjadala nafikiri ni kuhusu Mchuchuma or something (au kitu) akawa anasema serikali ina hisa 25.

Sasa tukawa tunahoji na mimi nilimuhoji ni kwanini serikali ina hisa asilimia 25... kwanini siyo 40 au 55, yaani mmekujaje na hii figure (tarakimu) ya 25 why not (kwa nini siyo) 40 na sisi hiyo migodi ni yetu. Na imekuwa ni kawaida mpaka leo kila mahali serikali inapoingia ubia tunaanza kulaumu, tumekuwa tunaonewa na kuwa na hisa chache.



Msajili wa Vyama vya Siasa nchini, Jaji Francis Mutungi.

**SWALI: Ukiwa kama kiongozi wa chama na mama wa familia, unawezaje kugawa muda wako?**

**JIBU:** Kwa kweli hapo kwenye muda ni tough (ngumu) na siwezi kusema kwamba niko perfect (kamilifu) kwa sababu siku zingine kazi za ofisi zinanilemea, hiyo huwezi ku-avoid (kuzuia) hasa kwenye siasa. Ninachojitahidi kufanya ni kutenga muda ili ninapokuwa nyumbani niwe mama na ninapokuwa ofisini nifanye kazi za ofisi... lakini ninasaidiwa sana na mume wangu.

**SWALI : Ni hatua ipi mtayakayoichukua iwapo msajili wa vyama vya siasa atakifuta chama chenu?**

**JIBU:** Tuna plan (mpango) B, ila siwezi kuisema kwa sasa kwa kuwa bado msajili hajafanya hivyo. Hiki ni chama cha siasa ambacho kipo kwa mujibu wa sheria.

**SWALI: Je hamuoni kuwa kitendo cha kumpokea Maalim Seif ndicho kilichowaletea matatizo?**

**JIBU:** Changamoto za aina hiyo zipo siku zote hata kabla ya ujio wa Maalim Seif, sema kwa sasa zinaonekana katika large scope (kwa uwanda mpana), mfano kama sasa tuna miezi takriban 11 bila ya ruzuku, zote hizi ni jitihada za makusudi za kutukwamisha.

# Mafunzo ya uongozi, maisha kutoka kwa Njelu Kasaka- 2

**Na Mwandishi Wetu**

KATIKA makala iliyopita, ilielezwa kuwa mwanasiasa mkongwe nchini, Njelu Kasaka, kupitia kitabu chake cha 'Njelu Kasaka Maisha, Siasa na Hoja ya Tanganyika- G55' anatoa mafunzo ambayo yana maana kubwa katika nyanja zote za maisha.

Sehemu hii ambayo ni mwendelezo wa makala hiyo, inabainisha zaidi mafunzo ya mwanasiasa hiyo ambaye katika utumishi wake aliwahi kuwa meneja wa benki ya CRDB, Mbunge, Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Ushirika, Mkuu wa Mkoa na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge Fedha na Uchumi.

Kasaka, ambaye katika miaka ya 1990 alijiibulia umaarufu kutokana na hoja yake ya kuanzishwa kwa serikali ya Tanganyika na hatimaye Bunge kuitisha azimio la kuundwa kwake, anaonyesha picha halisi juu ya uwezo wa kusimamia jambo na kuwa na msimamo kama makala iliyopita ilivyoeleza.

Pamoja na mambo hayo, Kasaka anabainisha mambo ambayo mtu anapaswa kufanya ili kujijengea heshima miongoni mwa mambo hayo ni;

**WAJIBU WA KIONGOZI**

Katika eneo hilo, Kasaka anafundisha kuwa mtu anapokuwa kiongozi anapaswa kwanza kufuata taratibu na kanuni katika eneo husika. Alipokuwa mbunge, kwa mfano, alipofuatilia suala la umeme Chunya makao makuu ya Shirika la Umeme Tanzania (Tanesco), alielezwa kuwa kuna taratibu za kufuatwa.

Pamoja na kuelezwa hali hiyo, anaeleza kuwa alifuatilia suala hilo iliyokuwa Wizara ya Maji, Nishati na Madini kwa ajili ya kuhakikisha suala hilo linaingizwa katika bajeti ya serikali kwa mwaka husika.

Baada ya kufika wizarani, alijibiwa kuwa anapaswa kufuatilia Wizara ya Mipango ambako ndiko wanakohusika na kuweka mambo kulingana na vipaumbele na alipofika huko alielezwa kuwa hata likiwekwa anapaswa kwenda Wizara ya Fedha ili lipewe kipaumbele katika bajeti.

Kutokana na ufuatiliaji huo, jambo hilo lilirejeshwa Tanesco ambako liliwekwa kwenye mpango wa utekelezaji na hatimaye umeme kuwashwa rasmi katika mji wa Chunya Desemba 24, 1994.

Kutokana na ufuatiliaji huo hadi jambo kukamilika, fundisho lililopo ni kwamba mtu anapofuatilia jambo, ama binafsi au la umma, anapaswa kufuata taratibu zinazotakiwa pamoja na kujua nani anahusika na nini.

**KUKABILI CHANGAMOTO**

Katika kipindi chake cha uongozi, Kasaka alikumbana na changamoto mbalimbali na alizikabili ipasavyo. Alipokuwa Mkuu wa Mkoa wa Iringa, kwa mfano, anasema alikutana na changamoto tatu ambazo ni kipindupindu, wananchi kutumia maji machafu kutoka Mto Ruaha Mdogo na barabara kuu ya Tunduma- Dar es Salaam eneo la Iringa kuharibika kutokana na El-Nino.

"Nilipokabidhiwa ofisi nilibaini mambo mtatu kwenye taarifa ya mtangulizi wangu... kwanza, wananchi wa Manispaa ya Iringa walikuwa wanakunywa maji machafu yasiyo salama. Hata nyumbani mwa Mkuu wa Mkoa yalikuwa yanafika maji mchafu yasiyochujwa wala kuwekwa dawa za kuua vijidudu.

"Pili, katika msimu uliopita, zaidi ya wananchi 2,000 waliugua kipundupindu na kusababisha kuwapo kambi maalum ya wagonjwa wa kipindupindu mjini Iringa... Kutokana na umuhimu wake, niliamua kuyashughulikia matatizo hayo mara moja, " anasema.

"Alifurahi sana kuniona kwenye kiti cha Mkuu wa Mkoa... Safari hii Mfikwa alifika na falsafa nyingine. Aliniambia niwe mwangalifu na watu wanaojenga urafiki na mimi. Kuna watu watafika hapa kumwona na kufanya urafiki na Mkuu wa Mkoa na wengine watakuja kumwona na kufanya urafiki na Njelu Kasaka ambaye ni Mkuu wa Mkoa."

Hata alipohamishwa kutoka Iringa kwenda kuwa Mkuu wa Mkoa wa Tabora, anasema alikutana na changamoto nyingi kubwa zaidi ikiwa mgogoro baina ya wakulima wa tumbaku, Chama Kikuu cha Ushirika cha Wakulima wa Tumbaku (Wetcu) na kampuni za ununuzi wa zao hilo.

Kutokana na changamoto hiyo alisimama kidete kuhakikisha matatizo yaliyokuwa yanaikumba sekta hiyo yanatatuliwa haraka na kuwawezesha wakulima kunufaika na jasho lao.

"Katika msimu wa 1998/99 vyama vya msingi tisa viligoma kuuza tumbaku yao kwa kampuni zinazotoa pembejeo kwa makubaliano ya kuuziwa tumbaku. Mfanyabiashara kutoka Dar es Salaam, Haji Mugishagwe, aliwaahidi wakulima kuwapelekea kampuni itakayonunua tumbaku yao kwa bei kubwa kuliko zinavyolipa kampuni zenye mikataba.

"Wakulima walishawishika na kutaka kuvunja mikataba na kampuni zinazonunua tumbaku miaka yote. Mgogoro huo bila kupatiwa ufumbuzi mzuri, ulikuwa na athari ya kuvuruga kilimo cha tumbaku mkoani Tabora," anasema.

Ili kuhakikisha mgogoro huo unatatuliwa, Kasaka anasema aliitisha vikao mbalimbali ndani ya ofisi yake, Wetcu na wanachama wake vikiwamo vyama tisa vilivyogoma na baadaye kuitisha mkutano wa wadau waliotoa maoni juu ya nini cha kufanya.

"Mkutano ulitoa ufumbuzi kwa kukubaliana kwamba vyama lazima viheshimu mikataba viliotia saini na kampuni na kwamba kampuni inayotaka kununua tumbaku lazima ianze na wakulima tangu mwanzo wa msimu.

"Kampuni iliyojitokeza ilikatazwa kwenda vijijini kuzungumza na vyama vya ushirika katikati ya msimu. Katika kuimarisha katazo hilo, niliagiza atakayekaidi akamatwe na hatua za kisheria zichukuliwe dhidi yake, " anabainisha.

**KUACHA UNAFIKI**

Tatizo la unafiki linawaandama watu wengi katika jamii ya sasa ya Kitanzania ama kwa sababu ya maslahi binafsi au nidhamu ya uoga. Wakati wa vuguvugu la kudai serikali ya Tanganyika, baadhi ya wabunge waliokuwa wanaunda kundi la G55, walijitoa kwa sababu mbalimbali.

Kasaka katika kitabu chake anamtaja aliyekuwa Mbunge wa Chilonwa mkoani Dodoma, Donald Kusenha, na mwenzake Dk. Chinuno Magoti (Taifa) walitangaza kujitoa kutokana na sababu mbalimbali.

Kusenha, kwa mujibu wa Kasaka, alisema alichukua uamuzi huo kwa sababu aliyekuwa Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais, John Malecela, wanatoka mkoa moja. Dk. Magoti kwa upande wake alisema anajitoa kwa sababu anatoka Mara sambamba na Mwalimu Julius Nyerere, hivyo kutofautiana kwake kutamfanya asieleweke.

Viongozi hao wawili ambao mwanzo walijiunga na kundi hilo kwa hiari yao wanaonyesha wasivyo na msimamo na ujasiri katika mambo wanayoyaamini. Kwa maneno mengine ni vigeugeu au wanafiki.

Tatizo kama hilo limewakumba watu wengi ndani ya jamii na hata kushindwa kueleweka wana msimamo gani kwani wanakuwa kama bendera fuata upepo- kila uvumiako wao wapo.

**KUWA NA MSIMAMO**

Kiongozi au mtu yeyote anapaswa kuwa na msimamo juu ya kile anachokiamini na kukiishi hata kama kuna watu wa juu yake watamtisha au kumshinikiza abadili msimamo wake.

Katika funzo hilo, Kasaka anabainisha pale alipokuwa Meneja wa CRDB Mkoa wa Iringa alipoweka msimamo wa kumfukuza mmoja wa maofisa wake kutokana na makosa mbalimbali.

Anasema kutokana na uamuzi huo, ofisa huyo alikwenda hadi makao makuu kulalamika kuwa anaonewa na kusababisha viongozi wa ngazi za juu wa benki, kwenda kujaribu kumtaka abadili msimamo wake lakini alisimamia jambo hilo hadi ofisa huyo alipofukuzwa kazi.

**KUCHUKUA TAHADHARI**

Jambo lingine ambalo mwanasiasa huyo mkongwe anaifundisha jamii ni juu ya kuchukua tahadhari katika kila jambo. Mfano wa tahadhari ambayo anaielezea ni ile ya G55 walipoambiwa wanaitwa na watu wasiojulikana wakati wa suala ya Tanganyika. Katika hali hiyo anasema walichukua tahadhari hata kusita kwenda kuonana na watu hao.

Pia anaiasa jamii kuwa makini hususan mtu anapokuwa na nafasi katika jamii kwani anaweza kujipatia marafiki wengi lakini wote si wakweli bali wako kwa maslahi binafsi. Kwa maneno mengine baadhi ya watu hao watataka urafiki kwa sababu ya nafasi aliyoanayo.

Kasaka anatoa mfano wa Mzee John Mfikwa, aliyekuwa rafiki yake mkubwa alipokuwa Meneja wa CRDB Mkoa wa Iringa, aliyempa wosia juu ya kuchukua tahadhari kuhusu watu watakaomwendea akitekeleza majukumu yake.

"Nilipofika Iringa nikiwa Mkuu wa Mkoa, siku moja rafiki yangu John Mfikwa, mfanyabiashara niliyemuaga mwaka 1990 wakati naacha kazi CRDB kwenda Chunya kugombea ubunge, alifika ofisini kwangu kunisalimu.

"Alifurahi sana kuniona kwenye kiti cha Mkuu wa Mkoa... Safari hii Mfikwa alifika na falsafa nyingine. Aliniambia niwe mwangalifu na watu wanaojenga urafiki na mimi. Kuna watu watafika hapa kumwona na kufanya urafiki na Mkuu wa Mkoa na wengine watakuja kumwona na kufanya urafiki na Njelu Kasaka ambaye ni Mkuu wa Mkoa.


"Alisema utakapotoka kwenye kiti cha Mkuu wa Mkoa, marafiki wa Mkuu wa Mkoa hutawaona tena lakini waliofika kwa Njelu Kasaka, Mkuu wa Mkoa, utaendelea kuwaona," anasema.



Njelu Kasaka

Na Mashaka Mgeta

# Tshisekedi na kiu ya amani, maendeleo ya Afrika



Rais wa DRC, Felix Tshisekedi, akisaini kitabu cha wageni Ikulu ya Entebbe nchini Uganda. PICHA:MTANDAO

ALIPOTANGAZWA kuwa mshindi wa kiti cha urais katika Uchaguzi Mkuu wa Desemba 30 mwaka jana nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Felix Tshisekedi alitabiriwa kuwa kiongozi asiyekuwa na 'jipya', isipokuwa kuziendeleza fikra za mtangulizi wake, Joseph Kabila.

Hali hiyo ilitokana na madai hasa ya upinzani nchini humo, kwamba Rais Tshisekedi alipanga njama na Kabila ili kuhujumu uchaguzi huo na hivyo kuibuka na ushindi usiotokana na matakwa ya raia wengi wa nchini humo.

Lakini akiwa jijini Kigali nchini Rwanda alipokuwa akishiriki Mkutano wa Kimataifa wa Kibiashara, Rais Tshisekedi ameonyesha uwezo wake wa kifikra na namna anavyoweza kuchagiza harakati za amani, utulivu na maendeleo kwa DRC, ukanda wa Maziwa Makuu na Afrika kwa ujumla.

Akiiangazia DRC chini ya utawaka wake, Rais Tshisekedi anaonyesha mwelekeo wa kulitoa taifa hilo kwenye wimbi la vurugu, machafuko ya kisiasa na mauaji ya yenyewe kwa wenyewe, akipitia njia ya kujibu mahitaji wa raia wake.

Alikuwa akizungumzia mwelekeo mpya wa DRC kwa upande wa ndani na nje ya mipaka yake, ikianzia kwa nchi jirani, zilizo mfano wa chemchem ya migogoro inayoliathiri eneo la Maziwa Makuu.

Jawabu lenye kutoa taswira ya 'DRC mpya' kutoka kwa Rais Tshisekedi ni kutambua umaskini unaowakabili wananchi, matumizi sahihi na rasilimali na kukomesha migogoro hasa ya kisiasa.

Anasema kuwapo kwa migogoro kati ya mataifa hakuwezi kuondoa ukweli kuhusu ujirani uliopo kati ya mataifa hayo na kwamba wahusika wa migogoro wanapaswa kutambua kwamba wao watapita, lakini mataifa hayo na raia wake wataendelea kuwapo.

Anasema, "vita ndogondogo na migogoro havina maana kabisa na vinatupotezea muda kabisa, tunapaswa kuutumia muda huo kushughulikia mahitaji ya wananchi wetu," anasema Rais huyo wa taifa lenye rasilimali nyingi hasa madini na misitu, lakini pia likikabiliwa na migogoro ya mara kwa mara.

### MIGOGORO AFRIKA

Rais Tshisekedi anasema inawezekana kwa nchi za Afrika kuondokana na migogoro na chuki zilizojikita kwenye mioyo ya raia, akitolea mfano wa mafanikio yaliyofikiwa na Rwanda chini ya Rais Paul Kagame.

Anasema mafanikio hayo anatamani yatokee nchini DRC na namna Rais Kagame alivyoitoa jamii yake kwenye fikra za kulipiza visasi baada ya mauaji ya halaiki ya mwaka 1994 na kuwa mfano bora wa taifa lenye mafanikio ya kibiashara na kisiasa.

### WAASI WA DRC

Rais Tshisekedi anatambua kuwapo hatari ya vikundi vya waasi nchini kwake, lakini anasema kwa mtazamo wake, vikundi hivyo haviunganishwi kwa matakwa ya kiitikadi bali maslahi ya kibiashara.

Kwa mujibu wa Rais Tshisekedi, vikundi vya aina hiyo vinawajumuisha wafanyabiashara wadogo na majangili wanaotorosha rasilimali kama vile madini na mazao ya misitu hasa mbao kwa njia haramu.

Kwa mujibu wa takwimu za taifa zinazohusu misitu, asilimia 67 ya eneo zima la DRC linalokadiriwa kuwa na ukubwa wa hekta milioni 155.5 lina misitu, kati ya hizo, hekta milioni 99 zikiwa na 'misitu minene' inayosababisha mvua.

Misitu hiyo ya DRC inasadikiwa kuwa sawa na nusu ya misitu yote inayosababisha mvua barani Afrika

Rais Tshisekedi anasema majangili wanaotorosha rasilimali hizo wanapata usaidizi wa raia, hali inayosababishwa na changamoto zinazowakabili wenyeji wa DRC ikiwamo ukosefu wa ajira, hivyo namna inayofaa ni pamoja na kuhusisha vitendo hivyo na uhalisia wa maisha ya watu kupitia ushirikiano wa kikanda.

### MIRADI YA MAENDELEO

Anasema yapo mambo mema na yenye manufaa kwa waafrika hususani katika ukanda wa maziwa makuu kuyafanyia kazi, akitoa mfano wa uchimbaji wa gesi kwenye Ziwa Kivu lilipo nchini Rwanda karibu na mpaka wake na DRC na mradi wa kuzalisha umeme kwa kutumia maji ya Mto Rusizi ili kutanua wigo wa kukua kwa uchumi wa mataifa hayo.

Mto Rusizi unatiririsha maji yake Kusini mwa Ziwa Kivu, Mashariki mwa Afrika ya Kati kupitia eneo lenye mipaka kwa nchi za DRC, Rwanda na Burundi. Pia unatokea ziwani Mashariki mwa Bukavu katika DRC na kutiririsha maji umbali wa kilomita 160 Kusini mwa Ziwa Tanganyika.

Rais Tshisekedi anasema ushirikiano wa kikanda ni nyenzo muhimu katika kukabiliana na migogoro, hivyo unapaswa kutanuliwa hadi kuwezeshana katika masuala yanayohusu rasilimali.

Akatoa mfano wa nchi yake kwamba ipo tayari kutoa rasilimali na fursa nyinginezo kwa mataifa jirani ya kiafrika, miongoni mwa hayo ni Mto Congo unaweza kutumika katika kupunguza migogoro inayotokana na Mto Nile kama uliopo kati ya Ethiopia na Misri, kuhusu ujenzi wa bwawa wa Grand Renaissance.

Misri inalalamikia ujenzi wa bwawa hilo lililopo Ethiopia kwa maelezo kwamba litaathiri mfumo wa maji kwenye mto Nile, lakini Ethiopia inakana madai hayo.

Nchi hizo pamoja na Sudan zimeshafanya mikutano kadhaa kuhusu mradi wa uzalishaji umeme kwa kutumia maji kwenye bwawa hilo utakaogharimu Dola bilioni nne za Marekani, lakini hakuna suluhu iliyopatikana.

Mto Congo kupitia bwawa la Inga, unakusudiwa kuzalisha kiasi cha megawati 44, 0000 za umeme baada ya ujenzi wake kukamilika katika awamu nane.

Pia anasema kuna vyanzo 100 nchini DRC vinavyoweza kuzalisha umeme wa megawati 16,000, nishati ambayo inaweza kusambazwa barani Afrika na hivyo kusaidia mipango ya kudhibiti upungufu uliopo, unaokwamisha jitihada za maendeleo ya viwanda.

Rais Tshisekedi anaongeza kuwa vyanzo hivyo vitakuwa nyenzo muhimu katika kutatua kero na migogoro inayohusiana na maji hasa katika Mto Nile.

Kwa mujibu wa Rais Tshisekedi, maji yanayotoka Mto Congo yanaweza kusukumwa kwenda Mto Chad kupitia mradi wa transaqua unaowanufaisha watu zaidi ya milioni 20.

### UTATUZI WA MIGOGORO

Rais Tshisekedi anaamini kwamba mazungumzo ni njia muhimu ya kuondoa migogoro na kuweka hali ya utulivu iliyo msingi mkubwa katika kufanikisha utengamano kupitia eneo huru la biashara barani Afrika (AfCFTA)

Rais Tshisekedi anaamini kwamba ushirikiano thabiti wa kikanda utasaidia kuondokana na kero za maji na nishati. Anasema nchi zilizo kwenye ukanda huo zinapaswa kujikita zaidi katika masuala muhimu yanayowaunganisha kwa maslahi ya nchi zao kama KIVU

Februari mwaka huu, Rwanda ilisaini makubaliano ya kuzalisha gesi kwenye Ziwa Kivu kupitia mradi wenye thamani ya Dola milioni 400 za Marekani. Mradi huo unaoendeshwa na kampuni ya Gasmeth Energy utachimba gesi kwenye kina kirefu cha ziwa hilo na kuisindika ili itumike kama mafuta.

**Makala haya yameandikwa kutoka vyanzo mbalimbali. Mwandishi anapatikana kwa simu namba +255 754 691540 ama barua pepe:mgeta2000@yahoo.com.**

MAKALA

# Ulaya waipa Uingereza miezi sita, May atafuta msaada wa Corbyn

Na Nimi Mweta

NCHI 27 za Umoja wa Ulaya (EU) zimewapa viongozi wa vyama vya siasa vinavyohitilafiana katika Bunge la Uingereza kuhusu mpango wa kujitoa katika umoja huo, miezi sita mingine wafikie muafaka unaoendana na kilichokubaliwa kati ya Uingereza na umoja huo.

Mkataba tarajiwa wa kujitoa umeshindwa kuafikiwa baada ya Bunge kukataa mara tatu mapendekezo ya Waziri Mkuu Theresa May ambayo yanaendana na 'mistari' ya EU kuhusu kisichoweza kujadiliwa tena.

Kilichobaki ni kuwapa Waingereza muda wa kutosha kufikia uelewano wao kwa wao, na badala ya Juni 30 alizopendekeza Waziri Mkuu May, wakapewa miezi sita.

Bado kuna kitendawili kama baada ya muda huo kupita Uingereza itakuwa imefanikiwa kupata muafaka, au italazimika kufanya kura nyingine ya maoni kuhusu suala hilo, licha ya kuwa kura kama hiyo pia inaweza isitoe jibu halisi.

Itakuwa ni kura ya dhamira ya kujitoa, ambako hadi sasa hakuna mabadiliko ya wazi katika Bunge la Uingereza, kuwa labda wapiga kura wao sasa wamepata picha tofauti ya nini kinapaswa kufanyika, hivyo dhana ya kupata matokeo mengine haina nguvu bungeni hivi sasa.

Ndiyo maana mkakati wa May kuanza majadiliano na chama cha upinzani, Labour kuhusu nini kifanyike ni hatua muhimu ila ni miiba tu kufikia muafaka wowote.

Wakati mjadala wa makubaliano na EU unafanyika bungeni tena kwa mizunguko isiyoisha, mgawanyiko katika Bunge hilo umejipambanua katika maeneo mawili.

Kundi la kwanza ni la wanaohofia kuwa mkataba huo unaibakiza Uingereza kwa nguvu mno wakati inatakiwa itoke haraka, wakati kundi la pili linahofia kuwa mkataba huo unafanya Uingereza iwe na uhusiano dhaifu kibiashara na Ulaya, hautoi uhakika wa kuuza bidhaa za Uingereza na kutetea haki ya raia wa Uingereza walioko maeneo mengi barani Ulaya.

Zaidi huo ni msimamo wa chama cha Labour, ambako bado kinataka au hakipingi Uingereza kujitoa, ila kwa 'mkataba bora.'

Labda ni hapo kutakuwa na mtihani kwa Waingereza kuamua kama bado wanatazamia upatikane 'mkataba bora' unaokubalika na pande zote za kisiasa nchini humo jambo ambalo haliwezekani au wakubali nchi hiyo itoke katika umoja huo bila mkataba.

Cha kushangaza ni kuwa Bunge la Uingereza lilipiga kura hivi karibuni kuainisha dhamira ya kutojitoa Umoja wa Ulaya bila mkataba, ila azimio hilo halikubadili nia za wabunge wa vyama tofauti kuhusu mkataba wanaotaka, au kuukubali mkataba uliofikiwa kati ya May na kiongozi wa ujumbe wa EU katika majadiliano hayo, Michel Barnier.

Kila chama kina mkataba kinaotaka, Kusadikika.

May ametafuta kila njia kuondoa mgawanyiko huo bungeni kabla ya kuomba urefushaji wa muda wa kujitoa Uingereza ambao awali ulikuwa ukamilike Machi 29 mwaka huu, halafu Ulaya ikasema utaishia Aprili 12 kama hakuna mkataba na Mei 12 kama upo mkataba.



Waziri Mkuu wa Uingereza, Theresa May, akiwa Makao Makuu ya Umoja wa Ulaya (EU), nchi yake iliongezewa miezi sita kufikia mkataba wa kujitoa EU. **PICHA: MTANDAO**

> "Akikwama katika mazungumzo na Labour, tena si ajabu ndani ya wiki mbili au tatu zijazo, May itabidi arudi kwa Conservative, ili waafikiane kama wanajitoa kwa mkataba uliopo au bila mkataba.

Baada ya Bunge la Uingereza kufikia Aprili 10 bila muafaka wowote, halafu May akafika miji mikuu ya nchi muhimu za umoja huo kuomba aongezewe muda hadi Juni 30, inaelekea umoja huo uliona kuwa hatua hiyo haitasaidia.

Kwa maana hiyo waliwasiliana wao kwa wao kupata msimamo wa pamoja kutoa nafasi pana ili wasisumbuliwe kila kukicha na maombi ya kuongezewa muda tena.

Akizungumzia mgawanyiko huo na jinsi unavyokwama kutoa picha ya dhamira ya pamoja kama nchi au taifa kwa suala la kujitoa EU, May alisema wiki chache zilizopita kuwa wabunge 'wanajua wasichokitaka ila hawajui wanachotaka,' kwa maana kuwa ni rahisi kwao kukubaliana kuhusu nini hawataki.

Hawana uwezo wa kukubaliana kuhusu wanachotaka, kwani likitolewa pendekezo lolote, wabunge walio wengi wanalikataa, kwa sababu zinazotofautiana.

Mpango wa pili wa kujitoa uliafikiwa na Umoja wa Ulaya baada ya ule wa kwanza kukataliwa kwa kura nyingi, yakatolewa mapendekezo nane ya njia nyingine yakapigiwa kura, yakakwama yote.

Wakati ambapo May ameanza mazungumzo na kiongozi wa Labour, Jeremy Corbin kuhusu mpangilio wa kujitoa unaoweza kupata kura nyingi bungeni, bado wachunguzi wa habari hawaamini kuwa majadiliano hayo yanaweza kuzaa matunda.

Iweje wabunge wa Conservative wamkatalie mara kadhaa May kwa mkataba na Ulaya uliosimamiwa na kujadiliwa na mawaziri wa chama chao, halafu wakubali kupokea mpango mbadala unaotokana na mapendekezo ya Labour?

Ili mpango huo uendane na nafasi ya May kama kiongozi wa chama cha Conservative, inabidi ulinde vipengere muhimu kwa Conservatives ambavyo Labour hawatavikubali kamwe.

Kimsingi hapa inaelekea kuna kosa la kiufundi ambalo si ajabu May anaelekea kulifanya hivi sasa, ingawa hali hiyo bado haijadhihirika kikamilifu.

Ni kuwa angetafuta kwanza muafaka ndani ya Conservative ni mpango gani ambao wanaweza kuupigia kura wote kwani wana wingi wa viti bungeni ila kwa ufinyu kuliko mwanzoni.

Kwa maana hiyo tatizo siyo kuwa Labour wanapinga makubaliano May aliyofikia na umoja huo, kwani hali hiyo ni kawaida ya chama tawala na upinzani, ila kukosa kuungwa mkono na kipande kikubwa tu cha wabunge wa chama chake, Conservative.

Angeondoa hitilafu hiyo angekamilisha mchakato wa Brexit mapema zaidi ya sasa.

Kwa maana hiyo kuna miezi sita ambayo itamwezesha May kufikia tamati ya mchakato wa Brexit kwa njia yoyote ile, na ziko njia mbili zinazoonekana au tuseme tatu zinazowekwa mezani na moja itapita.

Njia ya kwanza ni hatua hii ya May kutafuta muafaka na Corbyn kuhusu jinsi ya kujitoa, ambayo kwa hali yoyote ni lazima ikwame kwani Corbyn hana nia ya kumsaidia May katika suala hilo; akiweza kulazimisha uchaguzi mkuu mpya ili suala hilo limalizwe na wapiga kura, au kura nyingine ya maoni kuhusu kujitoa Ulaya, ni jambo la heri kwake kuliko kujikana mwenyewe. Yaani, misimamo yake yote hadi sasa, amsaidie May kwa kinachodaiwa ni maslahi ya taifa.

Kwa hali hiyo inaelekea kuwa Waziri Mkuu May ni kama 'anazunguka mbuyu' kushindwa kutafuta kwa nguvu zaidi maafikiano ndani ya Conservative, na kuhangaika kuafikiana na Labour wakati wao wanataka wamtose kwenye uchaguzi mkuu mwingine kwa suala hilo.

Akikwama katika mazungumzo na Labour, tena si ajabu ndani ya wiki mbili au tatu zijazo, May itabidi arudi kwa Conservative, ili waafikiane kama wanajitoa kwa mkataba uliopo au bila mkataba.

Endapo wataafikiana kujitoa kwa mkataba itabidi waafikiane kuhusu mkataba uliopo au kitu kama ushuru wa forodha endapo EU itaafiki, au sivyo wajitoe bila mkataba na bila kukubaliana.

Hapo itakuwa ni suala la hatua kadhaa za forodha na mikataba na nchi tofauti, chini ya mfumo uliowekwa kwa mikataba ya biashara duniani; ni pamoja na kukaribiana zaidi na Marekani, au hata China kupitia Belt & Road.



# Waajiri watakiwa kupima afya za wafanyakazi

**Na Mwandishi Wetu, SONGWE**

WAKALA wa Usalama na Afya Mahala pa Kazi (Osha) Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini, umewataka waajiri kupima afya za wafanyakazi wao wanapowaajiri ili kuepukana na changamoto zinazojitokeza mara kwa mara kwenye mazingira ya kazi.

Kauli hiyo ilitolewa mwishoni mwa wiki na Meneja wa Osha, mikoa, Faston Mwakajwanga, wakati akitoa elimu kwenye kongamano la wamiliki wa viwanda na wajasiliamali ambalo limeandaliwa na mkoa wa Songwe.

Mwakajwanga alisema baadhi ya wafanyakazi huugua magonjwa ya Moyo, kisukari na Presha wakiwa kazini na kusababisha kupoteza maisha hivyo utaratibu wa kuwapima afya wanapopata ajira utasaidia kuwatengenezea mazingira rafiki ili kuendelea kufanya kazi pasipokupata madhira yeyote.

Alisema utaratibu wa waajiri kuwapima afya wafanyakazi wao hasa katika maeneo ya viwanda ni muhimu kwa sababu shughuli za uzalishaji zinahitaji mtu mwenye afya njema ambayo inaweza kukabiliana na kazi zote za uzalishaji.

Aliongeza kuwa shughuli za uzalishaji viwandani zinahitaji utulivu wa akili na sio mtu wenye msongo wa mawazo kwani anaweza kuingia kwenye hatari ya kupoteza maisha hasa kwenye matumizi ya mitambo au mashine.

"Ili kuepuka kuchukuliwa hatua za kisheria hasa kunapotokea malalamiko kutoka kwa wafanyakazi ambao wameacha kazi wakidai wameumia wakiwa kazini tunasisitiza kila mara waajiri kuwapima afya wafanyakazi wao sasa wengine hawatekelezi na wahakikishia Osha itaendelea kuchukua hatua," alisema Mwakajwanga.

Meneja wa Mamlaka ya Udhibiti wa Chakula na Dawa (TFDA), Rodney Alananga aliwahimiza wananchi kuzingatia matumizi bora ya bidhaa zinazozalishwa kwa kuhakikisha zina nembo yao.

Alananga aliwataka wananchi kuacha tabia ya kutumia bidhaa zilizopigwa marufuku licha ya kuwa zinauzwa kwa bei nafuu na badala yake kutumia bidhaa ambazo zimekidhi viwango vyote vya mamlaka zinazohusika na kuthibitisha ubora.

**"Ili kuepuka kuchukuliwa hatua za kisheria hasa kunapotokea malalamiko kutoka kwa wafanyakazi ambao wameacha kazi wakidai wameumia wakiwa kazini tunasisitiza kila mara waajiri kuwapima afya wafanyakazi wao sasa wengine hawatekelezi nawahakikishia Osha itaendelea kuchukua hatua," alisema Mwakajwanga.**

# Halmashauri yatenga bajeti taulo za kike kwa wanafunzi

**Na Grace Mwakalinga, MBEYA**

HALMASHAURI ya Wilaya ya Mbeya imetenga kiasi Sh.milioni 7.5 katika bajeti yake ya 2019/2020, kwa ajili ya ununuzi wa taulo za kike, (Pedi) ambazo zitatolewa kwa wanafunzi wa shule za sekondari.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, Mwalingo Kisemba alisema hayo jana wakati wa ufunguzi wa kampeni ya ulinzi wa mtoto yenye kaulimbiu inayosema, "Namlinda mtoto afurahie utoto wake, ujana wake," katika kata ya Tembela wilayani Mbeya iliyoandaliwa na vituo vya taarifa na maarifa kwa kushirikiana na TGNP- Mtandao.

Mwalingo alisema sababu ya halmashauri kutenga bajeti hiyo kwa ajili ya ununuzi wa Pedi kwa watoto wa kike inatokana na mazingira magumu waliyonayo watoto hao hasa wanaoishi kwenye mazingira magumu na kwamba wanashindwa kuhudhuria vipindi vya masomo wanapokuwa kwenye hedhi.

Alisema kutokana na umaskini wa familia baadhi ya watoto wa kike wameshindwa kutimiza ndoto zao na kukatisha masomo wakiogopa fedheha wanapokuwa hedhi kwani wanashindwa kununua pedi kwa ajili ya kujisitiri.

"Tunalishukuru shirika hili kwa kuelimisha umuhimu wa kutenga bajeti kwa ajili ya ununuzi wa taulo hizi za watoto wa kike kwani utaratibu huu katika halmashauri yetu haukuwapo, lakini kutokana na umuhimu huu tulianza kutekeleza katika bajeti ya mwaka 2018/2019 tulitenga kiasi cha Sh. milioni 1.6 na sasa bajeti ya mwaka 2019/2020 tumetenga kiasi cha Sh. milioni 7.5, naamini kiasi hiki hakiwezi kuwahudumia wanafunzi wote, tunaendelea kuwashirikisha wadau ili watushike mkono," alisema Kisemba.

Alisema katika kampeni hiyo, wazazi pamoja na wadau wengine wawajibike katika kumlinda mtoto hasa wa kike dhidi ya vitendo vya ukatili wa kingono ili aweze kutimiza ndoto zake.

Alisema miongoni mwa mambo ambayo yataimarisha ulinzi wa mtoto ni kumtimizia mahitaji yake hasa kumnunulia nguo za ndani ikiwamo pedi ili asipate vishawishi vya fedha kwa wanaume.

Ofisa Maendeleo ya Jamii Kata ya Tembela, Nestory Maguja alisema Kata yake bado inakabiliwa na changamoto ya ulinzi wa mtoto kwani amekua akipokea malalamiko juu ya wazazi kutelekeza familia na kwenda kunywa pombe vilabuni.

Alisema wazazi hutelekeza familia zao na kwenda kulewa pombe huku watoto wakishinda njaa hali inayosababisha kuwa ombaomba au kujiingiza kwenye vitendo vya wizi.

Mwenyekiti wa Vituo vya Taarifa na Maarifa Wilaya ya Mbeya, Flora Mlowezi alisema kwa kutambua umuhimu wa ulinzi wa mtoto hasa wa kike wamekuwa na utaratibu wa kununua pedi .

Alisema taulo hizo wanazogawa katika shule mbalimbali za sekondari katika Wilaya hiyo, lakini pia hutoa elimu ya masuala mbalimbali ya ukatili wa kijinisia, uwajibikaji wa wananchi na viongozi na utawala bora.



Kikundi cha ngoma za asili kikitoa burudani kwenye ufunguzi wa kampeni ya ulinzi wa mtoto katika Kata ya Tembelela, Wilaya ya Mbeya. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Askofu ahubiri amani kwa watu wote

**Na Grace Mwakalinga, MBEYA**

ASKOFU wa Kanisa la Anglikana Jimbo la Mbeya, Julius Lugendo, amewataka Watanzania kuendelea kudumisha amani, ili kuweza kufikia malengo ya kuwa na uchumi wa kati, na kwamba amani inapaswa kutunza na kuhifadhiwa.

Alitoa kauli hiyo juzi wakati akifungua tamasha la kuendelea kudumisha amani nchini.

Alisema maendeleo yeyote hayawezi kufanyika pasipokuwa na amani na kusisitiza wananchi kuwa mabalozi wa kusambaza amani iliyopo ili wawe huru kufanya shughuli zao na kufikia azma ya serikali ya viwanda na uchumi wa kati.

"Tanzania ni kisiwa cha amani ndio maana hata viongozi wetu wa nchi hupokezana uongozi kwa amani lakini kusingekuwa na amani wangeng'ang'ania madaraka na kuleta machafuko tuendelee kupendana na kusambaza amani,"alisema Askofu Lugendo.

Tamasha hilo la amani, lenye kauli mbiu "isemayo sambaza amani tunza nchi yako" litawashirikisha waimbaji maarufu wa nyimbo za injili, kwaya kutoka jijini Mbeya, ngoma za asili na wasanii.

Kupitia tamasha hilo wananchi wametakiwa kupendana na kutakiana mema kuachana na chuki na visasi ambavyo vinaweza kuhatarisha amani ya nchi.

Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Mbeya mjini, Afrey Msomba, alisema chama hicho kimekuwa mstari wa mbele kuhubiri amani kupitia vikao na mikutano mbalimbali wanayoifanya.

Alisema hata Rais Magufuli kupitia vikao na mikutano mbalimbali amekuwa akiwasisitiza wananchi kudumisha amani na kukemea mtu yeyote anayepanga kuleta vurugu.





# Mkurugenzi AFNET ataja changamoto ukatili kijinsia

**Na Elisante John, SINGIDA**

MKURUGENZI wa Shirika la AFNET Tanzania linalojihusisha na matatizo ya kijamii na kuyatafutia ufumbuzi, Sarah Mwaga, amesema kukosekana kwa vituo vya huduma jumuishi kwa jamii (one stop center), kunakatisha tamaa wenye kipato duni kufuatilia mashauri ya ukatili wa kijinsia

Aliyasema hayo hayo juzi wakati wa mafunzo kwa asasi za kiraia, watendaji wa kata, jeshi la polisi, mahakimu, madiwani na wakuu wa idara wa Halmashauri ya Wilaya ya Singida.

Lengo la mafunzo hayo lilikuwa ni kutengeneza mfumo imara wa ulinzi kwa watoto na wanawake walio kwenye hatari ya kufanyiwa vitendo vya ukatili wa kijinsia, kuchambua sera na sheria zinazowakandamiza, ili kujua nini kifanyike kwa kuzingatia mazingira ya wilaya hiyo.

Aidha, mkurugenzi huyo alisema kuwa kukosekana kwa vituo vya huduma hiyo kunachochea vitendo vya ukatili ikiwemo ukeketaji, ubakaji na ulawiti nchini.

Kutokana na changamoto hizo, Mwaga aliziomba asasi za kiraia, halmashauri za wilaya na wadau wengine wanaojihusisha na mapambano hayo, kuongeza juhudi zaidi ya kutoa elimu na kusogeza huduma muhimu kwa jamii ili kumaliza tatizo hilo.

"Hili ni tatizo kubwa sana na wote kwa pamoja tunapaswa kuungana ili kulikabili, vyombo vya dola navyo visimamie kwelikweli utekelezaji wa sera na sheria za nchi bila ya upendeleo na vitoe haki ili kumaliza tatizo hili hapa nchini,"alisema.

Mmoja wa washiriki hao ambaye ni diwani wa Kata ya Msisi, Emmanuel Sima, aliiomba jamii kubadilika kimtazamo kwa kuweza kuwafichua wote wanaojihusisha na vitendo vya ukatili wa kijinsia, badala ya kumaliza kesi zao kwa njia ya maridhiano ndani ya familia.

Alisema njia hiyo itasaidia kumaliza tatizo la ukatili wa kijinsia, kutokana na hatua kali kuchukuliwa na mamlaka husika, ikiwamo adhabu stahili kutoka kwa vyombo vyenye dhamana ya wananchi.

Katika kuhakikisha tatizo hilo linadhibitiwa, wajumbe hao waliunda mpango kazi wa kukabiliana na vitendo vya ukatili wa kijinsia kwenye halmashauri hiyo iliyopo kwenye mkoa huo ambao ni kati ya mikoa mitano nchini inayoongoza kwa vitendo vya ukeketaji kwa wasichana na wanawake.

Tanzania ina mpango wa kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto kupunguza hadi asilimia 50 ifikapo mwaka 2022, ukiwa ni sehemu ya utekelezaji wa sera ya maendeleo ya wanawake na jinsia (2000); mkakati wa taifa wa maendeleo ya jinsia (2005); sera ya maendeleo ya mtoto (2008); sheria ya makosa ya kujamiiana(1998).

# Maambukizi VVU yapiga kambi Nyanda za Juu Kusini

**Na Mwandishi Wetu, DODOMA**

TAARIFA ya utafiti wa viashiria na matokeo ya Virusi Vya Ukimwi ya mwaka 2016/2017 inaonyesha kuwa maambukizi ya ugonjwa huo yamejikita kwa watu wenye umri kati ya miaka 15 hadi 49.

Hayo yalisemwa jana na Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge, Kazi, Ajira na Watu wenye Ulemavu, Jenista Mhagama wakati akizindua taarifa ya utafiti wa viashiria.

Alitaja mikoa vinara wa maambukizi ya ugonjwa huo kuwa ni pamoja na Njombe, Iringa, Mbeya pamoja na Kagera.

Mhagama alisema mikoa hiyo ndiyo imeonekana kuwa na asilimia kubwa katika maambukizi ya VVU nchini katika umri huo ukilinganisha na mikoa mingine kwa mujibu wa utafiti.

Alisema kuwa katika utafiti huo unaonyesha kuwa mkoa wa Njombe maambukizi ni asilimia 11.6, Iringa asilimia 12.2, Mbeya asilimia 9.2 na Kagera 6.8.

Aliitaja pia mikoa minne ambayo maambukizi yake yapo chini zaidi kuwa ni Lindi asilimia 0.3, Manyara 1.8, Arusha 1.6 na Mtwara 2.1.

Aidha, alisema kuwa serikali bado inaendelea na jitihada za kutoa elimu katika maeneo mbalimbali ya nchi ili kuweza kupambana na maambukizi mapya ya virusi vya ukimwi nchini.

"Kutokana na utoaji wa elimu pamoja na jitihada mbalimbali zilizofanyika na serikali pamoja na wadau mbalimbali wa masuala ya Ukimwi, Tanzania umepunguza vifo vitokanavyo na ugonjwa huo kutoka 70,000 hadi 32,000 kwa kiwango hicho si haba tunastahili tujipongeze,"alisema Mhagama.

Alisema kuwa kwa mujibu wa takwimu hizo, maambukizi mapya ya VVU katika umri wa kati ya mika 15 hadi 49 yameshuka kutoka asilimia 5.1 kwa mwaka 2012 hadi asilimia 4.7 kwa mwaka 2016/2017.

Mkurugenzi Mtendaji wa Tume ya Kudhibiti Ukimwi Nchini (TACAIDS), Dk. Leonard Maboko, alisema kuwa utafiti unaonyesha kuwa zaidi ya 500,000 ya watu wanaoishi na VVU nchini hawajui hali yao ya maambukizi.

"Juhudi za pamoja zenye wigo mpana zinahitajika kuwafikia watu wanaoishi na VVU ambao bado hawajapima na kujua hali zao na kuanza dawa," alisema Dk. Maboko

Dk. Maboko alisema kuwa kila mwaka takribani watu 72,000 wanapata maambukizi mapya ambapo kiwango cha wanaume kujua hali ya maambukizi ya VVU kipo chini kuliko wanawake ambapo wanaume ni asilimia 52 na wanawake asilimia 65.3.



Baadhi ya wananchi wakisaidia kuhamisha bidhaa za maduka kwenye nyumba iliyokuwa inaungua moto katika eneo la One way, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Wakulima alizeti wafundwa kufikia soko la kimataifa

**Na Mwandishi Wetu, DODOMA**

WAKULIMA wa zao la alizeti nchini wameshauriwa kutumia mbinu za asili ili kuwawezesha kukidhi vigezo vya kufikia soko la kimataifa katika nchi za Ulaya na India

Ushauri huo ulitolewa jana na Kaimu Katibu Tawala Mkoa wa Dodoma, Happines Mgalula wakati wa ufuguzi wa warsha ya tathmini ya athari za mabadiliko ya tabianchi katika mnyororo wa thamani wa zao la alizeti iliyofanyika chini ya shirika la maendeleo la Uholanzi SNV.

Mgalula, alisema wakulima wa zao hilo wanashauriwa kuzalisha kwa kutumia mbinu za asili ili kuweza kukidhi vigezo vya soko la kimataifa katika nchi za Ulaya na India.

"Alizeti ni miongoni mwa mazao yaliyopewa kipaumbele kuzalishwa hapa nchini kutokana na umuhimu wake katika kuongeza upatikanaji wa mafuta ya kula ndani na nje ya nchi hivyo tutumie mbinu za asili katika kuzalisha zao hili" alisema.

Alizitaja mbinu hizo kuwa ni kutumia mbolea za asili katika kupanda na mbegu bora pamoja na kutumia viuatilifu vinavyoshauriwa na wataalamu wa kilimo kwa kila eneo husika.

Alibainisha kuwa zao hilo limepewa kipaumbele kuzalishwa hapa nchini kutokana na umuhimu wa kuongeza mafuta ya kula ambapo linachangia asilimia 51 ya mafuta yote yanayozalishwa na asilimia 40 ya mafuta yote yanayotumiwa hapa.

Aidha, alisema mahitaji ya mafuta ya kula kwa sasa hapa nchini yanakadiriwa kuwa kati mita za ujazo 300,000 hadi 400,000 na kutokana na ongezeko la idadi ya watu mahitaji haya yataendelea kuongezeka kila siku. Alisema kwa Dodoma zao la alizeti ni zao la kimkakati kuelekea kwenye ujenzi wa uchumi wa viwanda kwani tayari kuna viwanda 432 kati ya hivyo vikubwa vya kusindika alizeti ni sita, kati 19 na vidogo 407.

Msimamizi wa mradi wa kilimo shirika la SNV, Godfrey Kabuka, alisema mabadiliko ya tabia nchi yamesababisha upungufu wa mvua, maji, ukame na mafuriko ya mara kwa mara na ongezeko la joto kwa baadhi ya maeneo.

Kabuka alisema mradi huo wa kilimo wa shirika la SNV unafadhiliwa na Wizara ya mambo ya nje ya nchini ya Uholanzi kwa kuwasaidi wakulima wa nchi za Tanzania, Kenya na Uganda ili kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi yaliyojitokeza.

Aidha, alisema warsha hiyo ya siku mbili inashirikisha Wasindikaji, wadau wa kilimo cha alizeti kutoka Mikoa ya Dodoma, Katavi, Mbeya, Songwe na Singida kwa lengo la kufanya tathimini ya athari za mabadiliko ya tabia nchi .

Kadhalika, alisema mabadiliko ya tabianchi yamesababisha mabadiko ya hali ya hewa na kusababisha upungufu wa maji na kuongezeka kwa wadudu na magonjwa ya mimea mbalimbali.

Kwa upande wake Mtafiti wa masuala ya Tabianchi kutoka Nchini Kenya, Dk. John Recha alisema mabadiliko ya tabi ya nchi yameathiri nchi nyingi duniani zikiwamo za Afrika Mashariki.





# Unyanyapaa wadumaza juhudi za kupambana na VVU

**Na Mwandishi Wetu, ZANZIBAR**

KUONGEZEKA kwa maambukizi mapya ya Virusi vya Ukimwi (VVU), kumeelezwa kuwa kunachangiwa na kuwapo kwa hali ya unyanyapaa kwa jamii.

Akizungumza na Nipashe, Ofisa Habari, Mawasiliano na Uhamasishaji wa Tume ya Ukimwi Zanzibar, Sihaba Saadat, alisema bado baadhi ya watu wanashindwa kujitokeza kuzungumzia hali zao wakihofia kunyanyapaliwa.

Alieleza kuwa bado elimu inahitajika zaidi kwa jamii kuacha kuwanyanyapaa watu wanaoishi na virusi vya Ukimwi ili kuweza kufikia lengo la kutokomeza ugonjwa huo.

"Kama jamii haitokuwa tayari kutowanyanyapaa waathirika wa ugonjwa huo, hali ya maambukizi itaongezeka wakati hatutaki hali hiyo iongezeke tunataka Zanzibar bila ya kuwa na Ukimwi au maambukizi mapya ya VVU," alisema.

Aidha, aliitaka jamii kuwa na tahadhari ya kujikinga na ugonjwa huo na kuacha kufanya anasa na kutumia kondom wakati wa tendo la ndoa ili kuweza kulinusuru taifa na maambukizi mapya ya Virusi vya Ukimwi.

Naye Mratibu wa ushauri nasaha na upimaji wa Virusi vya Ukimwi kanda ya Unguja, Tuwera Amour, alisema kuna haja ya mama wajawazito wanapojigundua kuwa wameambukizwa kwenda kliniki mapema ili kuchunguzwa afya zao.

Alisema kuhudhuria kliniki mapema kunaweza kumlinda mtoto na maambukizi ya VVU.

Kwa upande wake, Mkuu wa Sera na Mipango kutoka Tume ya Ukimwi, Halima Ali Mohammed, alisema wasichana wengi hivi sasa wako katika hatari ya kupata maambukizi ya VVU kutokana na kufanya mapenzi kinyume na maumbile kwa kuhofia kupata ujauzito au kupoteza usichana wao.

Alisema kwa mujibu wa shirika la umoja wa mataifa linaloshuhulikia watoto duniani (UNICEF) ni asilimia 39.7 tu ya vijana wa Zanzibar ndio wanaofanya ngono ndani ya ndoa na waliobakia wanafanya ngono kabla ya ndoa hali ambayo ni hatari kwa maisha yao.

# Waziri ataka ushirikiano kutokomeza udhalilishaji

**Na Mwandishi Wetu, ZANZIBAR**

WAZIRI wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Riziki Pembe Juma ameitaka jamii kushirikiana na mamlaka zinazoshughulikia masuala ya udhalilishaji ili kuondoa aibu na kutokomeza vitendo hivyo.

Alisema hivi sasa kuna wimbi kubwa la watoto wanaofanyiwa vitendo hivyo jambo ambalo linaweza kuwakosesha haki zao za msingi ikiwamo haki ya kupata elimu.

Aliyasema hayo wakati akifungua warsha ya kujengea uwezo wakuza mitaala wa vyuo vikuu na taasisi za elimu Zanzibar katika ofisi za Mtakwimu Mkuu wa Serikali zilizopo Mazizini nje kidogo ya mji wa zanzibar.

Alisema ni vyema kuondoa muhali na kuacha kuwapa hifadhi wahalifu wa vitendo hivyo kwani kutasaidia watoto kuishi katika mazingira salama.

Aliongeza kuwa kuna baadhi ya walimu na wanafunzi wa vyuo vikuu Zanzibar hawajielewi, hawajitambui na hivyo kufanya vitendo ambavyo haviendani na maadili ya nchi.

"Niwaombe washiriki mtoke na maazimio ya pamoja ya kupinga vitendo vya udhalilishaji hasa katika sekta ya elimu ili taifa kuwa na watoto imara watakaoiongoza nchi yao,"alisema waziri huyo.

Aidha, alisema kuwa masuala ya mitaala ndio miongozo yenye mpangilio wa mambo kwa wanafunzi ambao wanatakiwa kusaidiwa na kujua hatua sahihi katika kupata taaluma.

Aliwataka wakuza mitaala hao kujua vyema sera ya elimu na msimamo wa wizara hiyo juu ya maudhui ya namna ya kuyaingiza masuala ya udhalilishaji katika mitaala yao.

"Elimu ya udhalilishaji inahitajika kwa wanafunzi shuleni ili kujua mbinu za kuepuka na vitendo hivyo ambapo chanzo kikubwa kwa wanafunzi ni ushawishi, " alisema.

Naye Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Dk Idrisa Muslim Hija, aliwataka washiriki wa warsha hiyo kujadili kwa kina juu ya vitendo vya udhalilishaji hasa kwa watu wenye mahitaji maalum ili kuwasaidia katika kuondokana na janga hilo.

Warsha hiyo ya siku sita imeandaliwa na kitengo cha elimu mjumuisho na stadi za maisha cha wizara ya elimu na mafunzo ya amali, kwa kushirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu (UNESCO).



Mama akiwa amejitwisha mzigo wa chupa tupu za plastiki, akizipeleka kuziuza ili ajipatie riziki, katika eneo la Tandale, jijini Dar es Salaam jana.
**PICHA: MIRAJI MSALA**

# RC ataka vijana kuwa wabunifu

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

MKUU wa Mkoa Mjini Magharibi, Ayoub Mohammed Mahmoud, amewataka vijana kuwa wabunifu kwa kutumia fursa mbalimbali zilizopo katika kujiajiri ili kujiendeleza kiuchumi na kuimarisha ustawi wa jamii.

Ayoub aliyasema hayo katika ghafla maalum ya kusheherekea kutimia miaka mitatu ya umoja wa kikundi cha wireless services group inayojishughulisha na utoaji wa huduma katika shughuli na mikutano mbalimbali.

Alisema vijana wanapaswa kupanua wigo kwa kutafuta shughuli za kujiajiri na kuacha mtazamo wa kutaka kuajiriwa na serikali.

Aliongeza kuwa iwapo watatumia fursa hizo wataondokana na hali ya utegemezi na hatimae kujihusisha katika mambo yasiofaa hususani matumizi ya dawa za kulevya.

Aidha, aliupongeza uongozi wa umoja huo kwa kuamua kujikusanya pamoja na kuweza kujiajiri.

"Mnachokifanya ni sawa na kuunga mkono kwa vitendo juhudi za serikali za kuwataka vijana kujishughulisha na shughuli zenye staha"alisema.

Ayoub alisema serikali ya Mkoa wake itaendelea kushirikiana kwa karibu na vijana ili kuona wanakua na shughuli za kufanya ambazo zinakubalika kisheria na kuweza kujiletea maendeleo wao na familia zako.

Akisoma risala ya kikundi hicho, Rashid Ali alisema madhumuni ya kuanzishwa kwa kikundi hicho ni kuweza kutoa ajira kwa vijana ili kuenda sambamba na adhma ya serikali ya kuwataka vijana kutafuta mbinu za kujiajiri na kuacha kutegemea ajira kutoka serikalini.

Alisema kikundi hicho pia kimedhamiria kuanzisha miradi mbali mbali ambayo itaweza kuwaongezea kipato kama vile kutafuta vifaa ambavyo wataweza kukodisha na kuingizia fedha, kuwapatia taaluma ya utoaji wa huduma kwa wanachama wa kikundi pamoja na kufanya usajili wa kudumu kwa kikundi hicho.

**"Mnachokifanya ni sawa na kuunga mkono kwa vitendo juhudi za serikali za kuwataka vijana kujishughulisha na shughuli zenye staha,"alisema.**

## HABARI KIMATAIFA

## Afrika Kusini yatakiwa kuwakamata wanaoua wageni

**JOHANESSBURG,** Afrika Kusini

SHIRIKA la Kutetea Haki za Binadamu Ulimwenguni (HRW) limeitaka serikali ya Afrika Kusini kuwakamata na kuwafungulia mashtaka waliohusika na visa vya mauaji na mashambulizi dhidi ya raia wa kigeni nchini humo.

Ripoti ya HRW ilieleza kwamba katika muda wa siku tatu kuanzia Machi 25 hadi Machi 27, makundi ya watu waliokuwa na vyuma na marungu walivunja nyumba za raia wa kigeni na kuwafukuza mjini Durban, Mashariki mwa Pwani ya Afrika Kusini na kisha kupora mali zao.

Shirika la Umoja wa Mataifa linalowahudumia wakimbizi, UNHCR, lilieleza kwamba watu sita waliuawa na kadhaa kujeruhiwa, hivyo kuzidisha hofu ya kuzuka tena kwa umwagaji damu wa raia wa kigeni katika taifa hilo ambalo masikini wasiokuwa na ajira wanawashutumu raia wakigeni kuchukua kazi zao.

Watu 88 raia wa Malawi walionusurika na mashambulizi hayo waliwaomba wawakilishi wa UNHCR kwamba wanataka kurudishwa nchini mwao, huku wengine wakiamua kurudi kwa hiari yao.

Mkurugenzi wa HRW nchini Afrika Kusini, Dewa Mavhiga, alisema kuwarudisha wakimbizi katika jamii zao bila ya haki na uadilifu kufanyika kwa mashambulizi waliyofanyiwa ni kutengeneza janga. **DW**

## AU yatishia kuisimamisha uanachama Sudan

**KHARTOUM,** Sudan

UMOJA wa Afrika (AU) umetishia kuisimamisha Sudan kufuatia mapinduzi yaliyotokea wiki iliyopita yaliyosababisha aliyekuwa Rais wa nchi hiyo, Omar al-Bashir kuondolewa madarakani na jeshi.

Katika taarifa yake, Baraza la Amani na Usalama la AU limesema ikiwa jeshi litashindwa kukabidhi madaraka kwa raia ndani ya siku 15, nchi hiyo itasitishiwa ushiriki na shughuli zote ndani ya umoja huo hadi pale amri ya kikatiba itakaporejeshwa.

Bashir ameitawala Sudan kwa miaka 30 kabla hajaondolewa madarakani wiki iliyopita kufuatia maandamano ya nchi nzima yaliyoanza mwezi Desemba.

Hata hivyo, umoja huo umesifu madai ya waandamanaji na kulaani hatua ya jeshi kuingilia na kufanya mapinduzi. AU ulio na wanachama 55 umeongeza kuwa serikali ya mpito ya kijeshi itakuwa ni tofauti namatakwa ya watu wa Sudan.

Umoja huo umekuwa na msimamo mkali kuhusiana na mapinduzi na uliwahi kuzisimamisha Misri na Jamhuri ya Afrika ya Kati mwaka 2013 kufuatia mapinduzi katika nchi hizo mbili. **DW**

# Daktari wa uzazi 'awapa mimba' wagonjwa 49

**AMSTERDAM,** Uholanzi

**Yanaonyesha yanathibitisha tuhuma kali kwamba Karbaat alitumia mbegu zake za kiume za uzazi katika kliniki yake.**

DAKTARI wa masuala ya uzazi nchini Uholanzi, Jan Karbaat aliyekuwa anashutumiwa kwa kupandikiza mbegu zake za uzazi kwa wagonjwa bila ridhaa yao, amethibitishwa kuwa baba wa watoto 49.

Vipimo vya vinasaba (DNA) vimefichua kuwa Dk. Karbaat aliyefariki dunia miaka miwili iliyopita, aliwapa mimba kinamama katika kliniki yake iliyopo katika eneo la Bijdorp, karibu na Rotterdam. Vipimo hivyo vilithibitishwa Ijumaa ya wiki iliyopita baada ya Jaji kuruhusu vitangazwe.

Mmoja wa mama wa mtoto aitwaye Joey, alisema: "Hatimaye amefunga ukurasa sasa anajua Karbaat alikuwa ndiye baba yake baada ya uchunguzi wa miaka 11 ninaweza kuendelea na maisha. Ninashukuru kwamba hatimaye ameelewa."

Tim Bueters, wakili ambaye aliwawakilisha watoto 49, alisema kuwa ameridhishwa na matokeo ya kesi baada ya miaka kadhaa ya kutokuwa na uhakika.

"Inamaanisha kwamba hatimaye imekuwa wazi kwa watoto ambao wanafanana," Bueters aliliambia shirika la utangazaji la NOS.

Dk. Karbaat alipelekwa mahakamani kwa mara ya kwanza mwaka 2017. Moja ya kesi hizo ilihusu mtoto ambaye alifanana kwa maumbile na Dk.Karbaat.

Mali za Karbaat zilichukuliwa kutoka kwenye nyumba yake baada ya kifo chake Aprili 2017 akiwa na umri wa miaka 89. Mwaka 2017 Jaji aliamuru kuwa vipimo vya vinasaba -DNA vinaweza kuchukuliwa na kuhifadhiwa kwa siri hadi matokeo zaidi ya kesi hiyo yatakapotolewa.

Februari mwaka huu, Mahakama ya Wilaya ya Rotterdam iliamua kuwa matokeo ya vipimo yanaweza kuwekwa hadharani.

"Yanaonyesha yanathibitisha tuhuma kali kwamba Karbaat alitumia mbegu zake za kiume za uzazi katika kliniki yake," ilieleza taarifa iliyochapishwa kwenye tovuti ya kampuni ya sheria ya Rex Advocates.

Kliniki ya Dk. Karbaat ilifungwa mwaka 2009 wakati alipotuhumiwa kuwa alikuwa na data zisizo sahihi kuhusu uzazi. **BBC**



Mwonekano wa Kanisa la Notre Dame baada ya moto kuunguza sehemu ya kanisa hilo. **PICHA: AFP**

# Moto wateketeza kanisa la miaka 850

**PARLIS,** Ufaransa

RAIS wa Ufaransa, Emmanuel Macron, amehaidi usaidizi wa kimataifa katika kulijenga upya kanisa kongwe la Notre Dame mjini Paris baada ya sehemu ya kanisa hilo kuteketea kwa moto na kuharibika.

Maofisa wa zimamoto walifanikiwa kuliokoa jengo hilo la historia lenye miaka 850, lakini paa na mnara wa jengo hilo vimeanguka, lakini moto huo ulidhibitiwa saa tisa baada ya kuanza.

Chanzo cha moto huo bado hakijajulikana lakini maofisa wanasema huenda ukahusishwa na ukarabati unaoendelea.

Kamanda Jean Claude Gallet alisema anachunguza mkasa huo, ambapo ofisa mmoja wa zimamoto alijeruhiwa wakati akikabiliana na tukio hilo.

Vyanzo mbalimbali kutoka mjini Paris vinaeleza kuwa moto mkubwa ulizuka katika kanisa hilo kongwe la Notre-Dame mjini Paris Ufaransa majira ya saa 12:30.

Jengo hilo ni moja ya makanisa maarufu na linalotembelewa na idadi kubwa ya watalii kutoka sehemu mbalimbali duniani kila mwaka.

Sehemu kubwa ya paa la majengo ya kanisa hilo yameteketezwa na moto, huku mwingine ukifanikiwa kuzimwa katika minara miwili ya kengele.

Wazima moto walifanya juhudi kuokoa vitu vya thamani vilivyoko ndani ya kanisa hilo na pia kuzuia mnara wa upande wa kaskazini kutoporomoka.

Maelfu ya watu walikusanyika katika barabara zilizo karibu na kanisa hilo kushuhudia mkasa huo, huku baadhi yao wakitokwa na machozi wengine wakiimba nyimbo za sifa na kumuomba Mungu.

Makanisa kadha nchini Ufarasa yalipiga kengele kuashiria tukio la moto huo.

Rais Macron ambaye alifika katika eneo la tukio alisema mawazo yake yako na waumini wote wa Kanisa Katoliki na Wafaransa wote kwa ujumla.

"Sawa na watu wengine nchini, nimesikitika sana kuona sehemu ya maisha yetu ya kila siku ikiteketea," alisema Rais Macron.

Msemaji wa kanisa hilo pia alikiri kuwa sehemu kubwa iliteketea. Mwanahistoria Camille Pascal alisema kuwa moto umeharibu sehemu kubwa ya kanisa.

"Kanisa hili limedumu Paris kwa takribani miaka 800. Matukio ya furaha na ya kusikitisha kwa karne kadhaa yamekuwa yakiadhimishwa kupitia mlio wa kengele za Notre Dame. Tunasikitishwa na kile kilichotokea na kile tunachojionea," alisema Pascal.

Meya wa Jiji la Paris, Anne Hidalgo, alitoa wito kwa wakazi kuheshimu mipaka iliyowekwa na maofisa wa zima moto ili kuwahakikishia usalama wao. **BBC**

# Mwisho kutumika stempu za karatasi Aprili 30

**Na Enock Charles**

KAMISHNA Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Charles Kichere, amesema Aprili 30, mwaka huu, itakuwa mwisho kwa bidhaa ambazo zimebandikwa stempu za karatasi kuwapo sokoni.

Kichere ameagiza bidhaa zote ambazo ziko sokoni katika awamu ya kwanza ya utekelezaji wa mpango huo unaohusisha sigara, mvinyo, pombe kali, bia na aina zote za vileo, ziwe zimebandikwa stempu za kielektroniki ifikapo Aprili 30, mwaka huu.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam, Kamishna Kichere alisema kuwa, kuna ongezeko la makusanyo ya ushuru ya Sh. bilioni 42.8 yaliyotokana na utekelezaji wa Mfumo wa Stempu za Kodi za Kielektroniki uliotozwa kwenye sigara, mvinyo, pombe lali, bia na aina zote za vileo ambao ulianza rasmi Januari 15, mwaka huu.

"Mfumo huu mpya wa stempu za kielektroniki umeonyesha mafanikio makubwa sana. Mwezi Machi mwaka huu tumekusanya ushuru wa bidhaa jumla ya Sh. bilioni 42.8 kutoka kwenye sigara, mvinyo, pombe kali, bia na aina zote za vileo wakati mwaka jana kipindi kama hicho tulikusanya Sh. bilioni 39.3. Kiwango hiki kinatarajiwa kuongezeka maradufu," alisema Kichere.

Alitoa mfano wa mzalishaji wa pombe kali aliyekuwa akilipa ushuru wa bidhaa kati ya Sh. milioni 140 hadi Sh. milioni 160 kwa mwezi, lakini baada ya kufunga mfumo wa stempu za kielektroniki amelipa Sh. milioni 274.

"Pia wapo waliokuwa wanalipa kati ya Sh. milioni 20 hadi Sh. milioni 30, lakini kwa sasa wanalipa Sh. milioni 85 hadi Sh. milioni 172 kwa mwezi," aliongeza Kichere.

Alibainisha kuwa, mfumo wa stempu za kodi wa kielektroniki unatekelezwa kwa awamu mbili, awamu ya kwanza inahusisha bidhaa za sigara, mvinyo, pombe kali, bia na aina zote za vileo wakati awamu ya pili ikihusisha bidhaa za vinywaji baridi, maji, juisi na CD/DVD, kwa sasa TRA inatekeleza awamu ya kwanza ambayo ilianza rasmi Januari 15, 2019 na awamu ya pili itaanza rasmi Mei Mosi, 2019.

"Stempu za kielektroniki, zinaruhusiwa kuendelea kuwapo sokoni hadi tarehe 30 Aprili, 2019 na baada ya hapo zitatakiwa kubandikwa stempu za kodi za kielektroniki kabla ya kuuzwa," alisema Kichere.



Balozi wa Uholanzi nchini, Jeroen Verheul (katikati), akiwa katika picha ya pamoja na Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Christopher Ole Sendeka (kulia), alipotembelea mkoani humo kujionea maendeleo ya kilimo yanayoratibiwa na Kituo cha Kuendeleza Kilimo Nyanda za Juu Kusini mwa Tanzania (SAGCOT), kushoto ni Mkurugenzi Mtendaji wa Sagcot, Geoffrey Kirenga. **NA MPIGAPICHA WETU**

# NEMC yajitosa kusimamia marufuku mifuko ya plastiki

**Na Mwandishi Wetu**

BARAZA la Taifa la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), limesema litatumia sheria kusimamia kwa ukali marufuku ya matumizi ya mifuko ya plastiki na kuwaomba wadau wote kutekeleza agizo la serikali kabla ya Juni Mosi, mwaka huu.

Akizungumza na waandishi wa kabari jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Dk. Samuel Gwamaka, alisema Sheria ya Mazingira na Kanuni zake vinazuia utengenezaji na matumizi ya kitu chochote kinachoharibu mazingira, ikiwa ni pamoja na mifuko ya plastiki.

"Marufuku hii ina maana kubwa sana katika ustawi wa mazingira ya nchi yetu. Usimamizi wa marufuku hii utaanzia ngazi ya mtaa hadi taifa maana katika ngazi zote hizi tuna ofisi za mazingira. Tutatumia sheria kwa nguvu zetu zote, bila ubaguzi. Tutatumia sheria bila kujali nafasi ya mtu katika jamii, cheo, rangi au mahali anakotoka," alifananua.

Hivi karibuni Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, alitangaza bungeni kauli ya serikali ya kupiga marufu mifuko ya plastiki na juzi Ofisi ya Makamu wa Rais, Wizara ya Muungano na Mazingira, iliandaa mkutano wa wadau jijini Dar es Salaam uliotangaza fursa za uwekezaji zinazotokana na marufuku hiyo.

Kufuatia matukio hayo, Dkt. Gwamaka amewashauri wadau wote kutekeleza agizo la serikali katika kipindi kilichowekwa ili kujiepusha na usumbufu utakao wakabili ikiwa watapuuza agizo hilo. "Kila mdau atimize wajibu wake kabla ya Juni 1, mwaka huu," alisisitiza.

Meneja Mkuu Msaidizi wa Kiwanda cha Kutengeneza Karatasi cha Mufindi, Mhandisi Gregory Chogo, alisema kiwanda chao kina uwezo wa kutosha wa kuzalisha malighafi za kutengeneza mifuko mbadala.

"Tamko la serikali limekuja wakati kiwanda chetu kiko katika hali nzuri ya uzalishaji wa karatasi ambayo ni malighafi muhimu katika kutengeneza mifuko mbadala. Tuna uwezo wa kuzalisha tani 4,500 kwa mwezi," alieleza.

Alisema marufuku ya aina hii imeishatolewa kitambo na serikali za Uganda, Rwanda na Kenya na kuongeza kwamba nchi hizo zimekuwa zikiagiza malighafi kutoka katika kiwanda chao.

Ameeleza mahitaji ya Tanzania ya malighafi ni kati ya asilimia 20-25 na kwamba kiasi kinachobaki kinasafirishwa nje ambako marufuku ya matumizi ya mifuko ya plastiki iliwekwa muda mrefu uliopita.

# Ndugai ahimiza usalama wa chakula, lishe

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

SPIKA wa Bunge, Job Ndugai, amezindua Jukwaa la Usalama wa Chakula na Lishe la Wabunge kutoka nchi 10 za Mashariki mwa Afrika, huku akihimiza umuhimu wa ushirikiano ili kujikwamua na tatizo la upungufu wa chakula.

Jukwaa hilo litaweka kipaumbele suala la usalama wa chakula na lishe ili kukabiliana na utapiamlo unaozikumba nchi hizo na kusababisha kudumaa kwa watoto.

Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO), ambalo limeandaa mkutano huo, limesema uzinduzi huo umekuja baada ya kubaini utapiamlo umekuwa kikwazo kwa maendeleo ya kichumi kwa nchi nyingi Afrika.

Inakadiriwa kuwa watoto wapatao milioni 58 Afrika chini ya umri wa miaka mitano ni wafupi na wamedumaa.

Limesema utapiamlo katika kipindi cha utoto umegharimu uchumi wa Afrika kwa asilimia 11 ya Pato la Taifa la nchi husika (GDP), kwa mwaka.

Akizindua jukwaa hilo juzi jijini hapa, Spika Ndugai, alisema ushirikiano kati ya nchi hizo utawezesha maeneo yaliyoathirika kwa njaa kupata chakula kutoka maeneo mengine.

Uzinduzi wa jukwaa hilo ulifanyika wakati wa mkutano wa kwanza wa aina yake wa wabunge kutoka Djibouti, Eritrea, Ethiopia, Kenya, Rwanda, South Sudan, Somalia, Sudan, Tanzania, Uganda na Bunge la Afrika Mashariki (EALA) na walianzisha kamati maalum ya ufuatiliaji wa masuala ya usalama wa chakula.

Aidha, katika mkutano huo walizindua pia Mpango wa Ushirikiano wa Kiufundi (FAO-IGAD) wa kusaidia utekelezaji wa majukumu ya jukwaa hilo.

Alisema hakuna nchi ambayo inaweza kuwa na maendeleo ya kiuchumi, kiutamaduni au yoyote yale kama haitaweza kujitosheleza kwa chakula.

Alisema yapo maeneo yenye tatizo la upatikanaji wa mvua za kutosha, hivyo maeneo hayo lazima utaratibu uwekwe kuhakikisha chakula kinapatikana kutoka maeneo mengine ambayo hayana upungufu huo.

Akizungumzia utekelezaji mkataba wa Malabo, nchi za Afrika zilikubaliana kuongeza bajeti ya kilimo hadi kufikia asilimia 10, Spika Ndugai alisema katika bunge linaloendelea mjini Dodoma, watatenga bajeti zaidi na zaidi katika eneo la chakula.

Akizungumza kwa niaba ya Spika wa EALA, Martin Ngoga, mbunge wa bunge hilo, Mathias Kasamba, alisema kuna umuhimu wa kujenga miundombinu mizuri ili kuwezesha usambazaji wa chakula kutoka eneo moja kwenda lingine kwa urahisi zaidi.


# MATANGAZO MCHANGANYIKO

NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0767 223311

## CHETI KIMEPOTEA



GRACE BANDIO anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S.0534/0021 kilichotolewa na ST. ANTHONY SEKONDARI mwaka 2001.

**Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.**

**Taarifa ya polisi: CD/LR/IR/RB/2437/2019.**

115183202

## CHETI KIMEPOTEA



**KISSA MWANDOLOMA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0418-0056** kilichotolewa na **LUTENGANO HIGH SCHOOL** mwaka 2009.

Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi: OB/RB/14181/2018

115182702

## WEBSITE DESIGN

Je ungependa biashara yako Ikuwe na kufikia watu wengi zaidi? Tembelea empire ICT tuna design website nzuri domain na hosting kwa bei nafuu.

Wasiliana Nasi

**0744 299 823/0677 066418**

Web: www.empireict.net

115182602

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKPIKI

**WANHOO** anatangaza kupotelewa na KADI YA PIKIPIKI yenye namba za usajili **MC 143 ALT.** Chassis namba **LBMPCJL37F1002625. Engine namba 25158FMI.** Rangi-RED. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DOM/TR/RB/19/282.**

115183501

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKPIKI

**FREDRICK ANDERSON** anatangaza kupotelewa na KADI YA PIKIPIKI yenye namba za usajili **MC MC 949** BJK. Chassis namba **L7GPCJLYXG4300728.** Engine namba **DY156FMIG6044435.** Rangi-RED. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.Taarifa ya polisi: **DOM/TR/RB/19/281.**

115183602

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu:+255 26 2324455
Fax: +255 26 232233
Barua Pepe ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA,
Tarehe 16/04/2019.

## TANGAZO


1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya Jumatano tarehe 17/04/2019 kampuni ya **A&H CONSTRUCTION CO. LTD** itasafirisha mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka MBEYA kuelekea **LIWETA(MBAMBA BAY)** gari hilo lenye namba za usajili: T503 DKA
2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:
   Urefu - mita 14.1m
   Upana - mita 3m
   Kimo - mita 410cm
3. NJia itakayotumika kutoka MBEYA hadi MAKAMBAKO kupitia SONGEA gari litasafiri muda wa mchana tu (kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.**

215182802

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA MAMBO YA NDANI**
**IDARA YA UHAMIAJI**

## OMBI LA URAIA



Taarifa imetolewa kwa Umma kuwa **FATEMA TUL KUBRA IOBALHUSSEIN FIDAHUSEIN,** mwenye picha hapo juu anaomba Uraia wa Tanzania kwa Mh. Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi. Utaifa wake ni MKENYA. Nchi anayotoka ni KENYA. Shughuli zake **MENEJA UENDESHAJI** ,na anwani yake ni S.L.P 38324 DSM, Yupo hapa nchini tangu 2016. Yeyote mwenye taarifa/sababu za kwanini mwombaji asipewe uraia wa Tanzania,atume taarifa ya maandishi kwa Kamishna Jenerali wa uhamiaji S.L.P 512 ,Dar es salaam.Kumb.-Na.DN.27053

115182602

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**MAGRETH ENOCK KASABA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T.882 DCL . TOYOTA RAUM** yenye chasis Na. **NCZ200081498** na Ingine **1NZB811667.**

Kwa atakaye iona atoe taarifa kituo cha polisi kilichopo karibu nae.

Taarifa ya Polisi. **IR/RB/1480/2019**

215182102

## KADI YA PIKIPIKI IMEPOTEA

**MOHAMED OMARI NDARO** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki yenye usajili wa **MC 861 BTU** aina ya FEKON. Chassis No. **LDAPA-JOB8HGB20934** na Engine No. **157FMI21F00934**

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

Taarifa Polisi. **MUH/RB/1301/2019.**

215183102

*Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku Tupigie 0767 223 311*

*KWA MATANGAZO MADOGO, MADOGO Tupigie 0767 223311*

JE UNAHANGAIKA PA KUUZA BIDHAA YAKO?

Nipashe

NI JIBU LAKO NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

*Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku Tupigie 0767 223 311*

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# KOMPANY ANA IMANI NA MKATABA MPYA MAN CITY



**MANCHESTER,** England

VINCENT Kompany amedai kwamba atasaini mkataba mpya na Manchester City kabla ya mwisho wa msimu huu.

Nahodha huyo wa City amejikuta msimu huu akishuhudia mechi nyingi akiwa benchi kutokana na kusumbuliwa na majeraha na amecheza mechi 20 tu katika michuano yote msimu huu.

Mkataba wake wa sasa unamalizika Juni mwaka huu na ilionyesha kwamba angemaliza kipindi chake cha miaka 11 ya kukaa hapo Manchester.

Licha ya hatima yake kutojulikana, Kompany amezungumzia kuhusu majaliwa yake na ana imani kwamba ataendelea kuvaa jezi ya Man City msimu wa 2019/20.

"Ndiyo, nitacheza msimu ujao," alisema akiiambia Goal.

"Mimi ni sehemu ya familia hii sasa, hivyo nitaendelea kuwapo hapa kwenye familia hii na naamini nitaendelea kuwapo hapa.

"Tunatakiwa kukubaliana au kutokubaliana, lakini haitabadilisha mahusiano yangu na klabu hii, naamini nitaendelea kucheza hapa.

# Emery: Nne bora sasa mikononi mwa Arsenal

**LONDON,** England

UNAI Emery amesema nafasi ya Arsenal kufuzu kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya ipo mikononi mwao, lakini akasema kuwa timu yake ilitakiwa kuutawala mchezo wote wakati wakiibuka na ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Watford waliomaliza wakiwa na wachezaji 10 uwanjani.

Arsenal ilichukua uongozi kwenye mchezo huo katika dakika ya 10 wakati golikipa Ben Foster alipofanya makosa wakati akiokoa mpira na akaugongesha kwenye mguu wa Pierre-Emerick Aubameyang na kujaa wavuni.

Dakika moja baadaye Troy Deeney alionyeshwa kadi nyekundu ya moja kwa moja baada ya kumpiga kiwiko, Lucas Torreira.

Ushindi huo wa 1-0 uliwapeleka Arsenal nafasi ya nne, ikifikisha pointi sawa na Chelsea, lakini ikiwa na mchezo mmoja mkononi.

"Nafasi yetu kwenye msimamo ni muhimu zaidi," alisema wakati akizungumza na waandishi wa habari.

"Nafasi ya nne ipo mikononi mwetu na kuweza kufuzu kwa michuano ya Ligi ya Mabngwa Ulaya tunaweza kuipata kwa kupigana uwanjani.

"Tuna kazi kubwa ya kufanya kuhakikisha kwamba kila mchezo tunaocheza tunautawala na kupata pointi zote tatu."





# *Carvajal afunguka kukosa furaha Real*

**MADRID,** Hispania

BEKI wa Real Madrid, Dani Carvajal amebainisha kwamba msimu huu ameshindwa kuonyesha kiwango chake na ameelezea hali ya sasa klabuni hapo inamfanya asiwe na furaha.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Hispania amekuwa na kipidi kigumu kwa 'Los Blancos' hao huku miamba hao wa Santiago Bernabeu wakiwa hawapo kwenye mbio za ubingwa wa La Liga na imetolewa kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya 16 na Ajax.

Akizungumza na Gazeti la Marca, Carvajal amezungumzia hali hiyo hapo Madrid, na amebainisha kwamba hajisikii vizuri, kwani ni wazi msimu huu watamaliza bila taji lolote.

Wakati alipoulizwa anajipa nafasi gani msimu huu kutokana na kiwango chake, alijibu: "Ninajipa mimi mwenyewe nafasi ya nne. Nikiangalia kiwango changu, naona sijafanya vizuri.

"Ni wazi kwamba, kiwango changu ni kibovu msimu huu, kwani sijawa katika ubora wangu ninaoutaka. "Umekuwa mwaka mbaya kwa Madrid, lakini ni wazi kwamba msimu ujao tunaweza kubadilisha hali hii, kwani hakuna anayeifurahia kwa sasa."

Baada ya kuondoka kwa Julen Lopetegui na Santiago Solari kufukuzwa na nafasi yake kupewa Zinedine Zidane, Carvajal amesema ana imani na kocha huyo kuirudisha timu katika zama zake.

## HABARI MICHEZO

# Chelsea, Real zapigana vikumbo Dortmund

**LONDON,** England

CHELSEA inapanga kushindana na Real Madrid katika mbio za kuwania kumsajili mchezaji kinda wa Borussia Dortmund, Alexander Isak, ambaye anafananishwa na gwiji wa Sweden, Zlatan Ibrahimovic.

Katika umri wake wa miaka 19, anachukuliwa kama mmoja wa wachezaji ambao watang'ara zaidi katika siku zijazo.

Isak alifunga mabao 12 katika Ligi Kuu ya Uholanzi na Gazeti la The Mirror limedai kwamba, Chelsea nao wanawania kumsajili mwishoni mwa msimu huu.

Amekuwa akifananishwa na Ibrahimovic kutokana na ukweli kwamba, staili yake ya uchezaji inafanana na mchezaji huyo wa zamani wa Manchester United na Paris Saint-Germain.

Chelsea kwa sasa inatafuta mshambuliaji mpya ambaye ataweza kuwa na uwezo wa kufunga mabao.

Mshambuliaji ambaye anayeicheza kwa mkopo, Gonzalo Higuain, ameshindwa kuonyesha kiwango chake tangu alipotua hapo Januari mwaka huu, huku Olivier Giroud akiwa hana uwezekano wa kuongezewa mkataba.

Hata hivyo, mbio za Chelsea za kuwani saini yake zitakumbana na kikwazo kutoka kwa Real Madrid ambao nao wamekuwa wakimwinda mchezaji huyo tangu mwaka 2016 wakati akiwa anaichezea AIK ya Sweden.




# BARCELONA YARUDI TENA KWA WILLIAN




**BARCELONA,** Hispania

BARCELONA bado inatarajia tena kutoa ofa kwa winga wa Chelsea, Willian wakati wakionyesha nia ya kutaka kumsajili mwishoni mwa msimu huu.

Vinara hao wa Ligi Kuu ya Hispania wanatafuta mrithi wa Philippe Coutinho, ambaye ameshindwa kuthibitisha kiwango chake baada ya ujio wa Ousmane Dembele.

Lionel Messi mara zote amekuwa akicheza winga ya kulia na kuifanya Barcelona kuhitaji winga mwingine wa kushoto.

Willian amekuwa akichukuliwa kama ndio jibu sahihi kwa kocha Ernesto Valverde kumaliza matatizo ya winga ya kutosha na wanaweza kumpata kwa bei rahisi mwishoni mwa msimu huu.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil ambaye kwa sasa ana umri wa miaka 31, ni wazi kwamba uwezekano wa kupewa mkataba mpya hapo Chelsea ni mdogo hasa kutokana na sera ya klabu hiyo ya kutowapa mikataba mirefu kwa wachezaji wenye umri zaidi ya miaka 30.

Ujio wa Willian hapo Barcelona maana yake ni kwamba utamaliza kipindi cha Malcom kukaa hapo Camp Nou.

Akiwa amecheza mechi tatu tu za ligi msimu huu, katika umri wake wa miaka 22, anaonekana ni wazi kwamba, ataondoka hapo.

# *Robertson: Bao la Salah limewazima wabaguzi*

**LIVERPOOL,** England

ANDREW Robertson amelisifu bao la kuvutia la mchezaji mwenza wa Liverpool, Mohamed Salah, kwa 'kuwafunga mdomo' mashabiki wanaendeleza vitendo vya kibaguzi wakati wakiibuka na ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Chelsea Jumapili.

Salah alifunga bao muhimu kwa Liverpool wakati wakipata mabao mawili ndani ya dakika tatu katika kipindi cha pili na kukifanya kikosi hicho cha Jurgen Klopp kukaa kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu England, EPL.

Kabla ya mchezo huo, Chelsea na Liverpool walidai kulisambazwa video kwenye vyombo vya habari vya kijamii, ambazo zilionekana kuonyesha mashabiki wengi wa klabu hiyo ya London wakiimba "Salah ni mshambuliaji," wakimzungumzia Mmisri huyo.

"Hiyo ndiyo namna ya kuwafunga mdomo," alisema beki huyo wa kushoto wa Liverpool, Robertson. "Si kitu kizuri lakini unakifuta kwa namna hiyo. Haikumwathiri yeye kwa ujumla - haikuonekana kama hivyo, alifanya hayo?

"Kwa kusikitisha watu wanatumia vitu kama hivi sasa kwa sababu inatokea mara nyingi sana. Raheem Sterling alisema siku nyingine kuwa njia pekee ya kuwafunga watu kama hawa ni kufunga mabao na kuwashinda.

"Lilikuwa bao zuri. Aliingia ndani na haraka alipiga, kila mmoja alijua liliingia."



# DONDOO SOKA MAGAZETI ULAYA




# AUBAMEYANG: AGUERO, SALAH WANASHIKIKA

## ●●● Ndiyo, kwa nini hapana, ninahisi kujiamini, mbio za Kiatu zinaendelea...

**LONDON,** England

STRAIKA wa Arsenal, Pierre-Emerick Aubameyang, ameelekeza akili yake katika kuwapiku Sergio Aguero wa Man City na Mohamed Salah wa Liverpool kwenye mbio za kuwania tuzo ya mfungaji bora, Kiatu cha Dhahabu Ligi Kuu England (EPL), kauli hiyo aki-itoa juzi baada ya bao lake moja kuipa timu yake ushindi wa 1-0 ugenini dhi-di ya Watford.

**Nyota huyo wa kimataifa wa Gabon, Aubameyang alimuwahi kipa Ben Foster aliyezembea kuwahi kucheza mpira aliorudishiwa na beki wa kulia, Daryl Janmaat, hivyo kuifanya Arsenal kupata bao hilo la mapema katika dakika ya 10 kwenye mechi hiyo iliyopigwa Uwanja wa Vicarage Road, ushindi ambao uliifanya 'Gunners' kupanda hadi nafasi ya nne kwenye msimamo wa ligi hiyo.**

Kadi nyekundu iliyotolewa kwa Troy Deeney muda mchache baada ya bao hilo, iliifanya Watford kuwa na mlima mgumu wa kupanda, lakini Javi Gracia aligongesha mwamba mara mbili, huku kipa Bernd Leno wa Arsenal akifanya kazi kuokoa hatari kutoka kwa Craig Cathcart na Adam Masina.

Arsenal ilikamatwa vilivyo na wachezaji hao 10 wa Watford katika kipindi cha kwanza, lakini hata hivyo kwa mara ya kwanza ilifanikiwa kumaliza bila kuruhusu bao ['clean sheet'] ugenini kwenye mechi ya EPL msimu huu, na kukipa kikosi hicho cha Unai Emery nafasi ya kukaa nafasi ya nne wakati huu wakijiandaa kuifuata Napoli kwenye mechi ya marudiano ya robo fainali ya Europa League Alhamisi.

Aubameyang sasa amefikisha mabao 18 kwenye EPL na sasa anazidiwa bao moja kutoka kwa Salah na Aguero, kwenye mbio za Kiatu cha Dhahabu wakati huu mshambuliaji mwingine wa Liverpool, Sadio Mane naye akiwa na idadi sawa na nyota huyo wa kimataifa wa Gabon.

Mshambuliaji huyo wa zamani wa Borussia Dortmund, Aubameyang aliibuka kinara wa ufungaji Bundesliga katika msimu wa 2016-17 baada ya kutupia mabao 31 na sasa anaona kuwapiku Aguero na Salah inawezekana licha ya mechi kubaki chache.

"Ndiyo, kwa nini hapana. Ninasikia kujiamini," Aubameyang aliiambia Sky Sports wakati alipoulizwa kama anaweza kutwaa Kiatu cha Dhahabu. "Mbio zinaendelea. Ninajua ni vita ngumu. Ninaamini kwamba nitaendelea.

"Nilijiamini. Ni muda mrefu nilitaka kufunga bao kama hili. Usiku wa leo [juzi], limepatikana. Nilijiamini. Kawaida makipa ukweli hawajui kama unakuja nyuma yao. Lilikuwa bao zuri kwangu, nimelipenda."

Aubameyang alicheza mwenyewe mbele kufuatia mshirika wake Alexandre Lacazette kusugulishwa benchi na mshambuliaji huyo akakiri angependa kucheza wakiwa washambuliaji wawili akiwa pembeni ya Mfaransa huyo.

Kipa wa Watford, Foster alikiri kwamba anastahili kulaumiwa kwa kufanya makosa makubwa kwa ushindi huo wa Arsenal, kufuatia kushindwa kuiwahi haraka pasi ya nyuma kutoka kwa Janmaat.

## ZISIKUPITE

### HAZARD, MANE WAIVURUGA REAL

REAL Madrid ina mipango miwili ya usajili - mmoja unajumuisha kumsajili mshambuliaji wa Chelsea na Ubelgiji, Eden Hazard, 28, na mwingine ni mpango wa "anasa" ambao unajumuisha kumsajili kiungo wa Manchester United, Paul Pogba na straika wa Liverpool, Sadio Mane, 27. ***(El Confidencial - in Spanish)***

### GUNDOGAN AITAMANISHA INTER

INTER Milan inavutiwa kumsajili kiungo Mjerumani Ilkay Gundogan, 28. ***(Tuttosport, via Calciomercato)***

### JUVENTUS KUMUWAHI UMTITI

JUVENTUS inajiandaa kuipiku Manchester United katika mpango wa kumsajili beki wa Barcelona, Mfaransa Samuel Umtiti, 25. ***(AS, via Manchester Evening News)***

### WATAJIWA DAU LA POGBA

MANCHESTER United imemwambia wakala wa Paul Pogba, Mino Raiola kuwa Real Madrid itapaswa kulipa pauni milioni 129.34 ili kuipata saini ya nyota huyo wa kimataifa wa Ufaransa mwenye umri wa miaka 26 kwa sasa. ***(Marca)***

### AZUA VITA UNITED, ARSENAL

ARSENAL na Manchester United zinamwania mshambuliaji wa Ajax, David Neres Campos, 22, wakati huu Chelsea na Everton pia zikivutiwa na Mbrazil huyo. ***(Sun)***

### COUTINHO APIGIWA HESABU

KIUNGO wa Barcelona, Philippe Coutinho, 26, anaweza kuwindwa na Chelsea kama 'Blues' itaondolewa kifungo cha usajili majira haya ya joto, tayari Mbrazil huyo ametupilia mbali kujiunga na Manchester United. ***(Sport)***

### RASHFORD KATIKA RADA BARCA

BARCELONA itamfuata mshambuliaji wa Manchester United na England, Marcus Rashford, 21, ikiwa na pauni milioni 1000, wakati huu Muingereza huyo akiwa amebakiza mwaka mmoja katika mkataba wake na miamba hiyo ya Old Trafford na akiwa bado hajasaini mwingine. ***(Mirror)***

### LYON KUMCHUKUA VIEIRA NICE

KIUNGO wa zamani wa Arsenal, Patrick Vieira, ambaye kwa sasa ni kocha wa Nice, ni miongoni mwa wanaowindwa kuifanya kazi hiyo Lyon. ***(Le Parisien - in French)***

### NYONGA KUMZUIA SUAREZ

KIUNGO Mhispania Denis Suarez, 25, anayeichezea Arsenal kwa mkopo akitokea Barcelona, amekuwa akisumbuliwa na nyonga, jambo ambalo linaweza kuzuia kufanikisha mpango wake wa kujiunga jumla na miamba hiyo Emirates. ***(Mail)***

### AGEUKA LULU VIGOGO EPL

NEWCASTLE United imejiunga katika mbio moja na Arsenal, Everton na Manchester City katika kuonyesha nia ya kumsajili kiungo wa Burnley na England, Dwight McNeil, 19. ***(Star)***

### AANDALIWA DAU UNITED

MANCHESTER United inaandaa pauni milioni 31, zinazohitajika ili kuvunja mkataba wa beki wa Roma na Ugiriki, Kostas Manolas, 27. ***(Leggo, via Sun)***

HABARI MICHEZO

## Ligi ya wanawake Bara kuendelea leo

Na Mwandishi Wetu

LIGI Kuu ya Wanawake Tanzania ambayo ilisimama kupisha Timu ya Taifa (Twiga Stars) iliyokuwa kibaruani dhidi ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), inatarajia kuendelea leo katika viwanja sita mbalimbali hapa nchini kwa vinara JKT Queens kuwa ugenini kuwakabili Baobab Queens kwenye Uwanja wa Jamhuri Dodoma.

Akizungumza na gazeti hili jana, mahodha wa JKT Queens, Asha Rashid, alisema kikosi chao kiliwasili Dodoma tangu juzi na wachezaji wote wako tayari kwa mchezo huo wa raundi ya 17.

Asha alisema wamejipanga kuendeleza "ubabe" katika ligi hiyo yenye kushirikisha klabu 12 kutoka mikoa mbalimbali ili waendelee kukaa kileleni.

"Hakuna mechi rahisi, kila siku ligi yetu inaimarika, wachezaji wanapata uzoefu na wanaonyesha ushindani, yote kwa yote tumejipanga kuondoka na pointi tatu," alisema Asha.

Mechi nyingine za ligi hiyo ni kati ya Kigoma Sisterz watakaowakaribisha Simba Queens kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika ulioko Kigoma wakati Alliance Girls watavaana na Yanga Princess kwenye Uwanja wa Nyamagana jijini Mwanza.

Tanzanite Queens wao watawakaribisha Mlandizi Queens mchezo utakaochezwa kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini Arusha huku Marsh Queens wakiwa ugenini Njombe kupambana na Mapinduzi Queens kwenye Uwanja wa Sabasaba na Evergreen Queens watacheza na Panama FC kwenye Uwanja wa Karume, Dar es Salaam.

Ligi hiyo inayochezwa kwa mtindo wa nyumbani na ugenini itaendelea tena Jumamosi katika viwanja sita.

# SIMBA, YANGA ZAPANIA KUBEBA 3 UGENINI LEO

Na Somoe Ng'itu, TANGA

VIGOGO wa soka Tanzania, Simba na Yanga zote za jijini Dar es Salaam, zinatarajia kushuka kwenye viwanja viwili tofauti nchini leo katika muendelezo wa vita ya kuwania ubingwa wa Ligi Kuu Bara kwa kusaka pointi tatu muhimu katika ligi hiyo.

**Mabingwa watetezi, Simba wao watakuwa wageni wa Coastal Union katika mchezo wa ligi hiyo utakaochezwa kwenye Uwanja wa CCM Mkwakwani jijini hapa wakati vinara Yanga wao watakuwa kwenye Uwanja wa Jamhuri, Morogoro wakivaana na Mtibwa Sugar.**

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Simba, Patrick Aussems, alisema wamejiandaa vizuri kuelekea mchezo huo na wanaamini uzoefu walioupata katika mechi za kimataifa za Ligi ya Mabingwa Afrika utawasaidia kufanya vema zaidi.

Aussems alisema Simba inajua ligi pia ni ngumu na hawataidharau timu yoyote watakayocheza nayo kwa sababu wanaelewa kila upande umejiimarisha.

Alisema licha ya kikosi chake kuwa na changamoto, lakini watajipanga kufanya vema ili waweze kutetea ubingwa wa ligi hiyo ambao wanaushikilia.

"Tumefanya maandalizi mazuri kwa ajili ya mchezo huu, tunafahamu tumebakia na mechi za ligi tu ili kupata tiketi ya kucheza mashindano ya kimataifa mwakani, tukimaliza mechi ya kesho (leo), tutakuwa na michezo mingine minne katika siku nane, ni ngumu lakini tutakabiliana nayo," alisema Aussems.

Mbelgiji huyo aliongeza kuwa watakuwa makini kwa sababu wanaweza kukosa baadhi ya wachezaji kutokana na kuumia au kupata kadi za njano.

Naye Kocha Mkuu wa Coastal Union, Juma Mgunda, alisema kuwa anatarajia kukutana na ushindani katika mchezo wa leo kwa sababu wanakutana na timu yenye wachezaji wazoefu na ambao wametoka katika mashindano makubwa Afrika.

"Tuko tayari, tunajua wao wanahitaji pointi ili waweze kujiweka katika mazingira bora ya kutwaa ubingwa na sisi tunataka kukaaa mahali salama zaidi katika msimamo," alisema Mgunda baada ya kumaliza mazoezi ya asubuhi jana kwenye Uwanja wa Mkwakwani.

Katika mchezo wa leo Simba itawakosa Paschal Wawa, Juuko Murshid na James Kotei ambao ni majeruhi.

Wakati huo huo, Kutoka Morogoro, Kocha Mkuu wa Yanga, Mwinyi Zahera, alisema wanahitaji kushinda ili kuendelea kujiimarisha katika vita ya kuwania ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara ambayo bado nafasi iko wazi kwa timu tatu.

Zahera alisema Mtibwa Sugar ni timu nzuri na hasa inapocheza Morogoro, lakini kwa upande wake hana wasiwasi na kikosi chake.

Meneja wa Yanga, Hafidh Saleh, aliliambia gazeti hili kuwa katika mechi ya leo watamkosa beki wao wa kati, Kelvin Yondani ambaye alionyeshwa kadi nyekundu katika mchezo uliopita na Feisal Salum mwenye kadi tatu za njano.




Meneja wa Bia ya Castle Lager, Pamela Kikuli (katikati), Meneja Udhamini wa Kampuni ya Bia (TBL), David Tarimo (kulia) na Balozi wa Castle Lager Africa nchini Tanzania, Ivo Mapunda wakionyesha zawadi za washindi wa Bonanza la Wanawake mara baada ya mkutano na waandishi wa habari uliofanyika jijini Dar es Salaam jana. Bonanza hilo linatarajiwa kufanyika mwishoni mwa wiki katika Viwanja vya Leaders jijini Dar es Salaam. **NA MPIGAPICHA WETU**

# *Soka la wanawake ndani Castle Lager 5s*

Na Mwandishi Wetu

KAMPUNI ya Bia Tanzania (TBL) kupitia Bia yake ya Castle Lager, imetangaza fainali za mashindano ya soka ya Wanawake ya Castle Lager 5- Aside (wachezaji watano kila upande) yatakayofanyika Jumamosi Aprili 20, mwaka huu katika Viwanja vya Leaders jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, Meneja wa Bia ya Castle Lager Pamela Kikuli, alisema fainali za mashindano hayo zitashirikisha timu 16 kutoka vitongoji mbalimbali vya jijini Dar es Salaam.

Alisema mashindano hayo ambayo yanafanyika hapa nchini kwa mara ya pili, yamekuwa yakifanyika katika nchi nyingine za Afrika ambapo kwa mwaka jana Tanzania ilishiriki katika mashindano hayo katika kiwango cha kimataifa nchini Zambia kwa upande wa wanaume.

"Mwaka jana tuliyafanya kwa mara ya kwanza na kupata mwakilishi aliyeshiriki katika michuano ya kimataifa ya Afrika huko Zambia kwa kuzikutanisha timu kutoka Afrika Kusini, Zimbabwe, Swaziland Lesotho na wenyeji Zambia.

"Kwa mwaka huu, tunatarajia kuwa na mashindano bora zaidi yatakayotusaidia kupata washindani na mabalozi wazuri katika michuano ya kimataifa, hivyo tumeona ni vyema tukashirikisha na wanawake ili kuleta hamasa zaidi," alisema Kikuli huku akifafanua:

"Lengo ni kuwafikia wanywaji wa bia ya Castle Lager ikiwa ni pamoja na kuwapa fursa ya kutimiza ndoto zao."

Kwa upande wake, Balozi wa Bia ya Castle Lager, Ivo Mapunda aliishukuru Kampuni ya Bia nchini(TBL), kupitia bia ya Castle Lager kwa kuwashirikisha wanawake kwani kwa kufanya hivyo mashindano ya mwaka huu yatakuwa na msisimko wa hali ya juu na kuwaomba wakazi wa jiji la Dar es Salaam kujitokeza kwa wingi Viwanja vya Leaders kushuhudia fainali hizo.

Mapunda alizitaja timu shiriki kuwa ni Chinga Queens kutoka Kariakoo, Siza Sisters ya Kariakaoo pia, Tabata Queens (Tabata), Dragon (Mwananyamala), Bulyaga (Temeke), Mwangaza Queens (Temeke), Furaha Queens (Gerezani), Umoja Queens (Kidongo Chekundu), MRJ Queens (Mlandizi), Wema Dallas Queens (Mlandizi), Jupita (Buguruni Sukita), Mercury (Msimbazi), La Capilla (Mbagala), Santiago (Mbagala), Girls Queens (Msimbazi) na Msimbazi Queens ya Msimbazi.

Naye Meneja Udhamini, David Tarimo alizitaja zawadi za washindi kuwa bingwa atajinyakulia Kombe, medali za Dhahabu, Pesa taslimu Sh. 900,000 pamoja na kuiwakilisha nchi kwenye fainali za Kimataifa zinazotarajiwa kufanyika nchini baadaye mwaka huu.

Mwisho Kikuli aliwaomba wakazi wa jijini Dar es Salaam kujitokeza kwa wingi kushuhudia mashindano hayo ambayo yatakuwa na burudani kutoka kwa Msanii wa Bongo fleva, Maua Sama pamoja na Dj kutoka E.A.Redio, RDJ Mammy.

# Michezo

Jumatano Aprili 17, 2019

Nipashe




Aubameyang: Aguero, Salah wanashikika UKURASA 30



Beki wa pembeni wa Arsenal, Ainsley Maitland-Niles (chini), akifanya kazi ya ziada dakika za majeruhi kwa kuzuia shuti la mshambuliaji wa Watford, Andre Gray, wakati huo kipa wao, Bernd Leno akiwa ameshapotea. Katika mechi hiyo iliyopigwa Uwanja wa Vicarage Road, Arsenal ilishinda 1-0. **HABARI UK. 30**

# *Wanyama aihofia Taifa Stars Afcon*

●●● Asema ni kundi gumu kwa wote, azungumzia upinzani mkubwa zitakapokutana na Harambee Stars huku akifafanua...

**LONDON,** England

NAHODHA wa Timu ya Taifa ya Kenya 'Harambee Stars' na kiungo kisiki wa Tottenham Hotspurs ya Ligi Kuu England, Victor Wanyama, amesema mechi dhidi ya Taifa Stars katika michuano ya Afcon itakuwa ngumu zaidi kwao.

Stars imepangwa Kundi C pamoja na Kenya, Senegal na Algeria kwenye michuano hiyo itakayofanyika Misri Juni mwaka huu.

Harambee Stars itacheza na Stars Juni 27 jijini Cairo na huo utakuwa mchezo wa pili kwa timu hizo.

**"Ni kazi ngumu, nilifikiri hawa watu wanataka watu wa Afrika Mashariki wapigane," alisema kiungo huyo wa Tottenham Hotspurs akiiambia BBC Sport.**

"Najua itakuwa mechi ya watani wa jadi, wao (Tanzania) ni ndugu zetu na itakuwa mechi ngumu pia, lakini tupo tayari kwa changamoto hiyo.

"Hakuna hata timu moja ya kuidharau kwa sababu hadi kufuzu Afcon inakupasa uwe na timu imara, hivyo tumo kwenye kundi gumu. Tutajaribu kadri ya uwezo wetu kusonga mbele."

Wakati Kenya ilishiriki michuano hiyo mwaka 2004, Stars hii ni mara ya kwanza tangu mwaka 1980.

Mchezo wa kwanza wa Kundi C utawakutanisha Tanzania na Senegal Juni 23, huku Kenya wakicheza dhidi ya Algeria siku hiyo hiyo.

Tanzania itamaliza hatua ya makundi dhidi ya Algeria Julai Mosi na siku hiyo hiyo na muda huo huo Kenya watakuwa wanaumana na Senegal.

# Serengeti Boys: Ni zamu yetu leo

**Na Mwandishi Wetu**

ZAMU yetu leo! Hiyo ni kauli kutoka kikosi cha Timu ya Soka ya Taifa ya Vijana ya umri chini ya miaka 17 (Serengeti Boys), wakati kikielekea kuwakabili yosso wenzao wa Uganda katika mechi ya Kundi A ya fainali za Mataifa ya Afrika (Afcon U-17) itakayochezwa Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam leo.

Mechi hiyo ya Serengeti Boys itachezwa kuanzia saa 1: 00 usiku na wakati ile ya mwisho katika hatua ya makundi itakuwa Jumamosi dhidi ya Angola.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Serengeti Boys, Oscar Mirambo, alisema wameyasahihisha makosa yaliyotokea katika mchezo wa kwanza dhidi ya Nigeria na leo wataingia wakiwa makini zaidi.

Mirambo alisema wamejiimarisha katika safu zote na anaamini leo vijana wake wataingia wakiwa bora kuliko walivyozoeleka kwenye mechi zilizopita.

"Tunajua tuna mechi mbili zitakazoamua hatima yetu, hivyo tunahitaji ushindi tu, wale ni watoto na kamwe hutakiwi kuwakatia tamaa, mpira unamatokeo ya furaha na maumivu, tunaamini kesho (leo) itakuwa ni zamu yetu kufurahi," alisema Mirambo.

Aliongeza kuwa pia wataivaa Uganda huku wakiwa wanaifahamu baada ya kuwaona wakati wakicheza na Angola, hivyo wanajua ubora na udhaifu wao ulipo tofauti na walipokutana na Nigeria.

Naye kocha wa makipa wa timu hiyo, Manyika Peter, alisema ameshafanya yale aliyotakiwa kumweleza golikipa wake na anaamini ataingia akiwa ameiva zaidi.

"Unajua kuna wakati mchezaji anafanya kitu uwanjani kwa kutumia akili yake, na anafanya makosa yanayoigharimu timu, nimeongea naye na naamini sasa atakuwa akifanya yale tu niliyomwelekeza," alisema kipa huyo wa zamani wa Yanga na Taifa Stars.

Mechi nyingine ya kundi hilo itakayoanza saa 10:00 jioni itakuwa ni kati ya Angola dhidi ya Nigeria ambao tayari kila mmoja ana pointi tatu mkononi.

Michuano hiyo ambayo itatoa timu nne zitakazokwenda fainali za Kombe la Dunia za Vijana baadaye mwaka huu, zitaendelea tena kesho kwa Cameroon kuivaa Morocco na Senegal kuikaribisha Guinea, mechi zote zikichezwa kwenye Uwanja wa Azam Complex.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002